# BUNGE LA TANZANIA

# MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NNE

## Kikao cha Pili - Tarehe 7 Septemba, 2016

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu!

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Maswali, tunaendelea na Kikao chetu cha Pili katika Mkutano wetu wa Nne. Na swali letu la kwanza kwa asubuhi hii linaelekezwa kwa Ofisi ya Waziri Mkuu na linaulizwa na Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi.

Na. 16

### Ajira kwa Watanzania

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI** aliuliza:-

Nchi yetu kwa sasa ina wataalam wengi katika sekta mbalimbali kama vile uhasibu, uchumi, uongozi, menejimenti, udaktari, utawala na kadhalika.

Je, Serikali haioni haja sasa kwa ajira zote kwenye *NGOs* na taasisi binafsi nchini kupewa Watanzania na kuacha mpango uliopo sasa wa kuruhusu wageni kuajiriwa hasa kwenye nafasi za juu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wageni wanaajiriwa nchini kwa kuzingatia Sheria ya Ajira ya Wageni Namba Moja ya mwaka 2015. Kabla ya kutoa kibali cha kazi kwa mgeni kamishna wa Kazi anatakiwa kujiridhisha kuwa nafasi anayoombewa mgeni ni adimu na mwajiri amefanya juhudi za kutafuta Mtanzania wa kuajiriwa katika nafasi hiyo. Aidha, sheria inamtaka mwajiri kutengeneza mpango wa kurithisha ujuzi na kuhakikisha mgeni anayeombewa kibali anarithisha utaalamu huo kwa Mtanzania ili muda wa kibali utakapokwisha Mtanzania huyo aweze kuchukua nafasi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa utaratibu wa utoaji vibali vya ajira kwa wageni unazingatiwa ipasavyo kwa kutumia sheria na miongozo iliyopo. Kwa hali hiyo, Serikali itaendelea kuona haki inatendeka kwa mujibu wa sheria ili Watanzania waendelee kupata ajira katika *NGOs* na taasisi binafsi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mavunde, Mheshimiwa Ndaki.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nashukuru pia kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kama nilivyosema kwenye swali langu la msingi tuna wataalam wengi katika sekta mbalimbali kama nilivyozitaja; na watalaam hao wapo hapa nchini na wengine wanafanya kazi za chini zaidi kuliko viwango vyao vya utaalamu na ujuzi. Je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kurejea Sheria hii ya Ajira kwa Wageni ili kwamba Watanzania hawa ambao wana ujuzi kwenye maeneo tofauti tofauti waweze kupewa au kuajiriwa nafasi hizi za juu kwenye *NGOs* na taasisi binafsi zilizoko hapa nchini? Swali la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwenye majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri anasema mgeni anapoombewa kibali anarithisha utaalam kwa Mtanzania. Je, Serikali ina utaratibu gani wa kufuatilia kama kweli hawa watu walioajiriwa wanarithisha huo utaalam kwa Watanzania kwa sababu tunaona wanapewa hizi kazi halafu anaendelea kufanya kazi hizo miaka miwili, anamaliza mkataba anaongezewa miaka mitatu mingine, anaendelea nenda rudi. Sasa Serikali ina utaratibu gani wa ufuatiliaji juu ya jambo hili, ili kuhakikisha kwamba Watanzania ambao wako chini ya huyu ambaye atarithisha baadaye…

**MWENYEKITI:** Imeeleweka.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Wanapata hizi nafasi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza ameuliza Serikali haioni umuhimu wa kurejea sheria hii na ihakikishe kwamba inatekelezwa, ili Watanzania waajiriwe katika nafasi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema pale awali, Sheria hii Namba Noja ya mwaka 2015 ndio sheria ambayo inatusaidia katika uratibu wa ajira kwa wageni. Kwa hiyo, kabla ya mgeni hajaomba nafasi yoyote katika nchi yetu hii utaratibu ni kwamba, lazima Kamishna wa Kazi ajiridhishe juu ya ujuzi ambao mgeni huyo anao na nafasi ambayo anaiomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimuondoe hofu tu Mheshimiwa Mbunge ya kwamba tutaendelea kuisimamia sheria hii kuhakikisha kwa kwamba wale wageni wote wanaokuja na wenye ujuzi ambao unapatikana nchini, basi nafasi zao hizo wasipewe na badala yake Watanzania waweze kuchukua nafasi hizo. Hilo linafanyika na tumekuwa tukifanya kaguzi mbalimbali ambazo tumebaini baadhi ya wageni wengi ambao mwanzo walitoa taarifa za uwongo na baadaye baada ya kubaini kwamba, ni taarifa za uwongo tumefuta vibali vyao na nafasi zao wameendelea kupewa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali la pili, alitaka kujua ni utaratibu gani ambao huwa tunautumia katika urithishaji wa ujuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria Namba Moja ya mwaka 2015, inaeleza wazi ya kwamba, mgeni yeyote ambaye anapata kibali cha kufanya kazi lazima kitengenezwe kitu kinaitwa *succession plan* ambayo inawasilishwa kwa Kamishna wa Kazi ya kuona ni namna gani mgeni huyu amekuwa ana Mtanzania ambaye anamu-*understudy* na anajifunza kupitia kwake. Kwa hiyo, ziko fomu maalum ambazo zinajazwa na kuwasilishwa kwa Kamishna wa Kazi kuthibitisha kwamba ni kweli kuna Mtanzania ambaye yuko chini na kweli ananufaika na ujuzi wa mgeni huyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mlipaswa kusimama wakati mwenye swali la msingi aliposimama, tunaendelea. Swali la pili linaulizwa na Mheshimiwa Mary Pius Chatanda.

No. 17

**Mfuko wa PSPF Kuchelewesha Mafao ya Wastaafu**

**MHE. MARY P. CHATANDA** aliuliza:-

Mfuko wa *PSPF* unachelewesha sana mafao ya wastaafu, watumishi wengi waliostaafu mwaka wa fedha 2015/2016 hawajalipwa mafao yao, hususan walimu wa Korogwe Mjini:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuondoa changamoto hii ambayo imekuwa kero kwa wastaafu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mbunge wa Korogwe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha changamoto ya kulipa wafanyakazi mafao inaondoka, Serikali katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Agosti, 2016 imefanikisha mkakati wa kuweza kulipa kiasi cha shilingi bilioni 511.8 ikiwa ni malimbikizo ya michango ya mwajiri. Pia katika kipindi hicho Serikali imelipa jumla ya shilingi bilioni 83 kama malipo ya deni la kabla ya mwaka 1999 *(Pre 1999 Liability)*. Kwa hali hiyo, Serikali imeendelea kulipa malimbikizo ya madai ya wastaafu na mafao mengine yatolewayo na mfuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha katika kipindi cha mwezi Januari hadi Julai, 2016 mfuko umelipa mafao ya pensheni ya mwezi kwa kiasi cha shilingi bilioni 117 na kwa sasa mfuko unaendelea na kulipa malimbikizo ya mafao ya mkupuo kwa wastaafu wapya na mafao mengineyo.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa niulize swali la nyongeza. Wafanyakazi wamekuwa wakikatwa fedha zao na kupelekwa kwenye huu mfuko wa *PSPF*. Lakini wafanyakazi hawa wanapokuwa wamemaliza huo muda wanacheleweshewa kupewa mafao yao. Je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kuona kwamba, wafanyakazi hawa wanapomaliza muda wao wawe wanaandaliwa *cheque* zao mapema ili kusudi ziweze kuwasaidia katika kufanya shughuli zao wanazokuwa wamejipangia kuliko hivi sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, je, Mheshimiwa Waziri amejibu amesema wameshaanza kulipa; anaweza sasa akanisaidia mimi orodha ya Mkoa wa

Tanga, hususan Korogwe, wale ambao wamekwishalipwa ili wasiendelee kunieleza kwamba wanadai? Nipate ile orodha ili iweze kunisaidia.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, aah, naona Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, sahihi kabisa.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa swali lake la kwanza alilouliza kuhusu kucheleweshewa malipo, kama ambavyo Serikali imekuwa ikitoa majibu humu Bungeni ni kwamba kucheleweshewa huku hakutokani na Serikali, kunatokana na waajiri ambao wanachelewesha kufikisha nyaraka za wastaafu hawa katika Mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii. Hivyo, nitoe tu wito wangu kwa waajiri wote wajitahidi kupeleka nyaraka zote zinazostahili kwa wastaafu miezi mitatu au sita kabla mstaafu hajastaafu ili tuweze kulipa mapema iwezekanavyo. Wakiweza kufanya hivyo, Waheshimiwa Wabunge tunaweza kabisa mstaafu anapokuwa amestaafu nyaraka zake zimekamilika na *cheque* yake itaweza kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, Mheshimiwa Mbunge naomba nifanye kazi mimi na wewe kuhusu wastaafu wote wa Wilaya ya Korogwe wanaolipwa na Mfuko wetu wa *PSPF,* tunapomaliza Kikao hiki cha Bunge naomba tushirikiane ili upate orodha halisi ya waliostaafu na orodha halisi ya waliolipwa katika kipindi hiki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mhagama.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mussa Sima.

**MWENYEKITI:** Samahani endelea.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Naomba kuuliza swali la nyongeza, Serikali ina mkakati gani sasa kwa watumishi ambao wamestaafu kwa hiyari ama wengine wamebadilisha kazi kwa mfano kuwa Wabunge, ili kuendelea kuchangia Mfuko huu wa *PSPF* badala ya kuwaondoa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati uliopo kati ya Serikali na watumishi hawa, nadhani ni ndani ya mtumishi yeye mwenyewe kwamba kama anaona anaweza kuendelea kulipa anaweza kuongea na watumishi wa mfuko huu, Wakurugenzi wetu wote na wote wako tayari na wanapenda kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mussa Sima nikwambie mimi ni mmoja wa waliokuwa watumishi wa Serikali na sasa naendelea kuchangia malipo yangu baada ya mimi kwenda kuongea na Mkurugenzi wa Mfuko wa *PSPF* na sasa mimi naendelea kuchangia.

Kwa hiyo, nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge wote, Waheshimiwa Watumishi wote na Watanzania kwa ujumla wanaoona wanaweza kuendelea kulipa basi waende wafike kwenye mifuko hii na wataweza kuendelea kulipa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sima, samahani sikuwa nimekuona vizuri. Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Samahani. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwanza kabisa niwapongeze Waheshimiwa Naibu Mawaziri wote wawili kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama tu kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba sheria hizi za malipo ya pensheni na mifumo ya kuchangia katika mifuko ya pensheni zimehuishwa na sasa kila mtumishi wa umma ama mtumishi katika sekta binafsi anapohama kiajira kutoka ajira moja kwenda ajira nyingine ama anapotaka kuhamisha mafao kutoka mfuko mmoja kwenda katika mfuko mwingine kwa mujibu wa sheria sasahivi anaruhusiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni suala tu kila mtu kufikiria na kuona ni namna gani anataka kuendelea kuhuisha mafao yake na anaweza kuhusiaha katika mfuko wowote kwa kuhamisha kutoka mfuko mwingine kwenda mwingine kama anabadilisha ajira ama anaamua kufanya hivyo na sheria sasa hivi zinaturuhusu. *(Makofi)*

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kwa *pensioners* ambao hawalipwi kupitia Hazina moja kwa moja kwamba, vile viwango vipya vya malipo hawajaanza kulipwa mpaka hii leo. Na haya malalmiko yamekuwa ni ya muda mrefu sana. Naomba *commitment* ya Serikali ni lini wastaafu hawa wataanza kulipwa viwango vyao vipya pamoja na *arrears* zao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimekuwa nikiliarifu Bunge lako Tukufu ni kwamba watumishi wote ambao wanalipwa kupitia Hazina walianza kulipwa fedha zao za nyongeza tangu mwaka jana mwezi wa saba, 2015. Kwa mifuko ambayo haijaanza kulipa kama ambavyo nilisema mwanzo, nyongeza hizi, sasa hivi Bodi za Mifuko hii

zinamalizia kufanya maamuzi, ili waweze kuanza kulipa nyongeza ambayo ni ya 50,000 kama ilivyotangazwa na Serikali.

Na. 18

**Kushusha Madaraka kwa Wananchi**

**MHE. MARGARET S. SITTA** aliuliza:-

Kushusha madaraka kwa wananchi *(D by D)* ni jambo muhimu sana katika masuala muhimu yakiwemo elimu, afya na kilimo na kadhalika.

Je, Serikali haioni kuwa ni mapema mno kushusha elimu ya kidato cha tano na sita kwenda TAMISEMI kabla ya kurekebisha changamoto za elimu za awali, msingi na sekondari hadi kidato cha nne?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Jimbo la Urambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugatuaji wa madaraka *(Decentralisation by Devolution)* ni suala la Kikatiba kwa kuzingatia Ibara ya 145 na Ibara ya 146 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977 ambayo inatambua uwepo na madhumuni ya Serikali za Mitaa kuwa ni kupeleka madaraka kwa wananchi. Utekelezaji wake unafanyika kwa kuzingatia Sheria ya Serikali za Mitaa, Sura Namba 287 ambayo inazungumzia suala la Mamlaka za Wilaya na Sura Namba 288 - Mamlaka za Miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa kugatua elimu ya msingi na sekondari kwenda katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa ulikuwa ni kupeleka madaraka kwa wananchi ili kuwapa fursa ya kushiriki katika kusimamia na kuziendeleza shule hizo. Uendelezaji wa walimu kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa umewezesha kubaini changamoto mbalimbali na kuzipatia ufumbuzi kwa haraka ikiwa ni pamoja na miundombinu na masuala ya kiutumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifahamike pia kwamba uendeshwaji wa shule kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita hauwezi kutenganishwa kwa sababu sehemu kubwa ya shule hizo zina kidato cha kwanza hadi cha sita, lakini pia wananfunzi wanaofaulu kidato cha nne wanajiunga na kidato cha tano hapohapo shuleni au shule nyingine. Aidha, kwa kuzingatia matakwa ya

Kikatiba na juhudi kubwa ya Serikali katika kuboresha elimu ni wazi kwamba suala la kidato cha tano na kidato cha sita kusimamiwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI ni muafaka sana. Kinachotakiwa ni kuunga mkono juhudi kubwa za Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli katika ukusanyaji wa kodi ili kujenga uwezo wa kutatua changamoto za kibajeti zilizopo.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa suala la ubora wa elimu ni muhimu kusimamiwa na Wizara ya Elimu yenyewe; je, Serikali inasemaje kuhusu kuimarisha macho yake ambayo ni ukaguzi ili ijue kinachoendelea katika shule hizo ambazo naona mimi pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kugatua madaraka, lakini kule chini kumezidiwa, mmewapelekea kazi kubwa.

Je, Serikali ipo tayari kuimarisha ukaguzi kwa kuifanya iwe SU yaani chombo kinachojitegemea ili kifanye kazi kikamilifu?

(b) Serikali inasemaje kuhusu hizi shule maalum; inazisimamiaje baada ya kugatua madaraka? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, Waziri haya, Waziri wa Elimu.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kuhusu Serikali kuboresha ukaguzi, hilo suala la kuboresha ukaguzi ni dhamira ya Serikali kwa sababu tunatambua kwamba wakaguzi ndio jicho letu, ndio wanaotuwezesha kubaini changamoto zilizopo na utaona hata katika bajeti yetu kuna mambo mengi ambayo tumefanya ya kuboresha ukaguzi. Sasa suala la kufanya ukaguzi uwe ni wakala hilo suala tunaliangalia na kuona kwamba je, kuna changamoto gani katika muundo uliopo na kama Serikali itaona kuna umuhimu wa kubadilisha mfumo hakuna tatizo lolote kwa sababu lengo letu sisi ni kuhakikisha kwamba ukaguzi unafanya kazi yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la shule za wanafunzi wenye vipaji maalum, kama alivyojibu Mheshimiwa Jafo kama Serikali tunafanya kazi kwa pamoja. Kwa hiyo, usimamizi wa shule upo kwenye Ofisi ya Rais, TAMISEMI lakini bado Wizara yangu inahusika katika kuangalia ubora kinachoendelea shuleni na kuhakikisha kwamba mitaala inafundishwa kama inavyokusudiwa. Kwa hiyo, bado Wizara ya Elimu ina shirikiana na TAMISEMI kuhakikisha kwamba hizi shule zenye vipaji maalum zinaendelea kufanya vizuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Freeman Mbowe.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kuwepo na mabweni katika shule kwa ajili ya kidato cha tano na sita ni jambo muhimu ama sharti muhimu la kupata nafasi ya kuwa na shule ya kidato cha tano na sita, na kwa sababu kazi ya ujenzi wa mabweni katika maeneo mengi imeweza kufanywa na wananchi wenyewe na Serikali ikaongezea nguvu zake; na kwa sababu vilevile sera ya Serikali katika ujenzi wa kidato cha tano na sita ni kupata wananfunzi kutoka maeneo mbalimbali ya nchi ili wachanganyikane, jambo ambalo ni jambo jema.

Serikali haioni kwamba kwa wale wananchi ambao wapo tayari kujenga mabweni ya kidato cha tano na sita; maeneo kama hayo yanapojitokeza wapewe kipaumbele katika kupata nafasi zaidi katika shule hizo? Japo na nafasi nyingine itolewe kwa wananchi katika Mikoa mingine? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Naibu Waziri TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS TAMISEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli na tunashukuru kwanza wananchi kwa dhati kabisa. Katika maeneo mbalimbali na hata katika pitapita yangu karibuni wananchi wengi sana wameamua ku-*invest* sana katika suala zima la kuhakikisha kwamba wanaboresha shule zao. Na hili limetusaidia sana kwa sababu shule nyingi katika kipindi hiki cha kati tumeweza kupata shule za kidato cha tano na kidato cha sita lakini nguvu kubwa katika upande wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hili naomba nikiri wazi kwamba sisi kama Serikali tutapenda kuweka kipaumbele cha kutosha kabisa jinsi gani tutafanya kuweka nguvu zaidi katika maeneo hayo; lengo kubwa ni kwamba Watanzania hawa na vijana wetu wanaofaulu kidato cha nne waweze kupata fursa. Kwa sababu mwaka huu ukiangalia kuna maeneo mbalimbali tulipata wanafunzi walifaulu zaidi hata ukilinganisha na idadi ya shule tuziokuwa nazo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbowe swali lako ni jambo la msingi na Serikali hii tutaipa jicho la karibu zaidi; lengo kubwa ni kwamba vijana wa Tanzania waweze kupata fursa ya elimu katika nchi yao.

**MWENYEKITI:** Ahsante, natambua umuhimu wa elimu nchini lakini tunaendelea, muda. Swali linalofuata namba 19 linaulizwa na Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, kutoka Baraza la Wawakilishi.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, wananchi wa Visiwa vya Ugunja wako tayari kusikiliza majibu ya Serikali ya swali namba 19 ambapo mmepokea mara mbili jawabu sijui nikamate *which is which?*

**MWENYEKITI:** Uliza swali Mheshimiwa.

Na. 19

**Umiliki wa Kisiwa cha Latham (Fungu Mbaraka)**

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB** aliuliza:-

Kwa mujibu wa taarifa rasmi ya Serikali Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) iliyotolewa mwaka 2014 Kisiwa cha Latham (Fungu Mbaraka) ni mali ya Zanzibar tangu kilipotangazwa rasmi mwaka 1898. Hata hivyo, zipo taarifa zilizothibitishwa kuwa Serikali ya Muungano kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu iliiandikia SMZ kuwataarifu kwamba kisiwa hicho ni cha Tanzania Bara.

(a) Je, Serikali haioni mgogoro huo wa umiliki wa kisiwa hicho ni aibu kutokea kwa nchi moja na kuonesha kwamba bado kero za Muungano hazijapatiwa ufumbuzi?

(b) Kisiwa cha Latham kimepakana na vitalu namba 7 na 8 ambavyo tayari *TPDC* imeshavigawa bila ridhaa ya SMZ; je, Serikali haioni kuwa mgogoro huo sio wa mpaka bali ni wa mafuta na gesi?

(c) Je, Serikali inachukua hatua gani kumaliza mgogoro huo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa swali ni kwamba kuna barua kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhusu hili suala, barua hiyo tumeitafuta kwenye Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar hatujaiona. Kwa hiyo, Mheshimiwa atusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda kwenye swali; kwanza (a) hakuna mgogoro wowote kuhusu umiliki wa eneo lolote baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa tafsiri na suala zima la mipaka la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar limewekwa

wazi kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba ya Zanzibar kabla na baada ya Muungano.

Vilevile katika orodha ya changamoto 14 za Muungano zilizokwishashughulikiwa na zinazoshughulikiwa hakuna suala lolote linalohusu umiliki wa eneo lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mgogoro wowote wa mafuta na gesi baina ya Serikali zote mbili, huko nyuma ni kweli kwamba leseni za utafutaji mafuta zilitolewa na *TPDC* katika eneo husika kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 1980 kwa sababu suala la mafuta lilikuwa ni suala la Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hakuna mgogoro wowote kati ya Serikali hizi mbili kuhusu suala hili, hakuna hatua zozote zilizochukuliwa na Serikali. Hata hivyo, Serikali zote mbili zilikubaliana kwamba suala la mafuta na gesi liondolewe kwenye orodha ya mambo ya Muungano na kuwezesha Zanzibar kuanza harakati za kutafuta gesi na mafuta na kwamba mpaka sasa Sheria mpya ya Mafuta ya mwaka 2015 imetoa fursa kwa Zanzibar kusimamia shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi katika maeneo ya Zanzibar na ndio maana Zanzibar sasa pia ipo katika mchakato wa kutunga Sheria yake ya Mafuta na Gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata pale ambapo mgogoro unaweza kuibuka tunao utaratibu mzuri wa kukabiliana na changamoto hiyo na watu wa pande zote mbili za Muungano ni ndugu na jamaa na hawawezi kufarakana hata siku moja kuhusu umiliki wa eneo lolote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jaku.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri nimuombe kumuuliza maswali madogo sana ya nyongeza.

Kwa masikitiko makubwa sana suala hili limeleta gumzo sana katika chombo cha Baraza la Wawakilishi, limeleta gumzo muda mrefu na hatimaye likatua katika chombo hiki muhimu kwa wananchi.

Mwaka 2014 Serikali mbili, Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iliunda kamati ya wataalam na kamati hiyo ya wataalam iliongozwa na wanasheria wazito wa nchi hii akiwemo Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa uliza swali.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio swali hili nakuja nalo; imeunda Kamati iliyokuwa inaongozwa na Wanasheria Wakuu wawili kutoka Zanzibar na Bara ili kutatua changamoto zilizokuwepo katika mafuta na gesi ikiwemo ya Kisiwa hiki cha Latham na ripoti hii wakaikabidhi kwenye Serikali zote mbili. Je, ni lini Serikali imetoa ripoti ya suala hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Zanzibar ina mipaka yake ninachokifahamu hapa kama ni Serikali moja ni majibu yaliyojibiwa hapa; Zanzibar mipaka yake na hili eneo Zanzibar na swali lao. Tukamate wapi ambapo pana ukweli?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Makamba.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu tangu mwaka 1968 ambapo suala la gesi na mafuta liliingizwa kwenye orodha ya mambo ya Muungano; baada ya hapo kwa muda mrefu kumekuwa na hoja na haja ya kuliondoa suala hilo kwenye orodha ya mambo ya Muungano; na zimefanyika jitihada mbalimbali ili kufikia azma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwaka 2010 ilikubalika baina ya Serikali zote mbili kwamba suala hilo liondolewe. Kamati anayoizungumza Mheshimiwa Jaku ya wataalam iliundwa ili kutafuta namna kwa sababu suala hili lipo Kikatiba na lingeweza kuondolewa Kikatiba; lakini kamati hiyo iliundwa mahususi ili kuwezesha jambo hilo lifanyike wakati mchakato wa kubadilisha Katiba unafanyika na matokeo ya kamati hiyo ilipelekea sasa kuapata mwanya ambapo Sheria ya Mafuta tuliyopitisha Bungeni mwaka jana iliruhusu Zanzibar iweze kuchimba na kutafuta mafuta na sasa kuna sheria inatungwa katika Baraza la Wawakilishi ya kuruhusu Zanzibar ichimbe na kutafuta mafuta hata kabla Katiba haijabadilishwa rasmi na kuliondoa suala hilo kwenye orodha ya mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo tunafahamu kwamba katika Katiba Inayopendekezwa suala hilo limezingatiwa na litaondolewa katika orodha ya mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa ambacho napenda kusisitiza ni kwamba sisi Jamhuri yetu hii ya Muungano kama nlivyosema kwenye lile jibu la msingi ni watu wa ndugu na jamaa moja; hakuna mgogoro wowote unaohusiana na mipaka au umiliki wa eneo lolote katika Jamhuri yetu ya Muungano wa Tanzania. Na sisi pia kama ndugu tumejenga utaratibu wa kiutamaduni na kitaasisi wa kushughulikia na changamoto za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninachopenda kutoa rai ni kwamba kwa wenzetu ambao wanapenda kutumia masuala ya Muungano kukabiliana na matatizo yao ya kisiasa, aidha, upande wa Bara au Zanzibar waache hayo mambo na watoe nafasi kwetu sisi ambao tumepewa dhamana ya kushughulikia mambo ya Muungano na Serikali iweze kufanya shughuli zake. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Muungano unaendelea na utadumu. *(Makofi)*

Tunaendelea; swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mbunge wa Kaliua.

Na. 20

**Ukaguzi Uliofanywa kwenye Vyama vya Ushirika- Tabora**

**MHE. MAGDAENA H. SAKAYA** aliuliza:-

Serikali ilifanya ukaguzi maalum kwenye Vyama vya Ushirika vya Mkoa wa Tabora pamoja na Chama Kikuu cha Ushirika *(WETCU)* tangu mwaka 2014 na kubaini ubadhirifu mkubwa uliofanywa na viongozi kwa kushirikiana na benki mbalimbali.

(a) Je, ni kwa nini mpaka leo ripoti hiyo haijawekwa wazi na hatua za kisheria kuchukuliwa kwa wote waliohusika na wizi huo?

(b) Vyama vingi viko kwenye hali mbaya na havikopesheki na hivyo kupelekea wakulima kukosa pembejeo za kilimo. Serikali ina mpango gani mahsusi wa kusaidia vyama hivyo vya ushirika kwa kuzingatia mchango wa zao la tumbaku kwenye uchumi wa Taifa hili?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mbunge wa Kaliua lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri mwenye dhamana ya ushirika alikabidhi taarifa ya ukaguzi kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi *(IGP)* kupitia kwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Tabora mnamo tarehe 18 Septemba, 2014 kwa ajili ya kuchukua hatua za kisheria dhidi ya makosa ya jinai yaliyobainika. Mwezi April 2016, Mrajisi wa Vyama vya Ushirika alituma maafisa Mkoani Tabora kufuatilia hatua zilizochukuliwa. Ilibainika kwamba uchunguzi umekamilika na watuhumiwa watachukuliwa hatua za kisheria. Hadi mwezi Juni, 2016 maombi

ya kuwafungulia mashtaka watuhumiwa yalipelekwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai akiridhia wafunguliwe mashtaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeanzisha kitengo cha sheria kwa ajili ya kuchukua haraka dhidi ya makosa ya jinai katika vyama. Tume imemwandikia *DPP* kuomba kibali kwa mujibu wa kifungu cha 133 cha Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2013 ili wanasheria wake wapewe mamlaka ya kuendesha mashtaka ya kesi zinazohusu Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyama vya msingi ambavyo havikopesheki, Serikali inaendelea kuvihimiza Vyama Vikuu vya Ushirika kuangalia utaratibu wa kuvikopesha kwa utaratibu wa kuanzisha *revolving fund* badala ya kutegemea benki. Chama Kikuu cha Ushirika *(WETCU)* kilielekezwa kuhakikisha vyama vyake vya msingi 112 kati ya 217 ambavyo havikopesheki viwezeshwe kukopesheka. *WETCU* imeviwezesha vyama 68 kushiriki kuzalisha tumbaku msimu ujao kwa kutumia fedha za *revolving fund*. Fedha hizo zinatokana na sehemu ya mgao wake wa ushuru wa iliyokuwa *Apex* ya tumbaku na sehemu ya ushuru wake jumla shilingi milioni 800. Inatarajiwa kwamba kwa vile fedha hizi ni *revolving* zitaweza kutumika kuviwezesha vyama vilivyosalia viweze kukopesheka.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana tangu tarehe 18 Septemba, 2014 mpaka leo ni miaka miwili; taarifa ilikabidhiwa na mpaka leo hakuna hatua zozote zilizochukuliwa za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haioni kuendelea kuchelewa kuchukua hatua kwenye masuala ya msingi kama haya yanayohusu masuala ya kilimo wakati tunasema kilimo ni uti wa mgongo; inazidi kudidimiza kilimo ambacho ndio hasa sehemu kubwa ya uchumi wetu na hivyo Serikali ipo tayari sasa kuchukua hatua za haraka kuhakikisha wale wote waliohusika wanafilisiwa kwanza mali zao wakati hatua za kuwafikisha mahakamani zinafuata?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili hakuna kilimo chenye tija bila kuwa na ushirika wenye nguvu; *COASCO* ambayo imepewa jukumu la kukagua vyama vya ushirika Tanzania imeshindwa kabisa kutimiza wajibu wake. Serikali sasa haioni sababu kuweza kukabidhi jukumu la ukaguzi wa Vyama vya Ushirika kwa Ofisi ya *CAG* ili watimize wajibu huu? Fedha zinazoibiwa ni fedha za Watanzania, ni fedha za wakulima lakini pia ni fedha za Serikali. Ili jukumu hili

likaguliwe na Ofisi ya *CAG* na hivyo kuweza kusaidia kilimo na wananchi kwa ujumla. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu Mheshimiwa Naibu Waziri; Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba hatua za kuwachukulia wahusika kuwapeleka mahakamani imechukua muda mrefu. Hata hivyo, nimueleze tu kwamba ni changamoto ya jumla katika sekta yetu ya kutoa haki na ndio maana kuna hatua mbalimbali zinaendelea ndani ya Serikali ili kuhakikisha kwamba haki inapatikana kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge baada ya kuona kwamba baada ya kuona kwamba utaratibu wa kuwatumia wanasheria wanaotoka kwa *DPP*; Wizara yangu kwa kupitia Tume ya Ushirika tayari imeandika barua ya kuomba ruhusa ya kuwatumia wanasheria waliopo kwenye Tume ya Ushirika ili wao waweze kuhusika katika kuendesha kesi za ushirika. Nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba pindi ombi letu hilo litakapokubalika na tunalifuatilia kwa karibu sana; wanasheria wetu watahakikisha kwamba kesi hizo zinaendeshwa kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusu *COASCO*; napenda vilevile kukubaliana na hoja ya Mheshimiwa Mbungekwamba *COASCO* imekuwa ikituletea matatizo na changamoto katika ukaguzi wa Vyama vya Ushirika. Badala ya kutumia Ofisi ya *CAG* kwa sasa Wizara yangu inafanya utaratibu wa kurekebisha kasoro za kiutendaji zilizopo ndani ya *COASCO* ili iendelee kutoa huduma za ukaguzi kwa haraka kwa sababu wao ndio wanatambuliwa kwenye Sheria ya Ushirika Namba Sita ya mwaka 2013 kama ndio wakaguzi wa vyama hivi vya ushirika. Tunatambua changamoto tunaifayia kazi, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Musukuma swali moja tu, muda wenyewe sio rafiki.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru; kwa kuwa Kanda ya Ziwa tunategemea kilimo na zao la pamba limekufa, tukahamasisha wakulima wetu walime zao la mpunga kama zao la biashara na bahati nzuri Mwenyezi Mungu akatujalia mpunga ukaiva wa kutosha na Rais wa Jamhuri ya Muungano alizunguka kwenye kampeni akisema wakulima hawatafungiwa masoko kwa kuwa wanalima kwa pesa zao na nguvu zao wenyewe.

Kwa kuwa Serikali imezuia wananchi na wafanyabiashara wa mpunga kupeleka nje, wakulima wetu kule wameivisha mpunga hawana sehemu ya kuweka huko nje na tunaenda kwenye msimu wa mvua. Je, Serikali ina mpango gani kama haijataka kufungua soko wa dharura wa kuweza ku-*protect* kile chakula kilichopo nje? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Swali lenyewe, haya la msingi sana, sijakuita bwana, sijakuita Mheshimiwa. Lakini naliruhusu kwa sababu ya umuhimu wake, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kurekebisha, Mheshimiwa Mbunge amesema Serikali imekataza wafanyabiashara kupeleka mazao nje, kauli sahihi ni kwamba Serikali imesitisha huku tukiweka utaratibu sawa kwa sababu tunajaribu kuangalia tuwe na utaratibu mzuri zaidi wa kuruhusu chakula kiende nje kwa sababu kuna hatari kubwa kwamba tukiendelea kufanya holela kama ilivyo sasa nchi yetu inaweza ikaingia katika janga la njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu Ukanda mzima wa Kusini mwa Afrika unakabiliwa na njaa, nchi 13 kati ya nchi 15 za Jumuiya ya Kiuchumi ya Kusini mwa Afrika *(SADC)* zinakabiliwa na njaa ikiwemo Afrika ya Kusini. Utaratibu ambao tumekuwa tukiutumia kupeleka chakula nje ulikuwa unatoa fursa chakula chote kiishe bila kufuata utaratibu. Kwa hiyo tulichofanya ni kwamba tumefanya tathmini ya taratibu ambazo tunatumia ili kuja na utaratibu ambao utaturuhusu na kuwaruhusu wafanyabiashara wetu waweze kupeleka nje lakini katika hali ambayo haitatuacha katika hali ya njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba utaratibu huo karibia unakamilika na muda si mrefu, namhakikishia kupitia Bunge lako tukufu kwamba utaratibu wa kawaida wa kupeleka chakula nje kwa wafanyabiashara utaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wavute subira, Serikali ya Awamu ya Tano haina nia ya kukwamisha wafanyabiashara na Watanzania kutumia mazao yao kibiashara, sisi wenyewe tunatafuta masoko, lakini lazima tufanye kwa njia ambayo sio holela kwa sababu tuna majukumu vilevile ya kuhakikisha kwamba nchi yetu haiingii katika baa la njaa.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, tunaendelea. Naelewa uzito wa suala hili, mimi nafahamu. Nia ya Serikali ni nzuri tu lakini mfanyakazi yeyote anayelipwa na mwajiri wake mnampangia matumizi ya pesa yake? *(Makofi)*

Tunaendelea, swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mbunge wa Bukoba Mjini.

Na. 21

**Mkoa wa Kagera Kuwa Miongoni mwa Mikoa Maskini**

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE** aliuliza:-

Kufuatia taarifa zilizotolewa na vyombo vya Serikali vinavyohusika na masuala ya utafiti na takwimu, Mkoa wa Kagera ulikuwa miongoni mwa mikoa mitano maskini ya mwisho Kitaifa.

(a) Je, ni mambo gani yametumika kama vigezo vya kuingiza Mkoa wa Kagera katika orodha ya mikoa mitano maskini Kitaifa?

(b) Je, ni jitihada gani za makusudi zinazochukuliwa na Serikali kuunusuru Mkoa wa Kagera na umaskini huo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mbunge wa Bukoba Mjini lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Mwenyekiti, vigezo vilivyotumika katika kubainisha Mikoa na Wilaya maskini ni uwezo wa kaya kukidhi mahitaji ya msingi kama vile chakula chenye kiwango cha kilo kalori 2,200 kwa siku, mavazi na malazi. Kwa kutumia vigezo hivi uchambuzi wa kina wa takwimu zilizotokana na utafiti wa mapato na matumizi katika kaya wa mwaka 2011/2012 na sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 ulibaini kuwa Mkoa wa Kagera ni miongoni mwa mikoa yenye kiwango kikubwa cha umaskini wa asilimia 39.3.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kunusuru Mkoa wa Kagera na umaskini, Serikali inafanya jitihada na kuchukua hatua mbalimbali kama ilivyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano kama ifuatavyo:-

(i) Kuendeleza maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji na maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya viwanda kwa kujenga miundombinu ya msingi ili kuwezesha uwekezaji na ukuaji wa viwanda vidogovidogo na vya kati katika Mkoa wa Kagera.

(ii) Kuendelea kuhamasisha wananchi wote ikiwemo Mkoa wa Kagera kutumia fursa na rasilimali mbalimbali zilizopo katika mikoa husika.

(iii) Kuendeleza Sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi kwa kuboresha upatikanaji wa huduma za ugani, upatikanaji wa pembejeo, utafiti, na masoko ya mazao.

(iv) Kukuza sekta ya viwanda, hususan vya kusindika mazao ya maliasili, kilimo na uvuvi.

(v) Kuendeleza viwanda vya nyama vilivyopo Kanda ya Ziwa ikiwemo Mkoa wa Kagera, viwanda hivyo vitasaidia kuendeleza ufugaji utakaoinua kipato cha mtu mmojammoja pamoja na kuendeleza uchumi wa mkoa husika.

(vi) Uendelezaji wa viwanda vya nguo katika mikoa inayozalisha pamba ambapo Kagera huzalisha kwa asilimia 2 ya pamba yote katika Ukanda wa Magharibi.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kuniruhusu kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Mkoa wa Kagera enzi hizo ukiitwa Ziwa Magharibi baada ya kupata uhuru ilikuwa ni miongoni mwa mikoa minne ambayo ilikuwa na utajiri na pato kubwa ikiwa ni Kilimanjaro, Dar es Salaam pamoja na Mbeya, na wakati huo ikiwa na Chama cha Ushirika *(BCU)* ambacho kilikuwa na nguvu kubwa kiasi cha kuikopesha hata Serikali, sasa maswali yangu.

La kwanza, je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba miongoni mwa mambo ambayo yamesababisha umaskini kwanza ni vita ya Kagera ambayo hata baada ya kualizika na Serikali ya Uganda kulipa fidia, wananchi hawakupewa fidia yoyote?

Pili, ugonjwa wa UKIMWI, lakini tatu Chama cha Ushirika cha *KCU* ambacho kimesambaratika na hususan kutokana na mambo mengi ya kisiasa badala ya kutetea zao la kahawa. Lakini pia Reli ya Kati ambayo kimsingi imesambaratika na haifiki Kemondo na hivyo wananchi wa Mkoa wa Kagera kupokea bidhaa kwa njia ya barabara ambayo inawagharimu vibaya sana.

Je, Serikali haioni kwamba kuna haja pamoja na mambo aliyozungumza ambayo kimsingi bado yanaeleaelea na hayana mashiko, kuweka mkakati mahsusi wa kuyaweka katika utekelezaji na hata kuyaweka katika mpango wa *BRN* (Matokeo Makubwa Sasa), lakini sambamba na hilo kwa kupitia Mpango wa *TASAF,* kama Serikali imetathmini kwamba mkoa ni maskini na kaya ni

maskini kwamba bajeti ya *TASAF* iongezeke ili kaya ziweze kupokea pato zaidi na kaya ziweze kuongezeka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kufuatana na sababu zilizotolewa na takwimu zilizotolewa, je, hizi takwimu zinatoa takwimu sahihi ambayo inaashiria ni kwa Wilaya zote au ni kwa baadhi ya wilaya zilizopo ndani ya Mkoa wa Kagera ndiyo zenye umaskini wa namna hii? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Haya tuulize kwa kifupi maswali yetu. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nakubaliana na sababu alizozisema na ndiyo maana Serikali iko kwenye mpango mkakati wa utekelezaji wa mpango wetu ambao tumeuwasilisha humu Bungeni kama alivyosema tuje na mpango mahsusi wa utekelezaji kupeleka kwenye *BRN,* Serikali iko kwenye mchakato wa kuja na utekelezaji wa maazimio yote na malengo yote yaliyopo ndani ya *BRN.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo utakumbuka ni kwamba tayari sasa hivi mchakato wa kutengeneza Reli ya Kati kwa *standard gauge* unaanza mwezi Disemba tunaanza utekelezaji na ambayo inaelekea upande huohuo wa Mikoa ya Magharibi na Kagera ikiwepo ili tuweze kufungua uchumi wa Mkoa wa Kagera na uchumi wa mikoa mingine ya upande wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu takwimu hizi, naomba niliambie Bunge lako Tukufu, takwimu hizi ni sahihi na zinaashiria Mkoa mzima wa Kagera kwamba upo katika kiwango cha umaskini wa asilimia 39 kama nilivyosema.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naomba niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa matatizo yaliyopo kwenye Mkoa wa Kagera, Mkoa wa Mwanza pia ni moja kati ya mikoa iliyotajwa kuwa mikoa maskini, sasa ningependa kujua mikakati ya Serikali mbali ya majibu mazuri na mipango ya miaka mitano na mwaka mmoja, ina mkakati gani wa kuwawezesha wafanyabiashara wadogo na wa kati ili kuwa sehemu ya kuhakikisha na wao wanakuwemo kwenye mpango wa kuhakikisha umaskini huu unatoweka wakiwa wana nafasi nzuri ya kufanya biashara zao kwa uhuru?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema na kama tulivyoainisha kwenye mpango wetu wa mwaka mmoja na mpango wa miaka mitano kwamba sasa hivi tunaangalia jinsi ya kuanzisha na kuendeleza viwanda vidogo vidogo pamoja na viwanda vikubwa vikubwa, vya kati pia ili tuweze sasa kutengeneza ajira kwa watu wetu. Na hii ni pamoja

na kuwawezesha wafanyabiashara hao wadogo na wa kati ili waweze kupata bidhaa zao kwa bei nafuu na pia tuangalie pia wafanyabiashara ambao wako katika sekta ya kilimo kwa sababu tumesema viwanda vidogo, viwanda vya kati na vikubwa vitatumia malighafi zinazozalishwa hapa nchini kwa hiyo ni mpango wa Serikali yetu kuweza kuwawezesha watu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa sababu tunakuja na *Microfinance Act* mwezi huu au mwezi wa 11 ni uhakika kwamba watu hawa, wafanyabiashara wadogo na wa kati watapewa elimu ya ujasiriamali na jinsi gani ya kuendeleza biashara zao pamoja na kuwezeshwa mitaji ni moja ya mikakati ya Serikali yetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda, tunaendelea na swali linalofuata, swali namba 22 linaulizwa na Mheshimiwa Saed Ahmed Kubenea, Mbunge wa Ubungo.

Na. 22

**Deni la Taifa**

**MHE. FREEMAN A. MBOWE (K.n.y MHE. SAED A. KUBENEA)** aliuliza:-

Serikali ya Awamu ya Nne ilikopa fedha kwenye Benki za Nje na zile za biashara kwa mfano mwaka 2011 Serikali ilikopa shilingi trilioni 15 na kufanya Deni la Taifa kufikia shilingi trilioni 21, kabla ya mwaka 2015 ilikopa tena kiasi cha shilingi trilioni 9 na kufanya Deni la Taifa kuongezeka kufikia shilingi trilioni 39.

(a) Je, mpaka sasa Deni la Taifa linafikia kiasi gani?

(b) Je, Serikali ina mikakati gani ya makusudi ya kudhibiti ongezeko hilo la Deni la Taifa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango napenda kujibu swali la Mheshimiwa Saed Ahmed Kubenea, Mbunge wa Ubungo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 Serikali ilipokea mikopo ya nje yenye masharti nafuu na ya biashara kiasi cha shilingi bilioni 1,333.28 na mwaka 2014/2015 Serikali ilipokea mikopo ya kiasi cha shilingi bilioni 2,291.6. Mikopo hiyo haikufikia kiasi cha trilioni 15 kwa mwaka 2011 na trilioni tisa kabla ya mwaka 2015 kama ilivyotafsiriwa na Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Juni, 2016, Deni la Taifa lilikuwa dola za Kimarekani bilioni 23.2 ikilinganishwa na dola za Kimarekani bilioni 19.69 mwezi Juni, 2015 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 18. Kati ya kiasi hicho, deni la Serikali lilikuwa dola za Kimarekani bilioni 20.5 na deni la sekta binafsi lilikuwa dola za Kimarekani bilioni 2.7.

Aidha, deni la Serikali lilitokana na mikopo ya ndani na nje kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Baadhi ya miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa barabara na madaraja nchini, mradi wa kimkakati wa kuboresha majiji, ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 400 kutoka Iringa mpaka Shinyanga, mabasi yaendayo haraka, ujenzi wa bomba la gesi na mitambo ya kusafishia gesi, upanuzi wa uwanja wa ndege wa Dar es Salaam na mradi wa maji Ruvu Chini na Ruvu Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa na mikakati mbalimbali ya makusudi kabisa ili kudhibiti ongezeko la deni hilo. Mikakati hiyo ni pamoja na kuongeza ukusanyaji wa mapato, kupunguza matumizi yasiyo ya lazima, kuendelea kutafuta misaada na mikopo nafuu na kukopa mikopo michache ya kibiashara kwa miradi yenye kuchochea kwa haraka ukuaji wa Pato la Taifa, kudhibiti ulimbikizaji wa madai ya kimkataba kwa wakandarasi na watoa huduma na kudhibiti madeni yatokanayo na dhamana za Serikali kwenye mashirika ya umma kwa kufanya ufuatiliaji wa karibu wa mikataba inayoweza kusababisha mzigo wa madeni kwa Serikali. Aidha, Serikali inaendelea na mchakato wa kukamilisha zoezi la nchi kufanyiwa tathmini *(sovereign rating)* kwa lengo la kupata mikopo nafuu.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mbowe.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa mujibu wa takwimu ambazo Mheshimiwa Naibu Waziri ametupatia, Deni la Taifa sasa mpaka Juni mwaka huu limefikia shilingi trilioni 51 na bilioni 40. Kiwango hiki cha fedha ni *almost* mara mbili ya bajeti ya Taifa. Wakati huo huo ukigawanya deni hili kwa Watanzania milioni 45 kila Mtanzania leo atakuwa anadaiwa shilingi 1,134,222.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kukopa ni muhimu katika wakati mwingine ili kuweza kusukuma mbele shughuli za kimaendeleo, lakini ulazima wa kukopa kwa kiwango ambacho tunaweza kukilipa kwa wakati ili Taifa liondokane na mzigo wa riba pamoja na kulimbikiza madeni liweze kujielekeza mapato yake zaidi katika kushughulikia mipango ya maendeleo, ni vyema tuwe na kiwango cha ku-*control* ukopaji wa Serikali.

Sasa swali langu la mwisho ni hili, tutakumbuka wakati wa Awamu ya Tatu, wakati wa Mheshimiwa Mkapa, Tanzania ilikuwa mojawapo ya nchi

zilizokuwa zimepata sifa ya kuwa miongoni mwa nchi zilizosamehewa madeni kupitia mpango wa *HIPC (Heavily Indebted Poor Countries)* ambapo Deni la Taifa liliweza kusamehewa na likashuka chini ya dola bilioni 10 na *almost* tulikuwa tunamaliza Deni la Taifa.

Je, ni kwa nini Serikali sasa hivi, kwa sababu bado mpango wa *HIPC* upo chini ya *World Bank* na *IMF,* ni kwa sababu gani Serikali isione uwezekano tena wa kufanya *initiative* ya kurudishwa katika Mpango *HIPC* ambao unasimamiwa na *World Bank* na *IMF* ili tupunguze mzigo huu wa madeni na hizo pesa tuzielekeze zaidi kwenye shughuli za kimaendeleo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haijaondoka kwenye mpango huo wa kusamehewa madeni na bado tunaendelea na mchakato huu kwa kushirikiana na *IMF* pamoja na *World Bank*. Zipo nchi ambazo zilikuwa katika mpango wa kuhakikisha tunasamehewa madeni kama nchi yetu lakini zilisitisha kutokana na migogoro ambayo ipo ndani ya nchi hizo, moja ya nchi hizo ilikuwa ni Iraq, Iran pamoja na nchi nyingine zenye migogoro ambazo zilisitisha sasa kusamehewa madeni. Hivyo bado tunaendelea na mchakato huo kuendelea kuwashawishi wadau hao wa maendeleo ili waweze kutusamehe madeni haya.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa ya kitaalam, lakini nilitaka kuongezea nyongeza tu na kuwatoa hofu Watanzania kwenye kile alichosema Mheshimiwa Mbowe kwamba ukiligawa deni hilo kwa kila Mtanzania.

Kwanza hakuna siku Watanzania watagongewa mlango wakigawanywa Deni hilo la Taifa na wala katika Taifa lolote hakuna utaratibu wa kupima deni kwa kuangalia mgawanyo wa ujazo wa watu bali Deni la Taifa linapimwa kufuatana na uwezo wa nchi kimapato inavyokusanya na inavyoweza ku-*service* deni hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo tunapoangalia kukua kwa deni tutakiwa pia tuangalie miundombinu ya nchi yetu imekuwa kwa kiwango gani kwa sababu wazo hilo linafuatana na uamuzi wa nchi inayochukua kwenye miundombinu, hata hivi sasa Waheshimiwa Wabunge tunavyoongelea *standard gauge* ya reli, tunavyoongelea miradi mikubwa mikubwa kama ya bandari tutakuwa tunaongelea uwezo wa nchi yetu kuweza kuendesha miradi, lakini ujenzi wake utategemea njia hizo hizo za kuweza kukopa. Ndiyo maana hata mataifa makubwa ambayo yameendelea leo hii yana madeni makubwa lakini yana uwezo wa kulipa madeni hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimoja tu ambacho natakiwa nimhakikishie Mheshimiwa Mbowe ambacho Serikali inakifanya, haikopi kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Serikali inapokopa kwa mara zote inakopa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambayo itazalisha kulipa deni hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Jamani Waheshimiwa Wabunge naomba utulivu. Naelewa hili swali ni la msingi sana. Nimshukuru sana Mheshimiwa Mwigulu na Naibu Waziri. Nimshukuru sana muuliza swali, mimi naendelea kuisihi Serikali ili kuwasaidia Wabunge na wananchi uelewa huu kwa sababu kupima Deni la Taifa uhimilivu wake, *sustainability* yake, vigezo hivyo siyo vya Tanzania tu ni vya Kimataifa na kama alivyojaribu kueleza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mambo ya Ndani.

Kwa hiyo, nadhani tukiendelea kuwaelimisha Wabunge na Wananchi kama alivyotoa majibu na mengine najua yapo kwa upande huu itasaidia sana.

Tunaendelea, swali namba 23 linaulizwa na Mheshimiwa Phillipo Augustino Mulugo, Mbunge wa Songwe.

Na.23

**Kupandishwa Hadhi Baadhi ya Barabara - Songwe**

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO** aliuliza:-

Kata za Wilaya ya Songwe zipo mbalimbali kwa zaidi ya kilometa 40 kutoka kata moja hadi nyingine. Iliyokuwa *RCC* ya Mkoa wa Mbeya ilisharidhia kupandisha hadhi barabaraya Kapalala hadi Gua na Kininga hadi Ngwala ziingie kwenye barabara za Mkoa lakini mpaka sasa hakuna utekelezaji.

Je, ni lini sasa Serikali itapandisha hadhi barabara hizo?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Phillipo Augustino Mulugo, Mbunge wa Songwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kupandisha hadhi barabaa unafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Barabara Namba 13 ya mwaka 2007 na kanuni zake za mwaka 2009. Aidha, maombi ya kupandisha hadhi barabara ya Kapalala hadi Gua na Kininga hadi Ngwala kuwa za Mkoa yanaendelea kufanyiwa kazi na Wizara yangu sambamba na maombi kutoka Mikoa mingine. Mara baada ya kukamilika kwa zoezi hilo taarifa itatolewa na Serikali kupitia kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Songwe.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mulugo.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti kwanza nipende tu kusikitika tu kwamba sijui Serikali inafanya kazi kwa upendeleo baadhi ya Wilaya zingine. Tumekaa *RCC* iliyokuwa Mkoa wa Mbeya na Mheshimiwa Mwambalaswa na Mheshimiwa Mary Mwanjelwa mashahidi hapa. Tumepitisha barabara za Chunya mbili kutoka Ngwala mpaka Kapalala na kutoka Gua ziende ziwe hadhi kwa Mkoa ziwe kwenye *TANROADS,* toka mwaka 2011 tulikaa *RCC* tukapitisha leo bado Serikali inasema tunafanyia kazi, miaka sita mnafanyia kazi? Mimi binafsi nimesikitika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti narudia tena, naomba Serikali inijibu kwasababu tayari Songwe imeshakuwa ni Wilaya mpya ni lini watatupatia fedha tupandishe hadhi barabara ya hiyo kutoka Kininga kwenda Ngwala ni kilometa 46. Nikitaka kufanya ziara kule nitembee kwa bodaboda na watu wananielewa hivyo na kuna wanyama wakali na kuna ndorobo nahangaika sana.

Naomba leo Serikali inipe majibu tunahangaika sana wenzenu. Mbona sehemu zingine barabara mnatengeneza? Kutoka mwaka 2011 mpaka leo hatujatengeneza barabara. Naomba Mheshimiwa Waziri uniambie hapa hapa, utaniletea lini barabara hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Profesa Mbarawa.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kumfahamisha kwamba Serikali hii haifanyikazi kwa upendeleo. Watanzania wote sisi kwetu ni sawa na nia ya Serikali hii ni kuwajengea miundombinu ya kisasa Watanzania wote. Kama uko Mbeya, kama uko Mwanza, kama uko Shinyanga kazi yetu ni kuwajengea Watanznia miundombinu ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli imechukua muda mrefu na tatizo kubwa ambalo tunalo ilikuwa ni fedha, fedha, fedha, lakini Serikali yetu ya Awamu ya Tano sasa tumejipanga na tutahakikisha kwamba siyo muda mrefu barabara zote tutaanza kuzipandisha hadhi. Lakini naomba waelewe tu changamoto tuliyonayo ni fedha, fedha kwa sababu ukipandisha hadhi barabara maana yake ni fedha unataka utengeneze sasa kwa kiwango cha juu zaidi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali ilikuwa imeniahidi kupandisha barabara ya Gulwe, Berege, Chitemo, Mima, Chazima, Igoji mpaka Seluka Ufufu. Barabara hii ni mbaya, Halmashauri haina uwezo. Je, Mheshimiwa Waziri ni lini sasa mtapandisha hadhi barabara hii pamoja na kuweka lami barabara ya Mbande - Kongwa - Mpwapwa na Kibakwe?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Profesa Mbarawa.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumemuahidi na tunalifanyia kazi mara tutakapopata fedha za kutosha barabara hiyo tutaipandisha kama nilivyosema mwanzo nia ya Serikali hii ni kuhakikisha kwamba barabara zote zinakuwa nzuri na zinapitika wakati wote na pale tunapokuwa na fedha za kutosha tutahakikisha kwamba barabara zote tunazijenga kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea kwa sababu ya muda Waheshimiwa najua mna maswali mengi tu. Swali linalofuata namba 24 linaulizwa na Mheshimiwa Juma Othman Hija, Mbunge wa Tumbatu.

Na. 24

**Ulipaji wa Ada Katika Vyuo Binafsi Nchini**

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA** aliuliza:-

Vipo baadhi ya vyuo binafsi vinalipisha wanafunzi ada kwa kutumia pesa za kigeni badala ya pesa za Kitanzania. Je, Serikali inachukua hatua gani kudhibiti usumbufu huo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Othman Hija, Mbunge wa Tumbatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka ya nyuma yalikuwepo malalamiko kuhusu baadhi ya vyuo vya binafsi kutoza ada kwa fedha za kigeni. Kifungu cha 48(1) cha kanuni zinazosimamia utoaji wa elimu katika vyuo vikuu yaani *The Universities General Regulations, 2013* kinakataza kuwatoza ada wanafunzi wa Kitanzania kwa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo vinaruhusiwa kutoza ada kwa fedha za kigeni kwa wananfunzi wasio raia wa Tanzania kama inavyobainishwa katika kifungu cha 48(2) cha kanuni tajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hiyo napenda kuchukua fursa hii kuwakumbusha wamiliki wa vyuo binafsi kuzingatia kanuni na taratibu zilizowekwa vinginevyo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao ikiwa ni pamoja na kupewa onyo, kuvifungia na kutoruhusiwa kudahili wanafunzi.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Juma Othman Hija swali la nyongeza.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mwenyekiti ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza swali moja fupi la nyongeza. Malalamiko haya ni ya muda mrefu sana na kila siku yanazidi kwa wananchi. Je, Wizara imewahi angalau kuwaonya wamiliki wangapi angalau kwa barua mpaka kufikia mwaka uliopita?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, *Engineer* Manyanya.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu imeshawahi kuwaonya wamiliki *IMTU* na mwenzao *KIU* kwa kukiuka masharti hayo na hivyo tunazidi kusisitiza wamiliki wote wachukue fedha ambayo ni ada kwa kutumia fedha za Kitanza ni ana pale inapobidi iwe tu kwa wananfunzi ambao wanatoka nchi za nje

**MWENYEKITI:** Ahsante tunaendelea. Swali namba 25 kwa Wizara hiyo hiyo linaulizwa na Mheshimiwa Salim Rehani toka Uzini.

Na. 25

**Watendaji Katika Taasisi za Elimu ya Juu Nchini**

**MHE. SALUM MWINYI REHANI** aliuliza:-

Kamisheni ya Vyuo Vikuu Tanzania *(TCU),* Baraza la Elimu ya Ufundi *(NACTE)* na Baraza la Mitihani Tanzania *(NECTA)* ni Taasisi za Muungano na zina Ofisi Zanzibar.

(a) Je, kuna Wazanzibari wangapi watendaji katika taasisi hizo?

(b)Kama hakuna, je, Serikali haioni kuwa hakuna uwiano kwa vile taasisi hizo ni za Muungano na kwa nini kusiwe na watendaji wa pande zote mbili za Muungano baina ya pande mbili?

(c) Je, kuna mipango gani ya kufanya taasisi hizi kuwa na watendaji wa pande zote mbili hasa Ofisi ya Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salim Rehani, Mbunge wa Uzini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, watendaji wa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania *(TCU)* na Baraza la Elimu ya Ufundi *(NACTE)* huajiriwa kwa mujibu wa kifungu 13, 14 na 15 cha Sheria ya Vyuo Vikuu Sura ya 346 na Sura 129 ya sheria ya Baraza la Elimu ya Ufundi Tanzania pamoja na kanuni na miongozo mbalimbali ya utumishi wa umma.

Kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi yaani *Staff Regulatiaons* pamoja na muundo wa utumishi yaani *Scheme of Service* wa taasisi hizo, Watanzania wote wenye sifa stahiki wanayo fursa sawa ya kuajiriwa bila kujali upande anakotoka muajiriwa. Hivyo Wizara haijaweka utaratibu wa kuwabaini watumishi kwa misingi ya maeneo wanayotoka. Aidha kwa mujibu wa sheria ya Bunge Namba 21 ya mwaka 1973 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002 iliyoanzisha Baraza la Mitihani, inabainisha kuwa muundo wa bodi ya baraza inajumuisha wajumbe watatu wanaotoka upande wa Zanzibar kati ya Wajumbe wote ambao ni kumi.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia utaratibu huo na kwa kutambua kwamba *TCU* na *NACTE* ni miongoni mwa taasisi zinazoshughulikia elimu ya juu na ufundi ambayo ni kati ya masuala ya Muungano na kwa kuwa Watanzania wote wana fursa na haki sawa, Serikali itaendelea kuajiri watumishi kwa vigezo vya sifa za kitaalamu ili kukidhi malengo ya utoaji huduma bora kwa jamii kama inavyostahili bila ubaguzi.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali ni kuhakikisha kuwa taasisi hizi zinatoa ajira kwa Watanzania wa pande zote za Muungano bila upendeleo wowote kwa kuzingatia sifa na mahitaji ya nafasi za ajira husika.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Rehani swali la nyongeza.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba nimuulize swali moja la nyongeza.

Kwa Zanzibar suala hili limekuwa na manung'uniko sana na hasa kwa kutokuweko watendaji katika hizi taasisi na hili limetokana kwamba wanafunzi

wengi wanaopata huduma kupitia *TCU*, *NACTE* na *NECTA* wamekuwa wanahisi hakuna uwiano na hakuna haki inayotendeka kwa vile hakuna watu ambao wanaohusiana wanaotoka upande ule kule. Je, Waziri au Wizara ina mpango gani wa kuweza kupata angalau maana yake watu wawili, watatu kuweza kuingia katika taasisi hizi ili kuepusha manung'uniko ya kila siku hasa yanayohusiana na masuala ya vyeti na mengineyo ambao wanataka kujiunga katika vyuo mbalimbali vya huku Tanzania Bara?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, *Engineer* Manyanya

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwaombe Watanzania tusifanye mambo kwa masuala ya hisia. Lazima twende katika misingi na misingi iliyopo ni hiyo ya kufuata sifa stahiki kwa nafasi zinazohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende tu kusema kwamba pamoja na kwamba hakuna hivi vigezo vilivyowekwa, kimsingi ukiangalia katika hizo taasisi zote wapo Wazanzibari ambao wanafanya hizo kazi na isitoshe kwa mfano kwa Baraza la Mitihani nafahamu hata Mkuu wa Kitengo kile kule Zanzibar anatoka Zanzibar. Lakini ukiacha hiyo nataka tu niseme kwamba sisi tumekuwa na mahusiano ya karibu sana na Serikali ambayo iko kwa upande wa Zanzibar na tunawasiliana katika masuala yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tarehe 11 Agosti, huu tulitembelewa na Mheshimiwa Waziri wa Elimu pamoja na Naibu wake na Katibu Mkuu na tuliweza kujadili mambo mablimbali ikiwemo ya kushirikiana na kusaidiana pale tunapoona upande mmoja haujakaa vizuri na kila jambo linalofanyika huwa tunashirikishana. Kwa hiyo, ninachoomba ni kwamba Mheshimiwa Mbunge tusiende kwa hisia. Kama nafasi zitaonekana kwamba Watu walioomba wenye uwezo wengi wanatoka Zanzibar basi itabidi wapewe kwa sababu tunachohitaji ni uwezo na siyo tu kuangalia upande wanakotoka.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge, oohh Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa mwenyekiti, napenda kuongezea katika majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa taaisis za Muungano kuwakilishwa kwa uwiano sahihi na muafaka kwa watu wa pande zote mbili, Serikali iliamua kwamba kuwe na *quota* kwa watumishi kwenye taasisi za Muungano na *quota* iliyokubalika ni asilimia 79 kwa asilimia 21 na sisi

ofisi yetu tuliwaandikia taasisi na viongozi wote ambao wanahusika na masuala ya Muungano kwanza watuletee idadi ya watumishi waliopo, lakini pili watuletee mpango kazi wa kufikia *quota* iliyokubalika ya taasisi za Muungano ziwe na uwiano sahihi wa kimuungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu na mwisho ni kwamba Serikali ilishafanya uamuzi wa kufungua Ofisi ya Tume ya Ajira Zanzibar kwa sababu moja ya changamoto ilikuwa ni kwamba Tume ya Ajira ambayo inaajiri hawa watendaji na watumishi wengineo ipo Bara peke yaake na hizi nafasi wakati mwingine hazifahamiki au hazifikiwi na watu wa upande wa Zanzibar, kwa hiyo, ofisi hii sasa imefungua ofisi yake Zanzibar na nafasi zitatangazwa kwa upana wake kwa watu wa Zanzibar na wenyewe wataziomba ili waweze kupata fursa za kushiriki katika taasisi za Muungano.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea. Swali namba 26 linaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa, Mbunge wa Bagamoyo.

Na. 26

**Mgogoro wa *TANAPA* na Jirani Zake**

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA** aliuliza:-

Kumekuwa na mgogoro wa muda mrefu wa mipaka kati ya *TANAPA* na vijiji na vitongoji jirani vinavyowazunguka.Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza mgogoro huu kati ya *TANAPA* na vitongoji vya Kitame, Razaba, Gama-Makani katika Kata ya Makurunge?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, Mbunge wa Bagamoyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro yote mitatu iliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge inahusiana na hifadhi ya Taifa Saadani iliyoanzishwa kisheria kwa Tangazo la Serikali Namba 281 la mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro baina ya Kitongoji cha Kitame, Kijiji cha Makurunge na hifadhi umetokana na malalamiko kwamba wananchi hawakushirikishwa katika zoezi la uwekaji wa mipaka hivyo kusababisha yaliyokuwa maeneo yao kuingizwa ndani ya hifadhi bila ridhaa yao. Hata hivyo, kumbukumbu zinaonyesha kwamba kuwa wananchi walishikikishwa kikamilifu

kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu ikiwa ni pamoja na kufanyika kwa mkutano wa kijiji mama cha Makurunge ambacho kitongoji hiki ni sehemu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro baina ya shamba la Razaba na hifadhi umetokana na utata wa takribani eneo la hekta 3,441 alilopewa mwekezaji *Bagamoyo Eco-Energy* kwa hati miliki namba 123097 ya terehe 9 Mei, 2013 ili amiliki na kuendesha shughuli za kilimo  cha miwa katika eneno ambalo kiuhalisia limo ndani ya hifadhi ya Taifa ya Saadani. Juhudi za kutatua mgogoro huu ziliendelea kufanyika kwa takribani miaka minne kwa kuhusisha ngazi za Vijiji, Wilaya, Mkoa na Wizara zinazohusika na hatimaye kutolewa maelekezo kupitia agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu agizo ambalo lilizingatia athari za mazingira zilizotishia uwepo wa hifadhi ya Saadani iwapo kilimo cha miwa kingeruhusiwa katika eneo linalozungumziwa.

Mgogoro baina ya Gama -Makani na hifadhi unatokana na malalamiko ya wananchi kuwa baadhi ya waliofidiwa wakati wa uanzishwaji wa hifadhi katika eneo hilo hawakuwa wamiliki wazawa wa maeneo hayo. Hata hivyo taarifa zinaonyesha kuwa mchakato wa malipo ya fidia ulifuata taratibu muhimu ikiwemo ushirikishwaji wa karibu wa uongozi wa Wilaya ya Bagamoyo, Serikali za Kata na Serikali za Vijiji husika ambao ulizingatia ilivyohitaji la kuwalipa wananchi waliostahili na si vinginevyo.

Pamoja na maelezo haya, Serikali imekwishaunda timu ya pamoja ya wataalam ambayo inaendelea na kazi ya kutafuta suluhisho la migogoro ya ardhi nchini ikishirikisha Wizara mbalimbali kama ilivyoahidiwa wakati wa Bunge la Bajeti lililoahirishwa mwezi Juni, 2016.

**MWENYEKITI:** Ahsante! Mheshimiwa Shukuru Kawambwa, Dokta.

**MHE. DKT. SHUKURU KAWAMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ingawa ni majibu ambayo mimi na wananchi wangu wa Bagamoyo yanatupa matatizo. Sasa naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja naomba kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kama atakubali kuielekeza timu hii ya pamoja iliyoundwa ili iweze kukutana na wawakilishi wa wananchi hawa akiwemo Mbunge na Waheshimiwa Madiwani wa jimbo la Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, *TANAPA* inawatoza fedha wananchi wa Makurunge na Matipwili wanapovuka daraja eneo la Gama katika Mto wa Wami wanapokuwa wanafanya shughuli zao, mtu Shilingi 5,000 na gari Shilingi 25,000, je, nini kauli ya Serikali kuhusu uhalali wa tozo hiyo?

**MWENYEKITI:** Ahsante! Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, *Engineer* Makani, majibu!

**NAIBU WAZIRI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dokta Shukuru Kawambwa Mbunge wa Bagamoyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, ushauri alioutoa nitaufikisha mbele ya Kamati hii maalum. Kwamba pamoja na utaratibu waliojiwekea wa kuweza kutimiza malengo yao kwa mujibu wa kazi walizopewa na hadidu za rejea.Ni jambo jema na ni wazo zuri na litaweza kuboresha matokeo ya kazi wanayoifanya kwa kuwashirikisha pia Mheshimiwa Mbunge pamoja ma Madiwani wanaohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili linlohusiana na *TANAPA* kuwatoza wananchi ada hizi; kwanza nalisikia kwa mara ya kwanza na kwa kuwa ni suala jipya kujua mantiki yake na sababu zake kwanini liko hivyo nahitaji muda kidogo, lakini kwa wakati huu nikiwa nimesimama hapa naliona lina ukakasi wa namna Fulani. Kwa hiyo namuomba Mheshimiwa Mbunge anipe nafasi, nalishughulikia mara moja katika kipindi hiki hiki cha Bunge na pengine kwasababu ya uzito wake kuwa mkubwa, mchana huu nikutane naye, nitakuwa nimeshafanya mawasiliano angalau ya awali kujua likoje halafu tuweze kutafuta suluhisho lake.

**MWENYEKITI:** Ahsante, waheshimiwa Wabunge muda; tunaendelea. Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga anauliza swali linalofuata namba 27.

Na. 27

**Kimondo cha Mbeya**

**MHE. JAPHET N. HASUNGA** aliuliza:-

Katika eneo la Ndolezi Wilaya ya Mbozi kuna kimondo ambacho ni cha aina yake katika nchi hii na dunia kwa ujumla:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhamasisha watalii wa ndani na nje ya nchi kuja kukiangalia Kimondo hicho ili kuchangia pato la taifa?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii napenda kujibu swali la Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga Mbunge wa Vwawa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubalina na Mheshimiwa Mbunge kuwa Kimondo hiki kilichopo Kusini Magharibi mwa Kilima cha Marengi, Kijiji cha Ndolezi Wilaya ya Mbozi, Mkoani Mbeya ni cha kipekee hapa nchini, na kwakweli na duniani kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na taarifa za kitaalamu kimondo hiki kinaaminika kuwa kati ya vimondo nane vikubwa zaidi duniani kikikadiriwa kuwa na uzito wa tani 12, urefu wa mita 3.3, upana wa mita 1.63 na kimo cha mita 1.22. Sehemu yake kubwa ni chuma ambayo asilimia 90.45 na sehemu iliyobaki inajumuisha nikeli asilimia 8.69, shaba asilmia 0.66, *sulphur* asilimia 0.01, fosfori asilimia 0.11. Kwa kuzingatia upekee na umuhimu wake, mwaka 1967 kilitangazwa kuwa Urithi wa Taifa kwa tangazo la Serikali Na. 90 la tarehe 1967. Taarifa kuhusinaa na tarehe na mwaka wa kuanguka kwa kimondo hiki bado haijulikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeendelea kutangaza Kimondo cha Mbozi kama moja ya vivutio muhimu na adimu nchini na duniani. Uhamasishaji umefanyika kwa kutumia njia mbalimbali ndani na nje ya nchi, ikiwa ni pamoja na vipindi vya runinga vya zamadamu (Televisheni ya Taifa *TBC*1) na utalii wa ndani kupitia Kituo cha *Channel Ten*. Pia machapisho ya Tanzania; *The Land of Great Heritage Sites* na *Tanzania Cultural Heritage Resources* ambayo nakala zake pia husambazwa katika maonesho mbalimbali na balozi zetu nje ya nchi. Machapisho mengine ambayo hutolewa kwa Kiswahili ni pamoja na Jarida la Ifahamu Idara ya Mambo ya Kale na Jarida la Maliasili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo na picha za kimondo hiki pia vimewekwa katikatovuti na mitandao mbalimbali duniani. Juhudi hizi pamoja na nyingine zimeendelea kuonesha matunda kwani takwimu zinaonesha kuongezeka kwa idadi ya watalii na mapato. Kwa mfano kati ya mwaka 2012/13 na 2014/2015 watalii waliongezeka kutoka jumla ya 990 hadi 1,681 na mapato kuongezeka kutoka Shilingi 811,000 hadi 2,426,000.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Japhet Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Pamoja na majibu haya ambayo ameyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mazingira ya kimondo chenyewe yako kwenye hali mbaya sana, na ukiangalia miundombinu na barabara zinazoenda kule ziko kwenye hali mbaya sana, hivi sasa hivi kimondo kile hata uzio wa kukizunguka kimondo kile ku-*protect* haupo. Sasa je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha mazingira ya kimondo kile ili kiwe ni kivutio kizuri

sana kwa utalii pamoja na kuinua pato la Mkoa mpya wa Songwe na Jimbo langu la Vwawa?

Mheshimiwa MWenyekiti, swali la pili; kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi ilishaandika barua ya kuomba Wizara hii ikikabidhi kimondo kwenye Halmashauri ili waweze kukiendeleza na kuweka vivutio mbalimbali ikiwa ni pamoja na migahawa, hoteli na vitu mbali mbali vitakavyowavutia watalii wa ndani na nje, Serikali ni lini sasa itakubali kukikabidhi kimondo hicho katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi?

**MWENYEKITI:** ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri, Maliasili na Utalii *Engineer* Makani, majibu, lini unakabidhi hicho kimondo?

**NAIBU WAZIRI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga Mbunge wa Vwawa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza linahusu changamoto ya miundombinu kutokuwa bora au kutokuwa rafiki kwa shughuli za utalii kwenye eneo hili ambako kimondo chetu kipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua wazi kwamba ili kuweza kuboresha utalii miongoni mwa maeneo ambayo yanatakiwa kutiliwa mkazo, na kwakweli yanatiliwa mkazo na Serikali, ni pamoja na kuboresha miundombinu kwenye maeneo yenye vivutio kama hili la kwenye kimondo cha pale Mbozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ya Serikali ambayo ametaka kuifahamu Mheshimiwa Mbunge ni kuboresha miundombinu hiyo kwa kutumia bajeti zake lakini pia kwa kushirikisha wadau. Kwa hiyo wakati Serikali inaendelea na utaratibu wa kutumia fedha zake za bajeti kuboresha miundombinu bado mheshimiwa Mbunge kwa kuungana na Serikali aweze kutafuta namna ambayo anaweza kushirikiana na Serikali kuweza kuwafikiwa wadau mbalimbali kwenye eno la Mbozi ikiwa wanaweza kufanya jitihada kuungana na Serikali katika kuboresha miundombinu kama alivyoitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na kimondo kukabidhiwa kwa Halmashauri, suala hili haina tofauti kubwa sana kiuendeshaji, Serikali ni ile ile, Halmashauri bado ni Serikali na Serikali kuu bado ni Serikali. Mawazo mema na mazuri yanaweza kupokelewa kulingana na ubora wake na wakati. Kwa hiyo nimshauri mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Halmashauri na washauri waweze kutuandikia Wizarani tutaweza kupima kuona ikiwa sababu hizo za kukabidhi kimondo hicho kwa Halmashauri linaweza likafanya eneo hilo likafanyika utalii kwa namna bora zaid na kwa tija zaidi kuliko ilivyo sasa.

**MWENYEKITI:** Ahsante,Waheshimiwa tunaendelea. Swali namba 28 linaulizwa na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 28

**Matumizi ya Fedha za Mfuko wa Pamoja wa Afya (*Health Basket Fund*)**

**MHE. CECILIA D. PARESSO** aliuliza:-

Mwongozo wa fedha za wafadhili wanaochangia katika Sekta ya Afya (*Health Basket Fund*) katika Halmashauri zetu unaelekeza asilimia 33 ya fedha hizo zitumike kwa manunuzi ya dawa na asilimia 67 zitumike katika shughuli za utawala, uaimamizi na ufuatiliaji;

(a) Je, Serikali haioni ni wakati muafaka sasa kubadili mongozo huu?

(b) Je, ni lini Serikali taacha kutegemea fedha za wafadhili na hasa katika Sekta ya Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsate. Kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso Mbunge wa Viti maalum lenye sehemu A na B kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haiwezi kubadili mwongozo wa mgao huo kwasababu unalindwa na makubaliano baina yake na wadau wa mfuko wa pamoja wa Afya (*Health Basket Fund*). Hata hivyo, kwa kuzingatia mahitaji ya sasa Serikali inaangalia uwezekano wa kufanya mapitio ya makubaliano hayo na wadau wa *Health Basket Fund.*

(b) Mheshimwa MWenyekiti, Serikali haitegemei fedha za wafadhili kuendesha huduma za Afya kwa asilimia 100. Wafadhili wanachangia tu gharama za baadhi ya huduma. Uchumi wa nchi yetu utakaporuhusu utegemezi utapungua kama siyo kwisha kabisa. Hata hivyo, katika kuelekea kujitegemea, Serikali imetengeneza mkakati wa ugharamiaji huduma za afya na imeandaa mapendekezo ya Sheria ya Bima ya Afya kwa wote ambayo yatawasilishwa hapa Bungeni pindi mchakato wa ndani ya Serikali utakapokamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatarajiwa Sheria hii kama itapitishwa na Bunge lako tukufu kila Mtanzania atapata huduma za Afya kwa kadi yake bila kiwazo cha kifedha.

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa majibu. Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa mahitaji ya Sekta ya Afya hapa nchini yapo, yalikuwepo na yataendelea kuwepo, ni kwanini Serikali mlikubali kuingia mkataba huu au makubaliano haya ya fedha hizo asilimia 33 zinaenda tu kwenye ununuzi wa dawa na asilimia 67 inaenda kwenye fedha hizo zinaenda kwenye masuala ya usimamizi na ufuatiliaji kwa maana ya *administrative cost*, ni kwanini mliingia makubaliano haya amabyo hayana manufaa kwa Sekta ya Afya hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Serikali imesaini Abuja *Declaration* ya kutaka asilimia 15 ya bajeti yake iende katika sekta ya afya. Ni ukweli usiopingika kwamba sekta ya afya hapa nchini kwenye zahanati zetu, vituo vya afya, hospitali za wilaya ina changamoto kubwa sana ikiwemo ukosefu wa dawa, lakini leo hatujui kipaumbele cha Serikali ni nini. Serikali leo inang'ang'ana kuhamia Dodoma wakati kwenye hospitali zetu hakuna dawa hata kidogo. Ni kwanini hamuwi na vipaumbele vya afya ya Watanzania kwanza kuliko haya mengine? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Dkt. Kigwangalla.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwamba kwanza ni kwanini Serikali iliingia makubaliano haya? Jibu ni rahisi tu, kwamba fedha za *Health Basket Fund* ni fedha za ziada za nyongeza ambazo tunapewa na wafadhili wetu. Sasa haiwezi kutokea mtu akaja akasema nakuongezea kitu kutatua changamoto inayokukabili halafu ukakataa. Kwa hivyo kulikuwa hakuna sababu ya Serikali kusema eti ijiulize maswali mara mbili mbili wakati imepata wafadhili na wafadhili wanakuja kuongeza tija kwenye kutoa huduma za afya kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zaidi ya hapo, fedha hizi kutengwa, kwamba asilimia 33 iingie kwenye dawa na asilimia 67 iende kutumika kwa ajili ya ku-*administrate* mfumo mzima wa afya kwamba sio jambo la muhimu; pengine Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso ungejifunza kwa ukaribu zaidi namna ya ku-*administrate* mambo ya mfumo wa afya. Mfumo wa afya ni katika

mifumo *complex* ambayo unaweza ukaikuta hapa duniani, na si kazi rahisi ku-*administrate* utoaji wa huduma za afya. Wewe unapokwenda hospitali unaona ni kitu kirahisi tu unapoonwa na daktari na ukapewa dawa, lakini nyuma ya hiyo *visit* yako moja ambayo unaenda kuipata kwa daktari ukae ukijua kuna mchakato mrefu sana wa ku-*administer* mfumo mzima mpaka kufikia hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa afya unaendana na mambo kama ufuatiliaji, tathmini, tafiti, *surveillance* za muda mrefu pamoja na kukusanya takwimu. Haya ni mambo mhimu sana ambayo Serikali yetu kwa kweli haikuwa ikiwekeza kabla ya kupata hizi pesa za *Health Basket Fund*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzipata wafadhili wakasema kwamba ni lazima watusaidie katika eneo hili kwa kiasi kikubwa. Lakini hata hivyo kwenye jibu langu la msingi nimesema tunaangalia uwezekano kwa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri wakati akisoma hotuba yake ya bajeti hapa katika mwaka wa fedha unaokuja tufanye mapitio ili sehemu kubwa zaidi ya fedha hizi ziweze kuwekezwa kwenye dawa kama ambavyo tumefanya mabadiliko kwenye pesa zinazotokana na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusu *Abuja Declaration. Abuja declaration* kweli ni *commitment* ambayo nchi yetu iliingia kwenye miaka ya mwanzo ya 2000, kwamba tutatenga asilimia 15 ya bajeti yote kubwa kwenye sekta ya afya. Serikali yetu kwa nyakati mbalimbali imekuwa ikifanya jitihada hizo za kuongeza bajeti kwenye sekta hii, lakini bahati mbaya sana ukuaji wa uchumi haukuweza kuendana na kasi ya mahitaji yetu makubwa ya kuwahudumia Watanzaia kwenye sekta ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ifahamike hapa kwamba huduma za afya ni katika huduma zenye gharama kubwa sana kwenye taifa lolote lile; na kwa maana hiyo kusema uchumi wetu huu mdogo unaweza ukakidhi mahitaji yote si jambo la rahisi na si jambo la kusema linaweza likafikiwa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Serikali ya Awamu ya Tano kupitia maelekezo yaliyopo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM tumejikita kwenye kuitafsiri Ilani ile kwa kuhakikisha tunaanzisha Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ambao utamlazimisha kila Mtanzania kuwa kadi ya Bima ya Afya ili wananchi washiriki kwenye kuchangia huduma kabla ya kuzitumia, tukiamini kwamba kama kila Mtanzania atakuwa na Bima ya Afya maana yake atakuwa na uhakika wa kupata huduma hizo pale ambapo anazihitaji bila kupata changamoto ya kifedha, na hii ni njia mojawapo ya kukusanya pesa kwa watu wengi zaidi ambayo kwa kiasi kikubwa inaendana na misingi ya Sera ya Ujamaa na Kujitegemea ambayo sisi wa Chama Cha Mapinduzi tunaisimamia.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea, swali namba 29 linaulizwa na Mheshimiwa Halima Abdallah bulembo.

Na. 29

**Vituo vya Kulelea Watoto Wasio na Makazi**

**MHE. HALIMA A. BULEMBO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha vituo vya kulelea watoto wasio na makazi katika kila kanda nchini na kuwjajengea stadi za kazi na ujasiriamali?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima, Abdallah Bulembo Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua haki ya msingi ya mtoto ya kulelewa katika familia Serikali kwa sasa haina mpango wa kuanzisha vituo vya kulelea watoto wasio na makazi katika kila kanda nchini kwa sababu jukumu la kutoa malezi kwa watoto ni la wazazi ama walezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, pale ambapo wazazi ama walezi wamefariki au kwa sababu moja au nyingine wameshindwa kuwalea watoto, jukumu hio linapaswa kuchukuliwa na ndugu ama jamaa au wana jamii wengine. Lakini pale inaposhindikana watoto hao hulazimika kulelewa katika makao kwa ajili ya malezi ikiwa ni hatua ya mwisho baada ya njia nyingine kushindikana. Na wanapokuwa makaoni hupatiwa huduma zote za msingi kama chakula, malazi, matibabu, elimu ya msingi na sekondari, msaada wa kisaikolojia na kijamii na stadi za maisha, ufundi na ukasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inaendelea kutekeleza Mpango wa Ulinzi na Usalama wa Mtoto kwa Mwaka 2013/2017 katika jitihada za kuboresha malezi ya watoto kwa kuimarisha mfumo wa malezi, matunzo na ulinzi wa watoto katika ngazi ya familia na jamii. Kupitia mpango huo Wizara kwa kushirikiana na mamlaka za Serikali za Mitaa, pamoja na wadau wa maendeleo imeanzisha timu za ulinzi na usalama wa mtoto katika ngazi ya halmashauri, kata na vijiji ama mitaa katika halmashauri 38 nchini. Zoezi la uanzishwaji wa timu hizi linaendelea ili kufikia halmasahuri zote nchini.

**MWENYEKITI:** Asante, Mheshimiwa Halima Abdallah Bulembo swali la nyongeza kwa ufupi.

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii. Watafiti Joel Lugala na Jesse Mbwambo katika andiko lao la kitafiti linalosema au lililoandikwa *street children and street life in urban* Tanzania; *the culture of surviving and its implication for children health* la mwaka 2013; watafiti hawa katika hitimisho lao wanasema, Serikali ya Tanzania hailijui tatizo la watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Na kwa majibu ya Serikali ni dhahiri tatizo hili halieleweki na hitimisho hili ni thabiti. Je Serikali itachukua hatua gani kulielewa tatizo hili kwani linazidi kukuwa siku hadi siku? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali inatambua mfumo wa uchumi umebadilika hayo yanayosemwa kwamba watoto watalelewa na ndugu, au walezi hayapo kwa sasa. Watoto yatima wamekuwa wakinyanyaswa, wakidhulumiwa mali zao na ndugu wa wazazi; je, Serikali ipo tayari kubadili mtazamo wake kuhusu watoto wanaoishi katika mazingira magumu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Halima Abdallah Bulembo, Mbunge wa Viti Maalum kwa swali lake zuri la nyongeza aliloliuliza, lakini pili akiwa Mbunge mdogo kuliko wote hapa Tanzania amekuwa siku zote mstari wa mbele kutetea haki za vijana na watoto. Ni Mbunge wa kutiliwa mfano na ninakupongeza na ninaomba uendelee kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujibu swali Lake…

**MHE. MARIAM:** *(Aliongea nje ya kipazasauti, hakusikika)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Nalijibu Mariam haraka za nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujibu swali lake napenda kusema na narudia tena kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, kwamba mtazamo na msimamo wa Serikali uko wazi na hautotetereka. Kwamba sehemu ya kwanza na ya muhimu na ya lazima kwa malezi ya mtoto wa Kitanzania ni kwenye familia yake. Kama imetokea kwa sababu moja ama nyingine wazazi wamefariki ama hawana uwezo wa kutoa malezi yanayohitajika kwa mtoto,

familia pana *(extended family)* inapaswa kuchukua jukumu hilo na kama haiwezekani jamii pana inapaswa kuchukua jukumu hilo. Yote haya yakishindikana, sasa inakuwa ni wajibu wa Serikali kuwachukua watoto hawa na kuwatunza kwenye makao maalum kwa ajili ya malezi ya watoto, huo ndio msimamo wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na msimamo huu haimaniishi kwamba Serikali hailielewi tatizo hili, tatizo hili tunalifahamu, Serikali imefanya tafiti mbalimbali, na pamoja na hiyo tafiti ya akina Joe Lugala na wenzake tunaifahamu, na tumeifanyia, kazi na haimaanishi kwamba tafiti hiyo basi ndio hiyo hiyo tu hakuna tafiti nyingine na kwamba inatoa mwongozo wa kila kitu hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tafiti nyingi zimefanyika na zote tunazichambua na tunazifanyia kazi. Naomba nimtoe shaka Mheshimiwa Halima Bulembo kwamba Serikali iko macho kuhusiana na suala hilila malezi ya watoto, na kwamba tutaendelea kusimamia msimamo wetu, kwamba kisaikollojia, kijamii, na kwa maana ya kutoa ulinzi stahiki na mapenzi yanayohitajika kwa watoto wa nchi hii Serikali itakuwa mstari wa mbele. Nitoe rai kwenu nyote Waheshimiwa Wabunge na watanzania wote kwa ujumla mnaonisikiliza tujitahidi kuwalea watoto na kuhamasisha jamii ziwalee watoto kwenye *unit* ya *family*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.*(Makofi)*

**MMWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana, lakini nataka kuongeza suala moja. Kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, jukumu la kwanza la malezi ya mtoto liko chini ya wazazi la pili familia. Lakini kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto, kifungu cha 94 kinasema ni jukumu la Serikali za Mitaa kuhakikisha kinachukua hatua zote za kuhakikisha watoto wanaoishi katika mazingira magumu haki zao zinatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kusisitiza Wabunge wote, ni Wajumbe wa baraza la Madiwani. Sisi Wabunge tumechukua hatua gani ya kuhakikisha watoto yatima katika wilaya zetu, katika halmashauri zetu wanapata haki ya elimu, wanapata haki ya elimu ya ufundi wanapata malazi, na wanapata chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hili jambo si la Serikali kuu ni jambo letu sisi wote Wabunge, tunapokaa kwenye mabaraza ya madiwani tujiulize mmechukua mikakati gani ya kupambana na tatizo la watoto yatima na

watoto wa mitaani. Niliona niiweke hivyo wazi, wakisubiri Wizara ya Afya wao wakae tu kama si kipaumbele chenu haliwezi kuwa kipaumbele cha Watanzania kama sisi Wabunge hatutatia mkazo suala la watoto yatima,

Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Asante sana Mheshimiwa Waziri kwa maelezo, tunaendelea, swali letu la mwisho Mheshimiwa Khamis Mtumwa Ali Mbunge wa kiwengwa.

Na. 30

**Huduma ya Umeme – Vituo vya Polisi Zanzibar**

**MHE. KHAMIS M. ALI** aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa baadhi ya wakuu wa Vituo vya polisi hasa Zanzibar hutumia pesa ao za mishahara kulipa huduma za umeme katika vituo hivyo;

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuwalipa au kuwarejeshea pesa wanazotumia kulipa umeme katika vituo hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khamisi Mtumwa Ali Mbunge wa Kiwengwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikirejesha fedha hizo za umeme endapo askari amelipia au amenunua umeme kwa ajili ya kituo cha polisi kwa kupitia utaratibu wa kujaza fomu za madai na kuambatisha risiti ya malipo hayo kisha kuziwasilisha kwa mhasibu kwa ajili ya malipo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo Wizara yangu imekuwa ikijitahidi kupeleka fedha za kulipia umeme kwa wakati ili kuondoa usumbufu unaojitokeza kwa askari walioko vituoni na makambini kadri ya hali ya uwezo utakapokuwa unaruhusu.

**MWENYEKITI:** Asante, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Mtumwa Ali swali la nyongeza.

**MHE. KHAMIS M. ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza je. La kwanza, je Serikali haioni utaratibu huu wa askari au wakuu wa vituo kujaza fomu na kupeleka risiti

unaonesha urasimu, na inapelekea hadi askari anastaafu kutokulipwa pesa zake hizi za kulipa umeme?

Lakini la pili kwa upande wa askari wadogo ambao si maafisa kwa nini wasiwekewe pesa zao za posho za umeme na maji katika mishahara yao kama wanavyofanya JWTZ? Nashukuru.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Khamis Mtumwa, Mbunge wa Kiwengwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na swali lake la pili, ukweli ni kwamba sio askari wote ambao wanalipwa posho kuna askari ambao hawalipwi posho, kuna askari ambao wanaishi katika nyumba binafsi ambao ndio wengi. Kama unavyofahamu Waheshimiwa Wabunge sasa hivi tuna changamoto ya makazi kwa askari, ambao hawa kiutaratibu wanalipwa posho ya pango ni asilimia 15 ya mshahara. Kwa hiyo hawa hawana shida. Tatizo lilipo ni kwa wale askari ambao wanaishi kwenye nyumba za askari ambapo wakati mwingine kuna tatizo la kuchelewa kwa posho zao. Hata hivyo Serikali imejitahidi kuhakikisha kwamba madeni yote yakiwemo haya ya posho mbalimbali yanalipwa. Na tumekubaliana kufanya uhakiki, ambao tayari umeshakamilika, kwa madeni yote ya kuanzia mwaka 2014 mpaka 2016 na wakati wowote yanatarajiwa kulipwa kupitia hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusiana na swali lake la kwanza ambapo alizungumzia kuchelewa kwa malipo hayo hadi kufikia wakati askari wanastaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge kuna sababu nyingi ambazo zinasababisha ucheleweshwaji wa malipo ya madeni haya. Moja kama ambavyo mnafahamu wakati mwingine kunakuwa na ucheleweshaji wa kupata fedha za bajeti ama wakati mwingine zinakuja kidogo. Lakini pia wakati mwingine hata ambapo zinapokuja kuna matukio ambayo mara nyingi hatuyatarajii, ambayo yanajitokeza yanafanya matumizi yale yaweze kuhamishiwa na kutekeleza yale matumizi ya dharura, ikiwemo ya ujambazi, migogoro ya kijamii, hata operesheni za baadhi ya wanasiasa zisizokuwa na tija. Haya mambo na mambo mengine yanachangia wakati mwingine kufanya fedha hizi zitumike kwa matumizi mengine ya dharura na kuchelewesha malipo yale.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mwongozo

**MWENYEKITI:** Tuzingatie, nikisimama wote mnaketi, nimesimama. Waheshimiwa Wabunge angalieni muda. Kipindi cha maswali kwa muda au

mkutano ambao si wa bajeti, ni saa moja na nusu, dakika 90. Nimejitahidi kuzuia maswali ya nyongeza lakini tatizo bado naliona. Baadhi ya maswali ni marefu lakini pia na majibu sasa marefu, halafu usomaji pia hauna ile kasi ya kuweza kuokoa muda. Nawasihi sana viongozi Mawaziri tujitahidi katika hilo maana maswali yanaulizwa *specific* na mnapoyachuja mnaona anatafuta nini. Kwa hiyo tukienda kwa namna hiyo tutazingatia muda ambao tumepewa. Lakini pia na maelezo ya dibaji kwenye maswali, nenda tu moja kwa moja kwenye swali lako; hii zungukazunguka  mpaka bariadi unarudi halafu ndio unakuja kutua Dodoma haisaidii. *(Makofi)*

Hilo ni muhimu sana na Mheshimiwa Spika, naye alilisema lakini ni la kikanuni. Tumemaliza kipindi cha maswali, kama kawaida tuna shughuli za kazi, lakini nianze kwanza kutambua wageni ambao wametufikia siku ya leo.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii kuna mgeni yupo katika jukwaa la Spika, ni mgeni wa Mheshimiwa Freeman Mbowe kiongozi wa Upinzani Bungeni ambaye ni mtoto wake, Ndugu Clinton Mbowe, karibu sana, sijui na sina hakika kama unataka kufuata nyayo za baba yako. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Tunao wageni wawili wa Mhesimiwa Alex Gashaza ambao ni Dkt. Derick Nyasebwa, Dakari wa hospitali ya Uhuru Jijini Mwanza na ndugu Christopher Kilaja Katibu wa Fedha na Uchumi wa CCM Wilaya ya Muleba, karibuni sana wageni wetu . *(Makofi)*

Tunao wageni 39 wa Mheshimiwa Daniel Mtuka, Mbunge ambao ni wanafunzi 30 na walimu 9 kutoka Manyoni Mkoa wa Singida wakiongozwa na ndugu Iddy Majiyamoto, Mwenyekiti wa CCM Kata ya Kintinku, karibuni sana walimu karibuni sana na wanafunzi someni kwa bidiii.*(Makofi)*

Tuna wageni 5 wa Mheshimiwa Constantine Kanyasu  ambao ni viongozi wa Chama cha wafanyakazi Geita *Gold Mining (TAMICO)*  kutoka Mkoani Geita wakiongozwa na ndgugu Gideon Kagora Mwenyekiti wa *TAMICO (GGM)*na ndugu Julius Stephin Katibu *TAMICO (GGM),* karibuni sana Dodoma na Bungeni.

Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Victor Mwambalasa ambao ni watoto wake wanatokea mkoani Dodoma ambao, ni ndugu Fatma Mohamedy na Latiffer Shemgaa.

Kuna wageni watatu pia wa Mheshimiwa Ally Ungando ambao ni ndugu zake kutoka Kibiti Mkoani Pwani, ni ndugu Hassan Kitabu, ndugu Juma Dusu, na ndugu Salum Nakanoga. Karibuni sana kutoka Rufiji.

Wageni wawili wa Mheshimiwa Boniventure Kiswaga ambao ni walimu wa Sekondari na wapiga kua wake kutoka Magu Mkoani Mwanza, ndugu James Mchembe na ndugu Harman Nkwabi karibuni sana ndugu zetu. Hao ndio wageni tulionao kwa siku ya leo.

Matangazo ya kazi, ninalo moja. Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji leo saa saba mchana baada ya shughuli za Bunge kusitishwa kutakuwa na kikao cha kamati hiyo katika ukumbi wa Msekwa C, mnahimizwa Wajumbe wa kamati hiyo kuhudhuria kikao hicho. Tangazo la kazi ni hilo tu.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Mwongozo nilitegemea sasa tuanze kuchukua majina mwongozo Mheshimiwa Keisy nimekuona, mwongozo mwingine nani …

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Malocha,

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Oscar MukasaMalocha

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Musukuma

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Malocha.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MWENYEKITI:** Bado, Mheshimiwa Msukuma, ninao wane jamani wanatosha.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MWENYEKITI:** Nianze na Mheshimiwa Keissy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Nachukua mwongozo wa kifungu namba 46(1) kuhusiana na swali la nyongeza alilouliza Mheshimiwa Msukuma na kujibiwa na Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Sikuridhika nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kweli imekuwa kwamba nchi ikitokea njaa anaadhibiwa mkulima, mkulima kalima kwa hela zake hakusaidiwa chochote na Serikali lakini anapata adhabu kutokana na njaa popote atakapokuwa katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kujua hifadhi ya Taifa natoleaa mfano Wilaya ya Kansi tumelima tani 55,000 za mahindi, hifadhi ya Taifa

imenunua tani 5,000 tani 50,000 watapeleka wapi? Mpunga Mwambao wa Ziwa Tanganyika Serilkali hifadhi ya Taifa hata mwaka mmoja haijanunua mpunga. Mpunga ulikuwa 45, 000/= leo imefika 25,000/= na hakuna pa kuuza. Hakuna siku yoyote hifadhi ya taifa ikanunua mihogo leo wananchi wanakataliwa kupeleka mihogo popote pale, hata Burundi. Ikitokea njaa anadhibiwa mkulima wakati mtumishi akipata hela zake za mishahara ananywea pombe anahonga haulizwi hela zake, lakini kwa mkulima imekuwa adhabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Serikali inaonea wakulima ndugu zangu. Ni tathmini gani tangu mwezi wa saba mpaka mwezi wa tisa tathmini hawajafanya? miezi mitatu! Na kila sehemu kuna Wizara ya kilimo kila kijiji, tathmini gani inafanya? Inakuwa ni kuwaadhibu wakulima wetu hawana pa kwenda, hawana pa kuhifadhi mazao, mazao yako nje na msimu wa mvua uko karibu kuingia. Leo tunaadhibu wakulima wakati mnasema limeni ni uti wa mgongo kilimo. Kilimo katika nchi hii kinakuwa adhabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haturidhiki na Wizara ya Kilimo, inakuwa ni adhabu kwa wakulima wetu. Wakulima wetu wanatupa kura, tunakuja hapa sisi na kulipwa posho, leo tunawaadhibu wakulima kwa sababu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali itoe tathmini na iruhusu haraka sana. Kuna kiwanda cha *milling* kule Sumbawanga, kimesaga unga wananunua *Wakongo-man* kwa Dola, unafika Kigoma tani 450 wamezizuia mpaka unga unataka kuharibika Kigoma, kwa sababu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani mnasema kuna sikukuu ya wakulima kuna sikukuu ya wakulima wakati mnaadhibu wakulima nchi hii! Nataka jibu leo hii wakulima wapate nafuu, hawana pa kupeleka mazao yao. *(Makofi/Vigelegele)*

**MWENYEKITI:** Huo ni Mwongozo eeh! Mheshimiwa Malocha.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Mwongozo wangu ni kwa mujibu wa Kanuni ya 46, japokuwa nimetanguliwa na Mheshimiwa Keissy, lakini Mwongozo wangu ni kwamba, naomba Serikali ilete Taarifa ya Chakula nchini ili Waheshimiwa Wabunge waweze kujadili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Malocha, nisaidie umesimama kwa mujibu wa Kanuni ipi?

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa mujibu wa Kanuni Namba 46 na kutokana na swali la nyongeza la Mheshimiwa Musukuma lilivyokuwa limejibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo na Ushurika.

**MWENYEKITI:** 46(1) inasema nini?

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja nisome. Kanuni inasema:-

*Waziri anayeulizwa swali atakuwa na wajibu wa kulijibu swali hilo kwa ukamilifu kama lilivyoulizwa, isipokuwa kwamba, kama jibu husika ni refu au lina takwimu nyingi Waziri atampa Mbunge muuliza swali nakala ya jibu.*

**MWENYEKITI:** Sawa kabisa, nimekuelewa. Mheshimiwa Oscar Mukasa!

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. Nasimama kwa mujibu wa Kanuni 68 (7) sambamba na 46 (1).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha wakati anajibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chatanda ambalo msingi wake ulikuwa swali namba saba amelieleza Bunge kwamba, waajiri ndio wanaosababisha ucheleweshaji wa malipo ya pensheni ya watumishi wanaostaafu. Na kwenye maelezo yake amejikita kwenye kutoa rai, lakini hakuna mahali ambapo ameeleza namna gani Serikali inachukua hatua zenye meno ili kuzuia waajiri wasisababishe ucheleweshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Mwongozo wa juu ya namna gani majibu yake yanakidhi haja ya swali lililoulizwa? Na ikiwezekana namna gani tunaweza kupata majibu yanayokidhi haja hiyo ya Watanzania wanaostaafu na kucheleweshewa mafao. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nasimama kwa Kanuni hiyo ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyouliza swali la nyongeza pengine Waziri hakunielewa. Nimesema baada ya Serikali kuzuia wananchi kusafirisha mazao nje, hususan Kanda ya Ziwa na Mikoa mingine, Serikali haikuwa na maandalizi ya ma-*godown* ya kutunzia vyakula vya wale wakulima. Sasa vile vyakula vimerundikwa nje tu mabarabarani kwenye mashine na sasa tunaenda kwenye msimu wa mvua, Serikali imeandaa nini cha kuweza kuwalinda wale watu ili

yale mazao, wakati utafiti ukiendelea kufanyika yasiharibike na mvua? Alivyojibu hakujibu nilivyouliza swali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge mlioomba Miongozo, na mmeingilia mahali sahihi, kwa maana kwamba Kanuni ya 68 (7). Ili twende pamoja tu, Mwongozo wa Spika unahusu nini juu ya jambo ambalo limetokea Bungeni mapema siku hiyo, kama ilivyofafanuliwa, ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na Taratibu za Bunge. Na majibu ya Spika yanaweza yakatolewa papo hapo au badaye.

Lakini pia wote mmeegemea zaidi, kwa upande wa Mheshimiwa Kessy, Mheshimiwa Mukasa, kwenye pia Kanuni ya 46(1) ambayo inataka mjibu maswali anapotoa majibu yake ayajibu kwa ukamilifu. Na hapa tumeelekezwa kwenye swali lililoulizwa, la nyongeza na Mheshimiwa Musukuma, ndiyo imeanzia hapo ninavyoona mtiririko.

Nikianza na la Mheshimiwa Mukasa ambalo yeye la kwake ni jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kuhusiana na suala la mafao, anayechelewesha ni nani?

Sasa mimi nadhani kwa sababu ni jibu ambalo lilitolewa, ni jibu katika jibu la msingi, jibu la nyongeza unahitaji upate uhakika kile kilichoulizwa na muulizaji wa swali la nyongeza na jibu ambalo limetolewa na Serikali kupitia Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kama limekidhi matakwa ya 46(1) au la!

Sasa unapokaa hapa huwezi kuyasikia maneno yote, lakini ninyi kwa sababu mnamsikiliza mhusika inawezekana mkayachua maneno yote, lakini *Hansard* ipo. Mimi nilikuwa nadhani kwa hili acha meza ikajiridhishe, ikapitie yaliyoulizwa kwanza na majibu yaliyotoka kama kweli anachosema Mheshimiwa Mukasa ni sahihi au majibu yalikuwa na upungufu.

Huo ndio Mwongozo wangu kwa Mheshimiwa Oscar Mukasa.

Kwa Mheshimiwa Ally Keissy, Mheshimiwa Ignas Malocha na Joseph Msukuma, mimi labda kwa sehemu fulani ninechangia, maana nilisema mbona mfanyakazi yeye mshahara wake hamuulizi anavyoutumia?

Sasa mtaniwia radhi kama nimewaelekeza muulize maswali ya nyongeza, hapana! Naamini na ninyi mmejituma wenyewe tu, lakini hoja hii ni nzito na ukiomba Mwongozo, nimewasomeeni, huwezi kuomba mjadala kwa namna hiyo, kama mnataka mjadala tumieni Kanuni vizuri. Lakini kwa hili mimi naamini,

Serikali imo humu. Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu wa Serikali hii ya Jamhuri ya Muungano yupo, lakini na wasaidizi wake, Mawaziri wapo hapa, ningeomba tu tutumie nafasi hii walitolee tu maelezo na baada ya hapo twende mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Jenista Mhagama!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba nikiri kwamba Waheshimiwa wabunge tumewasikia. Wamelizungumzia jambo hili na kuonesha dhamira ya dhati ya kutaka kupata maelezo ya kina kutoka Serikalini, tukitoa ufafanuzi wa hali hii ilivyo na yaliyojiri katika suala hili kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa ya Kiti chako Serikali tunaahidi kwa haraka kadiri iwezekanavyo, tutaleta maelezo ndani ya bunge hili Tukufu Waheshimiwa Wabunge wapate kuyasikia na kuyaelewa, na wewe pamoja na Kiti chako mtatuongoza nini zaidi cha kufanya. Lakini tutatekeleza hali hii ya maombi ya Waheshimiwa Wabunge ya kuleta maelezo haya ndani ya Bunge lako Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Ni wakati wa Mkutano huu au?

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mvua!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati wa Mkutano huu na ikiwezekana kabla ya wiki hii haijaisha tutatekeleza suala hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani ni *undertaking* nzuri tu ya Serikali. Tuipe Serikali muda ikatuletee majibu yaliyo sahihi kwa suala zito hilo.

Tumemaliza hayo tuliyonayo ya Mwongozo. Katibu!

**NDG. LINA KITOSI – KATIBU MEZANI:** Miswada ya Sheria ya Serikali. Muswada wa Sheria ya Upatikanaji wa Habari wa Mwaka 2016 *[The Access to Information Bill, 2016]*. Majadiliano Yanaendelea.

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Asante.

Waheshimiwa Wajumbe mjadala bado unaendelea wa Muswada huu, lakini lazima tuhitimishe leo. Naelewa jana jioni wengine walipata mawazo mazuri wameenda kujiorodhesha kuchangia, lakini muda mnauona na ninyi, tutajitahidi kadiri tunavyoweza.

Sasa nianze na wachache tulionao leo, lakini Mheshimiwa Zubeda Hassan Sakuru yeye namshukuru sana ametoa jina lake, hatachangia kwa leo, nakushukuru. Kwa hiyo, tunaanza na Mheshimiwa Joseph Roman Selasini atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Alexander Mahawe na Mheshimiwa Makame Mashaka Fumu ajiandae.

Mheshimiwa Selasini!

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie katika muswada huu. Lakini kabla sijatoa mchango wangu ningependa nitoe ushauri kwa Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nchi ni ya Watanzania na hili Bunge ni Bunge la Watanzania wote. Ningependa kuliomba Bunge lako tukufu, sisi Wabunge tumepewa kazi ya kuishauri na kuisimamia Serikali, tuwe wakweli na ukweli utatuweka huru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba, tunajadili muswada huu tukiwa na kumbukumbu za kufungiwa kwa baadhi ya magazeti na vyombo kadhaa vya habari kama *television* pamoja na redio. Ni ukweli pia, kwamba, tunaujadili muswada huu tukijua kabisa kwamba, wanasiasa karibu wote tumefungwa midomo kwa dhana ya hapa kazi tu, lakini kila mmoja wetu anajua kwamba, kazi ya wanasiasa ni kitu gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasiasa kazi yao ni kufanya mikutano na uhamasishaji. Kwa hiyo, kila mmoja wetu anaifahamu hii *contradiction,* kwamba, wakati tunahimiza kufanya kazi kuna kundi kubwa sana la Watanzania ambalo linazuiwa kufanya kazi. Sasa ni dhahiri kwamba, miongoni mwetu kuna uwoga wa kusema ukweli na wanasiasa wanazuiwa kufanya kazi yao kwa matakwa tu ya mtu fulani, lakini jambo hili ni jambo la Kisheria na jambo la Kikatiba. Ndio maana waliochangia jana waliishauri Serikali na walitushauri sisi Wabunge kwamba, sisi Wabunge tunao wajibu wa kufanya kazi zetu za Kibunge bila uwoga kwa sababu, sasahivi tumeingiwa hofu na uwoga,

Sheria zinakanyagwa, Katiba inakanyagwa, tunakaa kimya na hakuna anayesema! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Waziri wa Sheria alishambuliwa sana, shemeji yangu Mheshimiwa Harison Mwakyembe, hata na Mwanasheria Mkuu vilevile. Na hofu ilioneshwa kwamba, tunapitisha Sheria, tunatunga Sheria, lakini Sheria hazifuatwi, hofu hiyo kila mtu anayo katika moyo wake.

Mheshimiwa mwenyekiti, ninaomba kwa masikitiko makubwa niseme jambo hili, hivi tunavyojadili hii sheria sijui kama Serikali inajua kuna vijana wameshikiliwa pale *Central Police* kuanzia tarehe 24.Mmoja amepigwa mpaka amevunjwa miguu yote miwili, hawajapelekwa Mahakamani!; Tarehe 24 hadi leo! Sijui tunapojadili muswada huu kama Mwanasheria Mkuu na Waziri wa Sheria anajua kuna vijana zaidi ya 10 wanashikiliwa *Oytser Bay Police* hawajapelekwa Mahakamani hadi leo. Hivi sasa tutaacha kusema kwa sababu gani? Tutaacha kusema sisi Wabunge kwa sababu tunamuogopa nani wakati sisi tumeapa kuhakikisha kwamba, taifa hili linakwenda vizuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nashauri hii mijadala tunayofanya hapa Bungeni tuondoe hofu ya kujiangalia kisiasa, kwa sababu Taifa hili litaharibika, hili ni Taifa letu wote. Wenzetu wa nje mtu mmoja pekee akipata matatizo Taifa linatetereka. Sasa leo hii tuna vijana wameshikiliwa Kituo cha Polisi kinyume cha Sheria kwa zaidi ya wiki mbili, hakuna mtu anayesema, hakuna Mahakama inayoangalia. Hivi ni nani katika nchi hii yuko juu ya Sheria anayeweza kuwanyanyasa Watanzania kiasi hicho? Halafu Waziri wa Sheria unasimama unatuletea muswada mwingine tunapitisha sheria hazitekelezwi, tunapitisha sheria mwingine anazikanyaga! Inatia aibu na kichefuchefu cha hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilitoka nje wakati unajadili huu muswada nikakutana na Mbunge mmoja rafiki yangu sana akaniambia ninyi mnashambulia Serikali, mnasema Katiba imekanyagwa, sijui nini na nini! Katiba-Katiba nini? Rais ndiye Katiba. Khaa! Nikashangaa! Leo Rais ndiye Katiba? Nikashangaa kweli kweli! Nikamwambia wewe Mheshimiwa Mbunge! Kauli yako hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nimefikia hatua ya kusema wako Wabunge tukichangia sasa tutawataja kwa majina; kwa sababu humu ndani CCM wanakunja mikono, wakiwa nje ni kitu kingine tofauti wanachokisema! Kwa hiyo, mimi nashauri sana tunapotunga hizi sheria tuzijue, wengine si zetu, kwa sababu umri wetu wa kuzitekeleza unakwenda, lakini tujue tunawatungia hizi sheria watoto wetu na kizazi kinachokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo hebu tuiangalie Ibara ya 6 ya Sheria hii. Hivi unaposema taarifa iliyoombwa chini ya sheria hii itachukuliwa kuwa imezuiwa kutolewa ikiwa mamlaka ya umma ambayo inasimamia taarifa hiyo inadai kuizuia kwa taarifa yoyote, au sehemu yoyote ya taarifa, chini ya Kifungu kidogo. Mimi nauliza ni nani katika sheria hii au ni chombo gani katika sheria hii kimewekwa ku-*determine* kwamba, taarifa hii inakwenda kuingilia usalama wa Taifa, ni nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, kama mimi ni Mkurugenzi, taarifa inaombwa kutoka kwangu. Na mimi naona hii taarifa inakwenda kuharibu kazi yangu ni rahisi kama Polisi wanavyosema sasahivi, taarifa za kiintelijensia zinasema kwamba, msifanye hivi na hivi. Ndiyo maana tunasema Kifungu hiki chote ni kifungu ambacho ninyi Serikali mnataka kutumia kama kichaka kuficha mambo yenu. Hivi ni nani atakaye-*determine* kwamba, mkataba huu wa kibiashara unakwenda kuingilia maslahi ya nchi? Kama sio ni kichaka tu cha kuficha mikataba ovu ya kifisadi ambayo imeingiwa na Serikali, ambayo hatima yake ni kulihujumu taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamesema wenzangu jana. Uko ufisadi mkubwa kabisa katika nchi hii ambao umeibuliwa na taarifa za kichunguzi. Leo hii tunataka kuzia wale wanaotusaidia kupata taarifa kwasababu tu Serikali inataka kutengeneza kichaka cha kwenda kujibania ili taarifa ambazo wananchi wanapaswa kuzipata wasizipate. Nasema kwamba taarifa inaombwa ndani ya siku 30. Taarifa haiwezi kuwa na maana kama haikutolewa wakati muafaka. Kwahiyo, mimi naungana na wenzangu wanaosema kwamba ibara hii ya sita ni ibara ambayo itaua ule moyo wa wananchi kutoa taarifa na kuisaidia Serikali kupata taarifa mbalimbali ambazo zitasaidia katika mambo ambayo yanaweza kuibua uchunguzi wa mambo mbalimbali katika Taasisi za Umma na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo, mimi napendekeza kwamba kifungu hiki cha sita chote kiondolewe au kiandikwe upya kwasababu kina kila vipengele ambavyo ukiona kabisa kwa mantiki yake kinakwenda kuua uhuru wa vyombo vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tujue, haki ya kutoa taarifa na kupata taarifa ni haki ya kikatiba; ni haki ambayo wanayo wananchi wote. Leo tunapoweka sheria ya kuwabana wananchi kutoa taarifa maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba ile haki ambayo imetolewa kwenye katiba tunakwenda kuichukua, tunakwenda kuipoka. Kwahiyo, ni rai yangu kwamba muswada huu kwa maoni yangu ni muswada ambao kama kweli nia ni nzuri lazima tukae huu muswada uandikwe upya ili muswada huu uweze kuwa ni wa manufaa kwa taifa hili. Vinginevyo, mimi ninavyouona muswada huu ni muswada ambao unakwenda kuua uhuru wa vyombo vya habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, mimi nimesoma kwenye zile *definition* kwenye muswada huu. Moja kati ya jambo ambalo limekuwa *defined* ni kwamba mtu ni raia wa Jamhuri ya Muungano. Lakini sheria yenyewe inasema sheria hii itatumika Tanzania Bara; sasa mimi naungana na wenzangu wanaosema kwamba sasa hapa ule mgogoro ambao tumekuwa tukizungumza kila wakati; mgogoro wa muundo wa muungano hapa ndipo unapokalia. Tunazungumza sheria ya Tanzania Bara lakini Wazanzibar ndio wanatumika kututungia sheria sisi watu watu wa Bara; sheria ambayo wao hawataigusa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama hii sheria ni sheria ambayo tunafikiria kwamba ni nzuri, chukueni hii sheria muipeleke Baraza la Wawakilishi waijadili; ipitishwe kama sheria ya Jamhuri ya Muungano. Vinginevyo ni kitu cha ajabu tumekaa hapa Wazanzibar wanachangia sheria hii kwa nguvu zote na rafiki yangu namuona kule bado kidogo atapewa nafasi atujibu; atachangia kwa nguvu zote kuonesha kwamba hii sheria imepanda imeshuka, lakini haiwahusu, hii inatuhusu sisi. Ndiyo maana tunasema kwamba ile hoja ya muundo wa muungano hapa ndipo mmejikoki (mmejiweka) vizuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kusema kwamba naomba sana, sisi Wabunge ushabiki tunaoufanya kwa mambo ya msingi mbaya sana, hautatusaidia chochote. Jana liliulizwa swali hapa la kitaifa kabisa, ambalo lilikuwa linatafuta elimu kwa ajili ya watanzania wote lakini limejibiwa kwa ku-*personalize* yale majibu kulingana na muuliza swali; tunakwenda wapi? Na hata hii sheria sisi tunajua *finally* sheria hii itapita, itapita kwasababu ninyi mlio wengi mmeamua kwamba itapita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini huko mbele ya safari; jana kuna watu walikumbushwa hapa, walikumbushwa habari ya viongozi waliotoka huko wakaja huku. Nawakumbusha habari ya Chiluba; sheria alizounda baadae zikaja zikam-*cost* yeye mwenyewe. Tuangalie kwasababu hakuna mtu ambaye anajua kesho itakuwa namna gani. Tujadili tukijua kwamba tunajadili kwa manufaa ya nchi yetu, na hii nchi ni yetu wote, na sana sana sisi tuliopewa dhamana tumepewa dhamana hii kwa ajili ya watanzania wengi ambao hawakupata nafasi ya kufika humu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikushukuru na nikupongeze kwamba *finally* umekuja kutusaidia kukaa hapo kuongoza Bunge letu; tunajisikia vizuri sana, tunakupongeza sana. Asante sana! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya Asante, Mheshimiwa Esther Mahawe atafuatiwa na Mheshimiwa Makame Mashaka Fumu na Mheshimiwa Goodluck Asaph Mlinga ajiandae. Mheshimiwa Esther Mahawe hayupo! Tunaendelea; Mheshimiwa Makame Fumu! Tunaendelea Mheshimiwa Goodluck Mlinga! Mimi naendelea, ndio ratiba; Mheshimiwa Katani Ahmad Katani.

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru lakini pia napenda nichangie muswada kama:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma muswada huu kifungu cha 5(3) utagundua kuna mapungufu makubwa ambayo tunapaswa kuyarekebisha kama Bunge na Napata shida kidogo kwasababu Waziri wa Sheria ni mtu ninaye muamini. Na ukisoma kifungu kile kimeeleza wazi, kimetoa tafsiri ya mtu; mtu anasema ni raia yeyote wa Jamhuri ya Muuungano wa Tanzania. Lakini muswada huu tunaochangia unahusu Tanganyika. Sasa labda wakati tunataka kuchangia na kuendelea na muswada huu labda utoe tafsiri sasa kwamba mtu ni raia yeyote wa Jamhuri ya Tanganyika kama tulivyotaka Serikali tatu; inaweza ikawa tafsiri sahihi kabisa, maana inaleta shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulizungumza Serikali tatu watu mkazikataa; leo tunazungumza suala la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunazungumzia na watu wa Zanzibar, na mmetoa tafsiri hiyo hiyo ya mtu; lakini kwenye muswada huu mnasema itumike Tanganyika tu; hili ni jambo ambalo nadhani Waziri kwasababu ni mtaalam sana wa sheria uone ikiwezekana kwa safari hii huu muswada tusiendee nao kwasababu una mapungufu makubwa ili muulete wakati mwingine tuujadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukienda kifungu cha sita nacho utaangalia; kuna mapungufu makubwa yanaendelea pale. Mmetoa mamlaka ya baadhi ya vyombo vya kiuchunguzi, wakati wanaendelea kuchunguza mambo yao; hamjatoa *duration* kwamba muda gani muda gani watachunguza. Kwa maana kuna uwezekano mkubwa ikachukua miaka hata mitano, kumi, kumi na tano kwasababu hakuna muda mle ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikuombe Mheshimiwa Waziri wakati mnaangalia hili jambo msije mkawa mna tengeneza jambo kwa ajili ya uchaguzi wa 2019/2020. Maana nahisi kabisa mnatengeneza kitu cha 2019/2020 ili kubana uhuru wa watu kutoa taarifa zao vizuri kwa maelezo tu kwamba mnaweza mkasimama na vifungu hivi vidogo vya kusema kuna uchunguzi, kuna hili; watu wakakosa fursa ya kupata haki zao za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo, niombe kama kuna marekebisho ya kifungu kile cha 5(3) mfanye marekebisho hayo, lakini kifungu kile cha sita ikiwezekana chote tukiondoe ili tuweze kwenda sawa kwa ajili ya haki ya watanzania hawa. Asante sana! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana, tunaendelea Mheshimiwa Devotha Mathew Minja.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Na mimi nichukue fursa hii kuchangia muswada uliopo mbele yetu. Katika Bunge lililopita Mheshimiwa Waziri alikuja na mikakati yake akisema atakuja na muswada hapa ambao utakuwa ni mwarobaini; muswada wa habari. lakini matokeo yake sasa imekuwa ni muswada wa taarifa, sijui imekuwaje ghafla ukabadilisha gia hewani. Lakini tunachosema tu ni kwamba huu ni mkakati si muswada kama vile tunavyoufikiria; huu ni mkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kwa muswada huu, kwa hali halisi na mambo yanavyoendelea hivi sasa ni kwamba unakwenda kupewa rungu. Tumeshuhudia mengi ikiwemo wewe mwenyewe binafsi kuvifungia vyombo vingi vya habari. Na muswada huu unakwenda kufunga midomo; muswada huu unakwenda kukupa mamlaka ya kufanya utakavyoweza kufanya kwasababu kuna baadhi ya vipengele ambavyo vinaonesha kwamba endapo mtu hataweza kupewa taarifa, Waziri ndiye msemaji mkuu na ndiye mwenye mamlaka ya mwisho. Muswada huu unakwenda kukupa wewe mamlaka hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, endapo mtu atakosa taarifa sahihi atakwenda kukumbana na Waziri ambaye ndiye mwenye maamuzi ya mwisho. Na kwa mamlaka hayo sasa haitoi fursa kwasababu Waziri anasimami Wizara. Inawezekana kabisa taarifa zinavyotafutwa zipo chini ya Wizara, sasa itakuwaje Waziri aweze kutetea hili? Tunaomba, kwa mujibu wa sheria kwasababu mahakama ndio yenye kuingilia kati, yenye mamlaka; suala hili lingekwenda huko badala ya kumuachia Waziri kuwa ndio msemaji mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikianza kifungu kile cha 19 ambacho kinamtaka Waziri kuwa wa mwisho katika…

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ibara ya 107A ambayo inaitaka Mahakama kuwa ndicho chombo pekee cha kutoa haki inayogombaniwa na si Waziri sasa. Endapo Waziri atapewa mamlaka haya, endapo mtu atakuwa amenyimwa taarifa mahali fulani pa kwenda kulalamikia isiwe ni Waziri; itoe fursa kwamba mtu aweze kwenda mahakamani na mahakama itoe haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 4 kina mgongano juu ya ni nani anapaswa kupewa taarifa. Kifungu hiki kinasema kwamba mpewa taarifa awe ni raia na si mtu. Tafsiri yake ni nini hapa? Wakati Mheshimiwa Waziri anaeleza alisema kwamba mlijaribu ku-*relay* nchi nyingine kwa mfano South Africa, Malaysia, Uingereza na kwingineko ambapo mnasema kwamba mtu yeyote anapaswa kupewa taarifa. Kwa hizo nchi za wenzetu kwa maana ya Uingereza,

Malaysia na South Africa sheria zao zinasema hivyo. Lakini hapa mmekuja na hoja kwamba mtu anayepaswa kupewa taarifa ni raia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama ni raia sisi wenyewe tunaji-*contradict* kwasababu gani? Yapo matukio kadhaa, kwa mfano *issue* ya *RADAR,* wakati huo sisi Tanzania tuliomba *information* kutoka Uingereza, na imetusaidia kupata taarifa kwa wenzetu; zikatuwezesha kupata *change* ya dola milioni 12. Sasa kama sisi tutasema mtu anaetaka kupata taarifa ni lazima awe raia kwa maana hiyo tunajifunga. Kama kuna watanzania ambao ni wawekezaji wapo hapa na wakafanya madudu; wakahitaji kupata taarifa hapa hatuwezi kuwapa taarifa kwasababu sheria hii itakuwa inawabana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahivyo, tunacho sema ni kwamba kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ibara ya 18(d) kwamba:-

*"Kila mtu ana haki ya kupata taarifa."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sisi tunasema kila raia kwa mujibu wa muswada huu. Kwahivyo, kuweka neno raia ni kwamba ni kichaka ambacho tunakwenda kujificha. Tumeona *issue* mbalimbali mfano sakata la *ESCROW* tuliweza kupata taarifa kwa wenzetu kutoka Malaysia kwasababu gani? Wao Katiba yao inasema kupata taarifa ni mtu yeyote na si raia. Sasa tutakapokuja na kipengele kwamba tunasema kwamba ni raia sasa tutakuwa tunajifunga kwamba baadhi ya taarifa hatuwezi kuzipata lakini pia hii ni kuleta ubaguzi; hamuwezi mkaja na muswada huu mnatuambia nchi zingine zimefanikiwa kwa mfano Malaysia na *South* Africa ambazo sheria yao ni tofauti na hii; haizungumzii raia inasema mtu kupata taarifa ni haki ya kila mtu. Hata Katiba yetu inasema hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kifungu cha kwanza kinasema sheria ianze kutumika mara tu Waziri anapoitangaza. iko miswada mingi ambayo imepita, zipo sheria nyingi ambazo zimepitishwa na Bunge hili lakini bado hazijaanza kufanyiwa kazi. Lakini kwenye hili kwasababu ni mkakati ikishapitishwa tu tayari ianze kufanya kazi; lakini kwanini isingepewa muda kanuni zikatengenezwa? Sisi tunasema ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge lazima tuungane katika hili kwasababu muswada huu unakwenda kunyamzisha vyombo vya habari; ni lazima tufikirie upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii vyombo vya habari vinafungiwa, mtu akiamka tu asubuhi anavyoamua anafungia vyombo vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Tanzania kwa *level* tuliyofikia sasa maendeleo tuliyo nayo tunajivunia ni vyombo vya habari. Ni nani ambae sasa

hivi atakubali kuwekeza kwenye vyombo vya habari kama tunakwenda kuwa na sheria ya namna hii? *Radio* moja ikifungiwa ina waajiriwa *permanent* labda 20, hujaweka wale ambao wanakwenda kujifunza, hujaweka watu wale ambao wanakuwa wanafanya mawasiliano ya moja kwa moja; kwa maana kuchangia hoja, hujaangalia familia za hao watu. Tunaathiri zaidi ya watu 100 kufungia redio moja; wafanyakazi tu peke yake achana na Watanzania. Sasa leo hii tunakuja na sheria hii ambayo mtu akifanya kosa tu dogo lazima afungiwe. Kwahiyo, tunasema, kwa wakati tulionao na hali tulizonazo tunaona huu ni mkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lakini vilevile kifungu cha sita tunapendekeza kiondolewe kabisa, kwanini? Mnasema kwamba mtu ambaye ata-*distort information* yoyote anapaswa kuhukumiwa kama zilivyo Sheria za Usalama wa Taifa. Ni kwanini tujifiche nyuma ya hizi sheria za usalama wa taifa wakati tunayo sheria ambayo inazuia hali hiyo ya mtu kama akisema uongo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunasema kwamba mtu atafungwa kifungo cha miaka 15 mpaka 20. Kwanini mtu kama ametoa *information* tu akakutane na kifungu kikubwa namna hii? na hakuna sehemu ambayo inazungumzia kwamba endapo hakuna *fine*, moja kwa moja kwamba mtu ni lazima akakumbane na kifungo cha ndani kwa maana miaka 15 mpaka 20; kwanini hakuna *fine* katika hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo mengine kwa mfano *informers* wanakupa habari nzuri ambazo zinaweza zikasaidia na zikajenga lakini kama siye msemaji atakumbana na kifungo hiki. Sisi tunasema kifungu hiki kiondolewe kwasababu kitakwenda kutunyima kupata taarifa; *so long* mtu ambaye ana *information* ambazo ni *reliable* zinaweza zikasaidia nchi, zikasaidia taifa; kwa mfano *issues* za njaa na mafuriko; tukasubiri afisa ambaye ameteuliwa na Serikali aende akatoe taarifa hizi. Hii ni kwenda kunyima vyombo vya habari kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano kwenye uchaguzi, tutakwenda kwenye uchaguzi mwaka 2020, kwa maana hiyo taarifa za awali za uchaguzi mwandishi hataruhusiwa kuzitoa ni mpaka asubiri Afisa Habari wa Wilaya? Tunachosema kwamba kuna mambo ya msingi ambayo kwa hofu tu ya kukumbana na hili ni lazima tuyaangalie, na tunapendekeza kabisa kifungu hiki cha sita kiondolewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mmezungumzia kuhusu utoaji wa taarifa kwa maana ya mtu atakapoomba taarifa apewe siku 30, hivi hiyo itakuwa ni taarifa au itakuwa ni kitu gani, kwa sababu uende uombe taarifa kwenye taasisi, ukae siku 30 usubirie kupata jibu kwamba hiyo taarifa ipo au haipo, ni kwa nini msingeweka siku tatu au siku moja kama ilivyo TAMISEMI. Siku 30 halafu

unajibiwa kwamba taarifa unayoihitaji haipo. Tunachotaka kumuambia Mheshimiwa Waziri, Muswada huu utakwenda kunyamazisha vyombo vya habari, utakwenda kuumiza wamiliki wa vyombo vya habari, utakwenda kuvunja morali kwa watu ambao wana *interest* ya kuwekeza kwenye tasnia ya habari, tunaomba kama kuna uwezekano wowote Muswada huu uondolewe tusubiri tupate maoni upya. Wadau mbalimbali wa habari walishiriki lakini maoni yao hayamo humu, hayakuzingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunasema, mtaupitisha kwa sababu ya wingi, lakini tunachosema kwamba tutafika kwenye hali ambayo, kama wenzetu Uganda ilivyo Rais anaamka asubuhi anafunga magazeti, anafunga redio. Sasa kwa sasa hivi *graph* ya vyombo vya habari ambapo kwa Afrika, Uganda ilikuwa inashika nafasi kama ya sita, sasa hivi inakaribia kuwa mwishoni kwa sababu ya vyombo vya habari kufungwa midomo na Serikali. Tunaomba ili Muswada huu uwe na maana, ni lazima Serikali ikubali kwamba kuna baadhi ya vitu ambavyo ni lazima vifanyiwe marekebisho makubwa, vinginevyo uwekwe pembeni tusubiri mpaka muda utakapofikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Tanzania ya leo hii, kwa teknolojia ilivyokua sasa hivi, mtu akipata taarifa mtu ataogopa, watu wataingiwa woga, tutakosa taarifa muhimu. Mbona tunashuhudia kwenye baadhi ya vyombo ambavyo vinakuwa *biased,* matukio makubwa wanaacha kwa sababu ya woga. Kwa hiyo, tunakwenda kutengeneza sheria ambayo itaendelea kudidimiza vyombo vya habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokiomba ni kwamba Serikali iko haja ya kuangalia upya jambo hili. Yapo mambo mengi ambayo tungeweza tukayafanyia kazi kwanza kabla ya kuja na muswada huu, zipo haki nyingi za watu za kupata taarifa, mngeangalia badala ya kujificha…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea, anayefuata ni Mheshimiwa Amina Mollel na Mheshimiwa Goodluck Mlinga ajiandae.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uzima na kutukutanisha tena hapa na vilevile ninakushukuru wewe kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika Muswada huu wa Haki ya Kupata Taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kumueleza tu kwanza Mbunge wa Tandahimba kwamba wakati wa kuchangia alisema nchi ya Tanganyika, hakuna nchi ya Tanganyika, naomba kwenye *Hansard* hili waweze kulibadilisha hakuna nchi ya Tanganyika, pia nimfahamishe kwamba kama jinsi

ambayo imeelezwa Muswada huu unahusu Tanzania Bara, hili siyo suala la Muungano, kwa maana hiyo Zanzibar inayo Wizara ya Habari inayojitegemea kule na masuala yao yatabaki kule Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo naomba nijikite kwa kuanza kueleza nikianzia na harakati za kupata Muswada huu. Itakumbukwa kwamba Muswada huu ulianza miaka kumi iliyopita (mwaka 2006) wakati huo lilipoanza vuguvugu la haki ya kupata taarifa. Kwa wakati huo ulipotolewa kwa mara ya kwanza katika tovuti ya Wizara ya Habari mwaka 2006, Muswada huu ulipingwa na wadau mbalimbali, hata wadau walipokutana na Wizara walizungumza na kutoa mapendekezo yao na wakakubaliana kwamba Muswada ule kwa wakati ule urudishwe ili uweze kufanyiwa maboresho. Serikali ilisikiliza baadhi ya maboresho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena Muswada huu ululetwa mwaka 2015 kwa hati ya dharura na ulikuwa pia na baadhi ya mapungufu, ulirudishwa Muswada huo na wadau walipewa nafasi ya kuweza kuupitia ili kuuboresha kwa kutoa mapendekezo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya mapendekezo ambayo tayari yapo katika Muswada huu mojawapo ilikuwa ni kuweka utaratibu wa kumwezesha mtu kuomba na kupata taarifa, jambo ambalo Serikali kwa hivi sasa imelizingatia. Vilevile kulikuwepo na sharti kwa taasisi za umma na watu binafsi, kuwa na Maafisa Habari ambao watakuwa na wajibu wa kuwapa watu taarifa wanazozihitaji, jambo ambalo katika Muswada huu imezingatiwa.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mollel, hebu kaa kidogo tusikie taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Dada yangu, Mheshimiwa Amina najua wewe ni mwandishi wa habari, lakini huu Muswada ambao unaujadili ni Muswada wa Habari tofauti na huu Muswada ulioletwa hapa, naomba kumpa taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mollel, unasemaje kuhusiana na hiyo taarifa?

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sipokei taarifa yake, naomba ulinde muda wangu na ninaendelea.

Katika maeneo ya baadhi ya vifungu mbalimbali vya Muswada ambao uliwasilishwa mwaka jana, Muswada huu kwa mara ya kwanza baadhi ya maoni ya wadau wa habari yamezingatiwa na maoni yao ninayo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya maoni hayo, kwa mfano, Muswada uliopita mwaka jana kulikuwa kuna kipengele ambacho kiliupa upendeleo Shirika la Utangazaji la Taifa *(TBC)* ambao ulivitaka vyombo vya habari vyote viweze kupewa taarifa katika chombo kile. Jambo hili lilipingwa na kwa hivi sasa limeondolewa na hii ni kwa mujibu wa maoni na mapendekezo ya wadau mbalimbali wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 18 ambacho kilielekeza kuwa taarifa iliyotolewa kwa mtu aliyeomba kutoka kwa mwenye taarifa haitatolewa kwa umma kimeondolewa vilevile, na kifungu hicho kilikuwa kimeua kabisa nia na madhumuni ya sheria lakini katika Muswada huu wa mwaka 2016 kifungu hiki kinaruhusu matumizi ya taarifa kutumika vilevile kutaka habari hizi zisipotoshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kingine ambacho kimeboreshwa na kipo katika Muswada huu wa Haki ya Kupata Taarifa ni kifungu ambacho umefanya mabadiliko mawili makubwa katika rufaa. Mfano, awali rufaa ya mwanzo kutokana na kunyimwa kupewa taarifa ilikuwa imepelekwa kwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, kwa sasa rufaa ya kwanza ya kunyimwa taarifa itaenda kwa Mkuu wa taasisi husika ambapo taarifa iliombwa na ngazi ya pili ya rufaa vilevile itakwenda kwa Waziri, hata hivyo bado kuna maboresho ambayo kwa namna moja au nyingine yanahitaji kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 10 kinaelekeza jinsi gani waombaji taarifa wanaweza kufanya hivyo kwa kutumia maandishi au kupitia njia za kielektroniki za mawasiliano kama barua pepe, vilevile kina maelekezo ya kusaidia waombaji taarifa ambao hawajui kusoma au kuandika na wenye ulemavu kuomba taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipengele hiki kimeboreshwa kwa maana kwamba na ninaiomba pia hapa Wizara husika kuangalia ni kwa jinsi gani makundi maalum yataweza kupewa taarifa. Mfano, kama watu wenye ulemavu wa kutosikia (viziwi) wahakikishe kwamba watu hawa wanapewa vipi taarifa na zinawafikia kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niende katika kipengele cha sita ambacho kinapigiwa sana kelele. Ni kweli, na ni ukweli ulio dhahiri kwamba kuna baadhi ya vipengele ambavyo vinahitaji kufanyiwa marekebisho, lakini Muswada kwa kiasi kikubwa umezingatia maoni na ushauri wa wadau wa habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kipengele cha sita na hapa nijikite zaidi katika kipengele ambacho kinazungumzia taarifa, mfano katika majeshi, taarifa za kiusalama, ni ukweli ulio wazi kwamba kwa mfano, ukiangalia kwamba katika mambo ya usalama, baadhi ya taarifa ambazo zimeshawahi kutolewa, mfano unapotoa taarifa kwamba kifaru cha Jeshi kimeibiwa, hizi taarifa, kwa sababu hata katika taaluma tunaambiwa kwamba kuna taarifa ambazo lazima uangalie *national interest,* kwa maana kwamba unapotoa taarifa hizi unawaambia nini maadui wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kipengele hiki kiendelee kubaki kwa ajili ya maslahi ya Taifa, kipengele ambacho kinazungumzia majeshi, kipengele ambacho kwa mfano ilizungumziwa kwamba rada ni mbovu, hivi, je, hauoni kwamba taarifa zako unazitoa kwa maadui ambao kwa namna moja au nyingine wanaweza kuvamia na kuweza kutumia nafasi hiyo! Kwa hiyo, kipengele hiki kinastahili kubaki hivyo kwa sababu ya *interest* ya Taifa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ni kweli kama ambavyo na wengine pia wamesema, kwamba kuna baadhi ya vipengele ambavyo vinahitaji kurekebishwa kwa mfano, haki hii ya kupata taarifa unaposema kwamba kwa raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hivi sasa tunaelekea katika nchi ya viwanda, kwa maana hiyo wapo wengine ambao ni wawekezaji na wanapokuja hapa kuna taarifa nyingine ambazo ni muhimu wanahitaji kuzipata, unapoweka muda mrefu wa siku 30 kwa maana hiyo kama ni taarifa ambazo ni muhimu utakuwa umembana huyo mtu asiweze kupata hizo taarifa. Kwa hiyo, siku 30 ni nyingi sana na ziangaliwe ni kwa namna gani basi wanaweza kupunguza hizo siku ili taarifa zipatikane kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kipengele kingine ambacho kinahitaji maboresho ni kipengele kwa mfano, kipengele kinachozungumzia upendeleo ambacho nilikizungumzia kuangalia kwamba ni namna gani mfano mtu anapokwenda kutafuta taarifa na zile taarifa akazikosa na vilevile anapotaka kukata rufaa kwamba Waziri ndiyo mwenye dhamana ya mwisho, napendekeza kwamba kiweze kuboreshwa kuangalia kwamba ni kwa namna gani kuwe na tume au mamlaka nyingine ambayo inaweza zikapelekwa zile taarifa na mtu ambaye anatafuta taarifa aweze kupata hizo taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikiri kusema kweli kwa mara ya kwanza kabisa Muswada huu umezingatia maoni mengi ambayo yana manufaa kwa Taifa hili na hata maoni ya wadau wa habari wameyatoa humu na wameelezea na kuridhishwa kwao ni kwa jinsi gani kwa mara ya kwanza Serikali imeweza kuzingatia hayo maoni yao. Kwa maana hiyo, ninaamini kabisa Muswada huu utakapopitishwa utaweza kwenda kufanya kazi lakini pia katika nchi yoyote ina utaratibu wake na katika hizi nchi mfano duniani kote mataifa makubwa na madogo yanaweka zuio kwenye taarifa zake ili kulinda maslahi

yake. Kwa maana hiyo wale watu ambao kwa namna moja au nyingine wamekuwa wakipata taarifa na kuzitumia hizo taarifa pasipo kuzingatia; mfano hata katika taarifa wanaposema kwamba habari ni nini, lazima uzingatie vitu vitano, kwamba hiyo habari ni nani, imetoka wapi, ni nani ametoa hiyo habari tofauti na wengine ndiyo utatumia kwamba ni habari za uchunguzi lakini hizo habari za uchunguzi wakati mwingine ukiangalia ni nani katoa bado jibu inakuwa huwezi kupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile itawazuia hata wale watendaji wa Serikali ambao kwa namna moja au nyingine wanaiba taarifa za siri na kuzitoa kwa nia isiyo njema. Muswada huu utakwenda kuwabana kwa maana kwamba itawataka pia hata hawa wanahabari kuhakikisha kwamba wanapata habari katika vyombo vinavyohusika kuwatoa habari ambayo ni mahsusi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo tunapozungumzia hapa ni vyema basi wakati mwingine watu tukajikita katika kuangalia kweli, wanasema kwamba mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni, yapo mambo ambayo Serikali ina nia njema kabisa na wadau wa habari pia wametoa maoni na yameweza kuzingatiwa, afadhali wakati mwingine, ndiyo, mnapozungumza tuangalie kwamba kweli tuishauri Serikali ni vipi ambapo hapa wamekosea tuboreshe hivi badala ya kuwa ndiyo namba moja katika kulalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Goodluck Mlinga, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph George Kakunda.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi leo naomba nianze nyumbani kidogo kwa sababu Muswada wenyewe unahusiana na taarifa. Rais wangu ni msema ukweli, na msema ukweli ili awe mpenzi wa Mungu inabidi akubali kuambiwa ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya uchumi sasa hivi ni ngumu sana huko mtaani. Mimi kama Mbunge kijana ninayewawakilisha vijana na vijana ndiyo wanaoongoza kwa kutokuwa na ajira, kweli kuna hali tete, kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Rais hapo alipopashika sipo, abadilishe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la pili ni kwa ajili ya wafanyakazi. Wafanyakazi ndiyo wanaosaidia kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, leo hii wanaishi katika maisha ya *tension,* wengi wanakwenda ofisini hawajui kama watarudi salama, kuanzia Makatibu Wakuu hadi Watendaji wa Mtaa, kweli

wanaishi maisha magumu. Wote mtakuwa mashahidi juzi kuna Mkuu wa Wilaya mmoja alitaka ku-*demote* walimu wakuu zaidi ya 500, kweli hatuwatendei wafanyakazi wetu haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudi Bungeni sasa. Kwanza naomba niendelee kumtakia afya njema Spika wetu wa Bunge, mimi ni mmojawapo kati ya watu ambao walikuwa wanamuombea kwa dua zote ili arudi salama tuendelee kulisukuma gurudumu hili. Kwa upande mwingine siyo kama wenzangu wa upande wa pili ambao walisema wamem-*miss* Spika, maadili ya Katiba ya nchi yangu na jinsi nilivyolelewa hairuhusiwi mwanaume kumwambia mwanaume mwenzako nimeku-*miss*.

Naomba niwashukuru wapinzani kwa kurudi Bungeni kwa sababu kitendo cha kuingia na kutoka kilikuwa kinaambatana na matukio mengi, pamoja na wizi, uporaji na unyang'anyi pamoja na ujambazi, kwa hiyo, kitendo hicho naamini sasa hivi hakitakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Muswada. Imeshajengeka tabia kila kitu kizuri sasa hivi kinachofanyika ni kwa ajili ya kuwabana wapinzani, Muswada mzuri umeletwa, Wabunge inatakiwa tuchangie, tuishauri Serikali lakini tumekuwa wakosoaji. Sasa leo muswada mzuri umeletwa mnasema uko kwa ajili yenu ninyi. Jamani, hivi CHADEMA kweli mko wengi kuliko CCM mna maslahi mapana kwa wananchi wa Tanzania kuliko CCM! Ninawaomba Watanzania, niwataarifu kuwa hakuna wasaliti kama Wabunge wa UKAWA, hawa watu ni wasaliti kuliko yule aliyemsaliti Yesu Kristo wa Nazareth.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila kitu kimekuwa cha kupinga. *NHC* sasa hivi wanafanyakazi, wanasema wanafuatwa wao. Polisi wakifanya mazoezi wanasema wanafanya mazoezi kwa ajili yao, jamani kitu gani ambacho tutakifanya kiwe kizuri kwenu ninyi?

Mheshimiwa Rais amesema siasa mpaka mwaka 2020, ninyi mnasema amewazuia ninyi. Jamani Chama cha Mapinduzi kina uongozi kuanzia Mwenyekiti hadi Mtaani tuko, wengi kama hiyo siasa CCM ndiyo tunaihitaji zaidi kuliko ninyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamefika kipindi mpaka wanamkufuru Mungu, wanasema kupatwa kwa jua kumetokea kwa ajili yao ili kuwe na giza wasiweze kufanya maandamano.

Mimi naomba niwaambie, haya mambo ya kuambiwa kila kitu anachosema Mwenyekiti mkikubali mtakuja kuamuliwa hadi mambo yenu ya nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu ni mzuri na ninachoomba Serikali isibadilishe hata nukta, hivi ulivyo ndiyo usainiwe kwa ajili ya kuwa sheria. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge naomba utulivu na tunaendelea. Tunakushukuru kwa mchango wako kwa kadri ulivyoweza. Mheshimiwa Joseph George Kakunda atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu Bungeni na ninaamini Bunge lako Tukufu litaupitisha Muswada huu baada ya marekebisho machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya marekebisho ya mwisho ninaomba wataalamu wake warejee kupitia Taarifa ya Helena ya mwaka 1997/1998 ambayo ndiyo ilikuwa msingi wa *Local Government Reform Programme*. Vilevile warejee taarifa maarufu inaitwa *ROSC* au *Report on Standard and Codes* ambayo ilitolewa na Shirika la Fedha Duniani *(IMF)* mwaka 1999 ambayo imekuwa msingi wa mabadiliko makubwa sana kifedha katika nchi yetu.

Vilevile warejee taarifa ya Benki ya Maendeleo ya Dunia *(World Development Report)* ya mwaka 2004 kuhusu kupeleka rasilimali kwa wananchi maskini. Taarifa hizo tatu zitawasaidia sana kuboresha baadhi ya vifungu kwenye huu Muswada, kama ambavyo na mimi nitavipitia vichache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa muhimu sana ni zile zinazohusu maendeleo ya wananchi. Taarifa ya *ROSC* ilifanyiwa kazi na Serikali vizuri sana kuanzia mwaka 2001 mpaka mwaka 2007. Wizara ya Fedha kila ilipokuwa inatoa fedha kupeleka kwenye Halmashauri, ilikuwa inatoa matangazo katika magazeti kuonesha kila Halmashauri imepata kiasi gani kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za hivi karibuni utoaji wa taarifa kama huo umeminywa, umekuwa hauonekani kwenye vyombo vya habari kiasi hata Wabunge wamekuwa wanapata shida kufuatilia kupata taarifa ni fedha kiasi gani zimekwenda kwenye Halmashauri. Maelekezo yaliyokuwepo wakati ule, fedha zikifika kwenye Halmashauri taarifa ile inabandikwa kwenye mbao za matangazo za Halmashauri na zinabandikwa kwenye maeneo yenye watu wengi kama sokoni zinabandikwa. Tumepata fedha kwa ajili ya mradi huu kiasi kadhaa, inaonesha *transparency* ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri yenyewe inapopanga matumizi ya fedha zile kwenda kwenye kata na vijiji, vijiji na Kata nazo zinabandika taarifa zile kwenye shule za msingi na kwenye maeneo ambayo watu wanapita. Hiyo inaonesha uboreshaji wa hali ya juu wa upatikanaji wa taarifa za maendeleo kwa wananchi ili waweze kufuatilia maendeleo yao mahali ambapo wanaishi.

Kwa hiyo, ninaomba sana vipengele vitafutwe kwa sababu sheria hii imechelewa sana. Kwa maoni yangu ilitakiwa itoke mwaka 2001, sasa kwa sababu tuko mwaka 2016 ndiyo inatoka sheria hii basi naomba vipengele vile vya kutoa taarifa kwa wananchi viwekwe mahususi ili kusudi kuwalazimisha Mamlaka za Serikali Kuu na Serikali za Mitaa kutoa taarifa za maendeleo kama hizo kwa wananchi bila kizuizi chochote ili kuongeza *transparent*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nizungumzie kuhusu sheria hii. Sheria hii haijagusa zile taarifa ambazo hasa hasa zinahusu moja kwa moja wananchi. Kwa mfano, taarifa za masoko, taarifa za wanunuzi wa mazao, taarifa za bei za mazao kabla mkulima hajaamua kuwekeza katika kilimo anatakiwa apate hizo taarifa, vipengele hivi ninaomba sana viwekwe. Vifungu vyote vilivyomo humu ni vya jumla tu vinahusu hasa Serikali Kuu lakini kule kwenye Serikali za Mitaa na hasa mambo yanayousu maendeleo ya wananchi bado hatujavigusa sana kwenye vifungu karibu vyote vya Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ambalo napenda kulizungumzia ni suala la kutunza taarifa kwa kipindi miaka 30. Katika baadhi ya taarifa, inawezekana muda huo ukawa hautoshi katika baadhi ya taarifa na katika baadhi ya taarifa unaweza ukawa unatosha. Nitatoa mfano, Afrika Kusini kwa kutumia sheria yao wametunza mahojiano ya kimahakama ambayo Mheshimiwa Nelson Mandela alishtakiwa na Serikali ya makaburu miaka ya 1960. Wameyatunza yale mahojiano kwenye vyombo ambavyo Mwafrika Kusini yeyote anayetaka kusikiliza mahojiano yale anaruhusiwa kwenda kusikiliza mahojiano yale na akajifunza na ikajenga uzalendo wa nchi ya Afrika Kusini.

Kwa hiyo, hata sisi kwa mfano kesi maarufu ambayo Mwalimu Nyerere alishtakiwa na wakoloni na akalipishwa faini, Mtanzania kwa sasa hivi akitaka taarifa hiyo aisikilize kwa kusikia kwa maneno maana yake najua ilirekodiwa wakati ule kwenye *tape* za wakati ule. Sasa imetunzwa wapi taarifa hii? Mtu au kikundi cha watu kikitaka kuisikiliza hiyo kesi kitaipata wapi? Ni tatizo! Najua kule Jeshini taarifa hizo zipo lakini inatakiwa iwekwe kwenye utaratibu huu.

Kwa hiyo, kumbukumbu kama hiyo kutunzwa kwa miaka 30 inaweza ikawa haitoshi, inawezekana tukaihitaji hata kwa miaka 100 ili iwepo vizazi na vizazi viweze kuitambua, kwa hiyo hiki kipengele cha miaka 30 ni lazima kuzingatia *classification* ya taarifa. Inawezekana taarifa zingine zikahitaji kipindi kirefu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kusoma kwangu Muswada, sijakuta sehemu inaonesha uhusiano wa Muswada huu na kazi za Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Serikali pale Idara Kuu ya Utumishi. Ni vyema ikaainishwa wazi pamoja na kwamba tunataja kwa ujumla, lakini kwenye sheria ile iliyoweka utaratibu wa kazi za Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Serikali pale Idara Kuu ya Utumishi, ni vema kuainisha vizuri majukumu ili kusudi najua kwenye kifungu cha sita utaratibu umewekwa vizuri kuhusu taarifa ambazo ni *classified,* lakini ni vizuri kuweka utaratibu mzuri wa kimahusiano ili isije ikatokea mgongano kati ya idara moja na idara nyingine ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele kingine ambacho ninapenda kuzungumza, tumekuwa na *clients service charter* karibu katika kila idara ya Serikali ambazo hizo ilikuwa ni *attempt* ya Serikali kuji-*commit* kwa wananchi kama wateja namna ambavyo watawahudumia. Wakati ule inaanzishwa hii mikataba ya huduma kwa mteja kwenye kila idara ya Serikali na katika kila Halmashauri, wakati ule ilikuwa ni wazo tu la Utumishi kuhusu *transparency*. Namkumbuka Mheshimiwa Mary Nagu alikuwa anaongoza sana harakati hizo. Sasa kwa sababu sheria hii ndiyo inakuja, ninaomba kiwepo kipengele kinacholazimisha hii mikataba ya huduma kwa mteja ipitiwe upya ili kusudi kifungu hicho kiwalazimishe kila idara kuwahudumia vizuri wateja wao na hasa wananchi. Hayo ndiyo mambo ya msingi zaidi ambayo nimeona mimi yamesahaulika kwenye muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mawili ya mwisho ninayotaka nizungumzie ni kifungu cha 10. Kifungu cha 10 kinalazimisha kwamba taarifa lazima iombwe kwa maandishi; kidogo hapo tutakuwa tunaondoa uhuru wa muombaji wa taarifa.

Ninaomba taarifa inaweza ikaombwa kwa maandishi au ikaombwa kwa mdomo. Ninaposema haya najua kwamba kwenye kifungu cha 10(4) kuna maelezo yamewekwa pale kwamba kama mtu hajui kusoma na kuandika anaweza akaomba kwa mdomo halafu yule mwenye taarifa ndiyo akaweka maombi yale kwa maandishi halafu yule akaweka dole gumba. Lakini hiyo ni kulazimisha tu maandishi yawepo. Ninachosisitiza mimi ni kwamba tuweke uhuru kwa mwananchi, anaweza akaomba taarifa kwa maandishi au kwa mdomo. Hiyo kidogo itapunguza na kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wananchi na hiyo itaongeza *transparency* ambayo kila mtu angependa aione *transparency* ina-*prevail*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine kwenye kifungu cha 11(1) hadi (3), vinaweka msisitizo wa siku 30 wa ombi kufikiriwa. Ninaomba taarifa hizi nyingi ziwe kwenye Wizara, ziwe kwenye Idara za Serikali, ziwe kwenye Mikoa, ziwe kwenye Halmashauri, ziko ndani ya taasisi. Kwa hiyo, zinaweza zikatafutwa na kutolewa ndani ya saa 24, kwa nini siku 30?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi siku 30 ni nyingi sana, kifungu hicho chote kifanyiwe marekebisho ili kupunguza muda wa kupewa taarifa, iwe aidha ndani ya saa 24 au ndani ya saa 48 ili kusudi kweli tuoneshe kwamba tuko *serious* kama nchi kuweka *transparency* katika jamii yetu ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa, kifungu kidogo cha sita na vifungu vingine vinavyozungumzia adhabu. Adhabu zilizomo ni kubwa mno! Hazitoi nafasi kwa wakosaji kupata adhabu na hapo hapo kujirekebisha ili warejee kuwa *productive* katika jamii. Kifungo cha miaka kumi gerezani, miaka 15 kwa kosa tu la kutotoa taarifa au kwa kosa la kuitumia vibaya taarifa, nadhani hizo adhabu ni kubwa sana zifikiriwe na kupunguzwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naipongeza Serikali kwa kufanya yote haya ni kutoa kwenye jamii ikiwemo Vyombo vya Habari na siyo kuzuia taarifa. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako mzuri. Tunaendelea Mheshimiwa Riziki Mngwali, atafuatiwa na Mheshimiwa Anatropia Theonest na Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba mbingu na ardhi ambaye kwa mapenzi yake mwenyewe ametupangia na ametuamulia na akatuchagua sote kuwa hapa leo, lakini kubwa akatupa uzima na afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nifuatie kwa kukushukuru wewe kwa kunipa fursa hii na mimi nichangie kilichopo mezani kwetu japo kwa uchache kwa sababu mengi yameshasemwa toka jana. Baada ya kukushukuru niseme jambo moja na lenyewe ni kitendo ambacho kinasemwa ni kitendo bora kufanywa hapa duniani, kitendo hiki ni kuhusiana kumcha Mwenyezi Mungu.

Kwa hiyo, na mimi nachukua nafasi hii kuwausia pamoja na kuusia nafsi yangu kumcha Mwenyezi Mungu. Maana yangu ni kwamba tunapousiana hivyo basi tunausiana kuchunga mipaka katika kila tunalolifanya na katika kila tunalolitamka, kwa sababu wale wanaoamini kama mimi kwa upande wetu, tunaamini kwamba kila tunalolifanya hapa duniani haliishii hapa, hiyo siku tunayoiita siku ya hukumu tutaulizwa pia. Naomba niliseme hilo ili siku hiyo nitasema niliwakumbusha wenzangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu kama nilivyosema pale awali yamesemwa mengi, lakini nifuatishe kwa nasaha kwamba tunatengeneza sheria hapa, sheria ambazo wenye lugha yao wanasema; *they can either break or make* hii jamii yetu, kwa hiyo, tuwe na tahadhari sana. Tusije tukatoka

na sheria ambazo badala ya kutengeneza zikabomoa, badala ya kusaidia zikaumiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasemaji wanasema sana kuhusu wenyewe wanaziita *claw back clauses* kwenye kutengeneza sheria au hata kama zile ambazo zimo kwenye Katiba. Ukiangalia Muswada ambao uko mbele yetu hapa leo una hizo *claw backs clauses* nyingi tu, kwamba jambo linasemwa vizuri lakini kikija kifungu cha sita ukikiangalia mwanzo mpaka mwisho unaona kama jambo lenyewe kumbe halitakiwi. Ukienda kwenye kifungu cha 10 unaambiwa uandike, ufanyeje! Ufanyeje, sasa kwa nini wakasema yote yale kwa mfano kwenye hicho kifungu cha 10 na kwa nini tusijikite tu kwenye kifungu cha 10(4) ambacho kinasema, nadhani ndiyo hicho kinatoa ruhusa kwamba asiyeweza kuandika na mambo mengine kwamba atasema tu pale kwa mdomo huyo mhusika anaweza yeye akajaza basi iwe hivyo. Tunakwenda kwenye maofisi fomu iko pale, mimi naitwa fulani nataka taarifa, kinachukuliwa kikaratasi kama hiki tunachoomba hapa kuchangia, unajazwa jina lako na ile taarifa unayotaka inapelekwa hapo.

Mhehimiwa Mwenyekiti, wengi wamesema kuhusu muda, hivi kuna haja ya kusema tusubiri siku 30 na hilo litatumika. Hao wenye taarifa watalitumia hilo. Mimi nakwenda kituo cha polisi, naenda kumuona *OCD* kwa sababu kuna watoto vijana wamepotea kwenye Wilaya yangu, kwenye Jimbo langu. Wazazi wanalalamika, wanasema hata tukienda hatusikilizwi, najipiga kifua nakwenda mimi kama Mbunge, naambiwa eehh mama sasa tuandikie hapo, tuandike nini? Watoto fulani na fulani wa nyumba kadhaa wamepotea na wamepotea kwa sababu wamechukuliwa na askari wako Mheshimiwa *OCD* niambie, naambiwa niandike. Hivi hizo taarifa nazo ni za kuandika?

Sasa labda tuseme ni taarifa za namna gani kama itabidi huu Muswada ushughulikie yote hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapata taabu sana kwamba masuala kama haya ya Miswada na bahati hii Mwenyezi Mungu ametusaidia katika Wizara ya Katiba na Sheria yupo msomi wa sheria, ambaye mimi siyo tu ninamheshimu kama kaka yangu, lakini pia huwa napenda kumpa daraja ya mwalimu wangu, ingawa hakunifundisha lakini marafiki zake wa karibu Profea Mahalu, Profesa Peter na Profesa Kabudi wamenisomesha, kwa hiyo Mheshimiwa Mwakyembe pia napenda kumpa heshima ile. Ninampa heshima hiyo kwa sababu miongoni mwao hawa wanamtaja kwa uzuri, napenda sana ule uzuri ninaousikia kwa wale wenzake ujioneshe hapa kwenye kazi hii, kwenye mamlaka haya, kwenye jukumu hili alilopewa kulisimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwakyembe tuongoze tutoke na miswada ya sheria na tuje tutengeneze Sheria kwenye Bunge hili ambalo tutaishi sisi na vizazi vyetu waje

waseme *yes!* tulikuwa na *Ph.D* kwenye Wizara ya Katiba na Sheria na *these are the laws* ambazo zilifanywa kwa wakati huo, nakusihi sana tusaidie hilo. Kwa maana hiyo basi tutaanza na muswada huu, Kamati ya Kudumu ya Bunge imesema, Kambi ya Upinzani imesema tutengeneze sheria ambayo kweli inatufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha sita kina utata sana, kifungu cha 19 kina walakini mwingi tu. Kifungu 19(2) kinasema; "Mkuu wa Taasisi ndani ya siku 30 baada ya kupokea maombi yaliyofanywa chini ya kifungu kidogo cha (1) ataamua maombi kwa mujibu wa taratibu walizojiwekea." Taasisi wamejiwekea wenyewe taratibu, mimi ninayekwenda kuomba taarifa sijui taratibu hizo lakini ninabanwa na taratibu hizo. Maslahi ya umma, umma ni nani kama syo mimi? Pia kuna hizo zinazobana. *(Makofi)*

Mheshimwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa kweli napenda tuuangalie huu muswada kwa namna ya kipekee na nilikuwa nawauliza wenzangu wanaojua zaidi taratibu na sheria hivi kusoma mara ya pili na mara ya tatu na kuhitimishwa na kupitishwa maana yake nini? Kama hatuna ulazima huo tuurudishe ufanyiwe kazi. Nasema hivyo kwa uzoefu mdogo pia niseme kwamba mara nyingi hizi kazi zinafanywa kwa *speed* ya ile kama tunazima moto vile. Tunawa-*overwork* wataalam wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kupata uzoefu kidogo nikiwa kwenye Tume ya Mheshimiwa Warioba, wale vijana tulikuwa tunawa-*overwork* mpaka wengine wanakuja asubuhi unamhisi mtu anatetemeka hivi, kwamba hajapata hata muda wa kupumzika, na nilivyowaona wachache waliokuja kwenye Kamati yetu unahisi hivyo, wana mengi hawa vijana, kama tunapanga hizi sheria kwa ajili yetu, jamani tuzipe muda, wataalam wetu tuwape muda walete mambo ambayo kweli yanasaidia na siyo kama haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *seriousness* inaonekana pia katika kuamua mnafanya nini. Hii karatasi hii inaitwa *order paper* au imeandikwa Orodha ya Shughuli za leo inasema tunajadili Muswada wa Sheria ya Upatikanaji Habari. Hii imeandikwa leo, jana Mheshimiwa Waziri kasema ni Muswada wa Upatikanaji Taarifa, sasa tunasema ya jana taarifa au ya leo habari? Tunachojadili hasa ni Muswada upi? Kama kweli tunataka kuwa *precise* na kujua tunajadili na ndiyo maana unatuona humu tunaogelea, kwamba wanaokuwa na upande wa habari unaonekana habari lakini taarifa nayo inatofautiana vipi na hiyo habari nayo pia haieleweki.

Kwa hiyo, sasa hayo pia ni masuala ambayo tungependa sana tuyaone yakifanyika katika Bunge lako hili, wengine tunapata hofu zaidi kwa sababu tulisimama pale, tukashika kitabu, tukaapa na kila siku siku asubuhi humu

tunaapa kwamba tutatumia busara zetu, tutatumia hekima yetu ili tutengeneze sheria ambazo zina maslahi na zinaleta haki na usawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, tujiulize hizo sheria ambazo tumeshazitengeneza au zimeshatengenezwa na Bunge lako zimesaidia vipi, hizi sheria kama hizi ambazo zinaletwa kisha zikajadiliwa katika mihemko ya kisiasa na kebehi na maneno ambayo hayajengi na wengine wanatoka kabisa nje ya mada tena unawavumilia halafu unawaambia kwa uwezo wako ulivyojadili na kuchangia, sijui kama inatusaidia kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba sana labda kwa uzoefu wangu wa kuwa mwalimu na huu uzee unaonikaribia nakuwa *very conservative,* lakini kuna mambo ambayo ningependa kabisa *seriousness* i-*prevail*, tujadili haya mambo kwa maslahi ya Taifa letu, kizazi hiki na kizazi kijacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa MWenyekiti, sidhani kama nina mapya mengi labda nikushukuru na nina hakika wengine pia watachangia zaidi na kama nilivyoomba, nafasi zaidi itatolewa *who to shelf* kwa muda tutoe muda zaidi ili tuje na Muswada na baadae sheria iliyo nzuri zaidi.

Ninakushukuru na nimalizie tu kwa lile jambo bora kwamba nawausia pamoja na kuiusia nafsi yangu tumche Mwenyezi Mungu na kwa maana hasa ya kumcha. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Riziki kwa mchango wako mzuri tu.

Waheshimiwa Wabunge, tutahitimisha Muswada huu leo saa 12, mtoa hoja ataingia. Sasa nawasihi ili hawa ambao tunao wachache hapa, mchana huu tuchukue dakika kumi tu kila mmoja halafu jioni wale wanne wanaweza wakawa sita, mnaonaje, sawa?

**MBUNGE FULANI:** Sawa!

**MWENYEKITI:** Haya! ninyi watu waungwana sana.

Mheshimiwa Anatropia Theonest atafuatiwa na Mheshimiwa, kama nilivyosema Mheshimiwa Sakaya.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa fursa hii, ninaushukuru Uongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, nawashukuru kwa uwasilishaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni walivyoweza kuudadavua muswada na kabla ya yote nianze kwa salamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe salamu nyingi sana kwa Mkuu wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Kamanda Sirro kwa kazi anayoifanya hasa baada ya kupitishwa kwa Sheria ya *CyberCrime,* kupambana vizuri na watu wanaotoa uhuru wa kujieleza. Anaweza kusema anaweza kufanya yote lakini ikiwa ni pamoja na kukamata na kupiga, lakini ajue unaweza kumpiga mtu sana, anaweza kuumia mwanzo lakini akaota sugu na ikawa ni mfumo wa kawaida. Kwa hiyo, apige tu, tutaota sugu, wataota sugu na itakuwa ni sehemu ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongeze pale kwamba siyo kila kimiminika kinazima moto, vingine vinachochea moto! Hiyo ni salaamu kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeupitia vizuri muswada, mwanzo mpaka mwisho nikajaribu kuaninisha, nikaangalia dhamira hasa ya Serikali tuliyonayo ya Awamu ya Tano inayojinasibu kwa kuchapa kazi, inayojinasibu kwa kuwataka au kwa kuwatetea wanyonge. Mimi natia shaka, nimeiangalia hiyo dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano katika muswada uliokuja, muswada nimeweza kuuchambua katika vipengele vikuu vitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele cha kwanza ni kwamba Muswada ni wa kibaguzi, Muswada ni wa kibaguzi katika Ibara ya Nne. Ibara ya Nne inambagua nani apate taarifa kinyume kabisa na Katiba ya Jamhuri ya Tanzania, kifungu cha 18 Ibara ndogo ya kwanza inayoeleza kila mtu anayeishi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ana haki ya kupata habari lakini huu Muswada unasema anayeishi ndani ya Jamhuri ya Muungano awe raia ndiyo mwenye uwezo wa kupata habari, huo ni ubaguzi wa hali ya juu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubaguzi mwingine tumeuona mkiibagua Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Masuala ya kisheria ni masuala ya Muungano kwa hiyo sasa muswada unaanza kupoteza uhalali au sheria inapoteza uhalali pale tu inapoamua kubagua kundi fulani dhidi ya kundi lingine. Tunawabagua watu ambao wako ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao wengine wana maslahi pia. Tunao wawekezaji, *donors*, kuna watu wamewekeza pesa zao kama *donors* ambao wana-*deserve* kupata taarifa kutoka kwenye Wizara mbalimbali ambako hela yao ndiyo ipo na hapo ndiyo nilipoona dhamira ya Serikali kuuleta huo muswada kwamba watu wanawapa pesa zao, kama *donors* kama *business partners* na mnawaambia kupitia sheria au muswada mliouleta hamna uhalali wa kupata habari. Hiyo ni *weakness* ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshauri Waziri wa Katiba na Sheria kwamba sheria yeyote ambayo inaonesha dhamira ya kubagua watu haina manufaa, tuondoe sasa kuwabagua wote walioko ndani ya Jamhuri kusema raia na badala yake tuseme kila mtu ambaye yuko ndani ya Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania ana haki ya kupata taarifa sambamba na hitaji la Katiba ya Jamhuri ya Muungano, hiyo ni ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pungufu la pili nililoliona katika huu muswada ni suala zima la kutaka kunyang'anya haki. Tunakaa upande mmoja wa kutaka kutoa taarifa, lakini upande wa pili tunaeleza ni namna gani ni ngumu kuwapa watu taarifa. Hiyo imejidhihirisha katika namna ambayo watu wanaweza kupata taarifa, mlolongo, *bureaucracy* na wote tunajua *justice delayed, it is justice denied*. Kama tunawachelewesha watu kupata taarifa haina tofauti na kuwanyima taarifa, nitakusomea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vifungu mbalimbali ambavyo nitaainisha kabla ya kifungu cha 14 na nianze na kifungu cha 11. Mtu anaomba kupata taarifa kwa mmiliki wa taarifa ambaye ombi lake linatakiwa ndani ya siku 30, unaongelea kutoa taarifa ndani ya siku 30 kwa mujibu wa muswada mliotuletea hapa. Kama haitoshi, yule anayemiliki taarifa anamwambia wa chini yake kwamba atoe taarifa ina maana yule *third party* atoe taarifa au anatoa taarifa baada ya siku nane na wanaenda mbali zaidi, anayemiliki taarifa atamwambia mtu wa tatu kutoa tarifa haraka inavyowezekana ndani ya siku nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Serikali ya Awamu ya Tano inatambua haraka iwezekanavyo ni siku nane, hiyo ni haki kweli? Lakini kama haitoshi kifungu kinaonesha kama mmiliki wa taarifa amepata ombi, kama anaona hatatoa hiyo taarifa inahitajika siku 30 kutoa jibu la taarifa ipo au haipo. Tunaanza kwa siku 30 za kwanza, tunakuja siku 30 za pili ambazo amekata rufaa kwa kutopewa taarifa, lakini pia inafuata siku 30 kwa Waziri ambayo ni ngazi ya tatu kueleza *whether* atatoa taarifa au hatatoa taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu ambao mnasifia muswada tunaongelea siku 90 za raia wa Tanzania kupata taarifa ambayo sasa kwa mawazo ya muswada huu kipengele cha 6(2) kinaongelea mambo ya *national Interest*. Tumeweka kipengele hiki makusudi kama chaka, kwa sababu tumekuwa tukitumia kwanza neno la *national interest* tofauti na matarajio ya wengi na ni ngumu ku-*set boundaries* za *national interest*. Tumeona kadha wa kadha hili neno likitumika kunyima wanahabari taarifa makusudi kabisa na tunakileta hapa kwenye kipengele cha sita tukiwa na lengo lile lile la kunyima taarifa kwa sababu ya kifungu 6(2)kwamba ni kwa ajili ya *national interest*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi adhabu tunazozitoa ambayo ni kipengele changu cha tatu. Nilisema cha kwanza ni ubaguzi, cha pili *bureaucracy,* lakini cha tatu ni adhabu zinazokuja kutolewa.

Katika *organization*, katika Wizara kuna watu wamedhihirika kuwa wanafanya kazi bila kuwa na nia njema, lakini mle kwa watu ambao hawana nia njema kuna wenye nia njema ambao wamekuwa wakitoa taarifa na ninyi mnasema wale watakaotupa taarifa kwa mujibu wa kipengele cha 6(6) kinasema mtu yeyote atakayetoa taarifa iliyozuiliwa kinyume na mamlaka anapewa adhabu ya miaka 15 mpaka miaka 20. Ni kwa nini tunaamua kuwaadhibu watu kwa kiwango kikubwa namna ile. Kusudi iko *very simple* tu tunataka tuwazibe mdomo, hata wale waliokuwa wanafurukuta kwa nia njema waliyokuwa nayo kwa kuona mamlaka iliyokuwepo wanafungwa mdomo.

Mimi kama Mbunge mwenye wajibu wa kuishauri Serikali ni lazima tuangalie upya. Tunawafungaje watu miaka 20? Kwa kosa lipi? Ni lazima tuangalie. Hili kosa lina uhusiano gani na usalama wa nchi? Tujiridhishe. Kwa makosa mengine ya kawaida ambayo mmeainisha kifungo kiwe miaka mitatu mpaka miaka mitano, lakini *plus* faini au mtu anaweza kutoa *either* faini au akafungwa kifungo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza mambo makubwa matatu niliyoyaona katika hii sheria na ninaendelea kushauri kama wenzangu walivyosema, sheria yenye lengo la kubagua watu ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sheria yenye lengo la kushindwa kuwapa watu taarifa kwa sababu ya milolongo na taratibu iliyowekwa na huu muswada, kama hazitaondolewa au kama hazitakuwa *addressed otherwise* hatuna maana ya kupoteza muda kujadili kitu ambacho kinaenda kuwatesa watu wetu. Tumekuwa muda mwingi tunajadili hapa kwa ushabiki, tumekuwa muda mwingi tunasifia, tunasahau kwamba wajibu wetu ni kuikosoa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge mwingine amekuja anajaribu kusifia kwamba imeshirikisha wadau, nimejiuliza kwenye suala la wadau, kama tunaongelea habari za kutoa taarifa, tumewaletaje wadau wa habari? Tunasikia wamekuja wa MCT, JUKATA na TEF, *are these real stakeholders*? Kama tunaongelea Muswada wa Habari *then these are the people,* lakini kama ndiyo wao tumewa-*consult* tuna *mislead the public*. *There are stakeholder's* ambao wanaenda kutoa taarifa husika *not these ones! (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Sakaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi ajiandae.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi hii ya pekee nami niweze kuchangia kidogo kwenye muswada ulioko mbele yetu. Kabla sijaenda kwenye muswada naomba nitumie dakika zangu chache niwatoe wapiga kura

wangu wasiwasi. Wapiga kura wangu wa Jimbo la Kaliua na wananchi wote wa Tanzania niwatoe wasiwasi kuwa taarifa ambazo zimetolewa kwenye *media* na kwenye mitandao ya kijamii kwamba Mbunge wao kasimamishwa Ubunge, hizo siyo taarifa za ukweli, ni taarifa za uzushi, ni *propaganda* waachane nazo. Mimi Mbunge wao Magdalena Sakaya niko hapa imara na ninawajibika kwenye majukumu ya kazi waliyonituma kwa uaminifu wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muswada uliopo mbele yetu inawezekana ulikuwa una malengo mazuri sana lakini malengo hayo mazuri hayawezi kufikiwa kwa namna ambavyo muswada huu umeandikwa. Ukiangalia kuanzia mwanzo wa muswada mpaka mwisho kuna milolongo mingi ambayo mingine unaona kabisa haina sababu, kwa hiyo, inawezekana ile tija halisi ambayo tulikuwa tunaitegemea isifikiwe kutokana na kwamba kuna milolongo na kiukweli ni urasimu mkubwa ambao hauna sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipiga mahesabu ya kawaida kwa nini sasa hivi kwa Wizara ya Ardhi kwa mfano, kupata hati unachukua mwezi mmoja, kwa nini kupata taarifa ichukue karibu miezi mitatu? Wakati tunataka sasa hivi turahisishe mambo, twende kwa mwendo wa kisasa tuachane na kuishi kwa mazoea huku nyuma. Tunaomba ili muswada huu uweze kuwa na tija ni lazima kuhakikisha kwamba tunauandika kwa namna ambayo utakwenda kukidhi mahitaji na malengo yaliyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye kifungu cha 4(e) sheria inaweka kinga kwa wanaotoa taarifa njema zenye maslahi kwa Taifa. Ni kwa namna gani ningependa kujua sheria hii kuna watu ambao wamekuwa wanatoa taarifa mbalimbali kwenye taasisi mbalimbali kwa mfano taasisi zinazozuia uhalifu kwenye vyombo vya polisi, matokeo yake taarifa zile zinatolewa na watu wale wanadhuriwa maisha yao, wapo walipoteza maisha kwa sababu tu wametoa taarifa ambazo zina maslahi kwa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamlindaje mtu kama huyu ambaye ametoa taarifa polisi au kwenye vyombo vya dola kwa nia njema ya kuokoa Taifa wanamzunguka wanaenda kutoa taarifa zile kwa wale ambao ni wahalifu wanakuja kumjeruhi au kujeruhi familia yake. Sheria hii ituambie watu kama hawa wanakwenda kulindwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa wale ambao wanatoa taarifa za *informers* kwenye *public*, watu kama hao na wenyewe sheria hii inakwenda kuwaba namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele cha 5(4) namna sheria pia inatoa fursa kwa mamlaka yoyote kutunga sheria itakayotaka mamlaka ya umma kutoa taarifa. Tunalo tatizo sugu sana, namna gani sheria hii wana-*harmonize*

na Sheria ya *Local Government*. Kwa sababu tuna tatizo kubwa Sheria ya Serikali za Mitaa inasema kwamba lazima Serikali za Mitaa, Vijiji, Vitongoji, Kata mpaka Wilaya kila mwaka wawe na mikutano minne ya wananchi kutoa taarifa za mapato na matumizi, nchi nzima ni tatizo sugu. Taarifa hazitolewi, wananchi wanahoji hawaambiwi na bahati mbaya Mwenyekiti wa Kijiji na Mtendaji ndiyo wanatakiwa waitishe mikutano, kwa sababu wanaiba fedha za wananchi, wanakula hela za maendeleo, hawaitishi mikutano. Ningependa kujua sheria hii itawasaidijiaje wananchi kupata zile taarifa kwa wakati?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila baada ya miezi mitatu wahakikishe kwamba mikutano ya hadhara imekuwepo, wasomewe taarifa za mapato na matumizi, waambiwe fedha zao zimepatikana kiasi gani na zimetumikaje, halifanyiki. Kwa hiyo, ningependa sheria hii wa-*harmonize* na Sheria ya *Local Government* ili wananchi wale waweze kupata taarifa za maendeleo ya miradi yao na fedha wanazochanga kwa ajili ya shughuli zao za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni Kifungu cha 11, ukikiangalia kifungu hiki cha 11 kimeletwa muda mrefu sana, ni vigezo gani vimetumika kuweka siku 30 kwa nini tunaweka siku 30, kwa sababu kitendo cha kuweka muda mrefu kinaweka uwezekano wa taarifa ambayo ingepatikana kwa muda wa siku mbili kuchukua siku 30, ni kwa nini hakuna *categorization?*

Kwa hiyo, ningependa kwanza watuambie ni kwa nini wamefikia kuweka siku 30 na siyo siku chache labda mbili au wiki, inapolazimu ndiyo mtu asogezewe muda, kwa nini ni siku 30; kwa hiyo hilo nalo tunaomba tupatiwe ufafanuzi wa kutosha wakati Mheshimiwa Waziri Dkt. Mwakyembe anakuja kutujibu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 11(3) mwombaji wa taarifa atathibitisha vipi kwa sababu kifungu hicho kinasema kwamba ikiwa mmiliki atathibitisha kwamba taarifa hiyo haipo, ningependa kujua mwombaji wa taarifa atathibitisha vipi kwamba kweli taarifa ile haipo na kwamba hajanyimwa? Kuna chombo gani kimeandaliwa kuweza kuhakikisha kwamba wanaomba taarifa wanatendewa haki. Maana yake ukiangalia sheria hii imemlinda sana mmiliki wa taarifa lakini yule anayeomba taarifa hajalindwa kwa lolote, sasa tungependa kujua nani anayethibitisha kwamba kweli taasisi fulani, taarifa inayotafutwa mle haipo. Kwa sababu mmiliki anasema haipo na wewe umeandika barua siku 30 unajibiwa haipo, nani anayethibitisha kwamba kiukweli taarifa hiyo haipo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 19 pale ambapo Mkuu wa Taasisi anakuwa ndiye mmiliki wa taarifa unaomba taarifa kwa Mkuu wa Taasisi na yeye mwenyewe ndiye mmiliki na anakataa kutoa, sheria inasema lazima ukate rufaa kwa Mheshimiwa Waziri. Naona hii ni kuendelea kuweka mlolongo wa

mambo mengi, hivi Waziri atapokea taarifa za watu wangapi, atapata rufaa ngapi, kwa nini tusiweke sheria kumlazimisha mmiliki wa taarifa kuweza kutoa taarifa pale inapotakiwa kwa wakati? Kwa nini mpaka tuseme kwamba akikataa kutoa mmiliki twende kukata rufaa, Waziri ataacha ku-*concentrate* kwenye mambo mengine, tunaomba sheria hii imbane yule mmiliki wa taarifa ahakikishe kwamba anapotakiwa kutoa taarifa anaitoa na asipate *loophole* ya kuweza kukatalia taarifa zinazotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 20 kwenye *version* ya kiswahili inasema kwamba Waziri anaweza kutengeneza kanuni naomba itoke Waziri 'anaweza'; iseme Waziri atatengeneza kanuni nimeona kwenye *version* ya kiingereza ni nzuri '*shall make*' lakini ukija kwenye kiswahili inasema Waziri anaweza, maana ya kusema kwamba anaweza au asiweze, ni *option,* asipewe *option* ni lazima atengeneze kanuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 21, kinasema kwamba mmiliki wa taarifa kutoza ada iliyowekwa nani anaweka viwango vya ada kwa sababu kama mmiliki hataki taarifa itoke anaweza kuweka viwango vikubwa ili mhitaji wa taarifa ashindwe kumudu. Kwa hiyo, ni nani anayeweka viwango vya tozo za kuweza kupata taarifa zile lazima iwekwe wazi kwamba *who is going to make this option* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tozo zitakazowekwa ziendane na hali halisi ili anayehitaji taarifa aweze kuzipata kwa gharama ambayo ni *affordable* kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kifungu cha 23, kinahusu kinga kwa mtoa taarifa. ukiangalia sheria yote hii, utaona kwamba mtoaji wa taarifa amelindwa sana kama nilivyotangulia kusema lakini muhitaji wa taarifa au mwombaji wa taarifa hajalindwa kwa lolote kwa maana nyingine ni kama vile unampa mtu haki kwa mkono wa kushoto, unaichukua kwa mkono wa kulia unaiweka mfukoni kwa muda wote haiwezi kupatikana hiyo haki. Kwa hiyo, ni lazima sheria ieleze kwamba mmiliki wa taarifa analazimika kutoa taarifa kwa muda unaotakiwa kwa viwango vinavyotakiwa, ili kweli malengo ya sheria hii yaweze kutekelezwa na yaweze kufikiwa kama kweli dhamira ni Watanzania wapate taarifa kwa ajili ya maendeleo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako na kwa kuokoa muda pia. Mheshimiwa Angelina Malembeka.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.

Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha na mimi kuwepo hapa, pili nichukue nafasi hii kuwapa pongezi Wabunge wenzetu wa UKAWA kwa kurudi Bungeni. Nilikuwa najiuliza wenzetu hawa walitoka kwa hiari yao na wamerudi kwa hiari yao haya wanayoyasema wangeyasemea wapi kama wangekuwa nje. Kwa hiyo, kwa kurudi kwao nimefurahi sana kwa sababu hata sisi michango yao pia tunaipenda yapo mambo tunajifunza kutoka kwao. Kwa hiyo, nilikuwa najiuliza wanapokaa nje hayo maneno watasemea wapi?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuendelea pamoja na pongezi zao wanazozikataa nimpongeze kipekee Mheshimiwa Magdalena Sakaya kwa kutoa taarifa kwa sababu mara zote michango yake pia huwa mizuri ambayo pia inaisaidia Serikali. Sasa tulikuwa tunajiuliza kama na yeye anatoka inakuwaje sasa humu ndani, sisi tunapenda michango yote ya pande zote mbili ili Serikali iweze kuifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi niwapongeze Wabunge wenzangu wa Chama cha Mapinduzi ambao hawajawahi kununa wala kutoka ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa Muswada wa Sheria ya Upatikanaji wa Habari wenzangu wamechangia mengi, lakini na mimi ninayo machache ya kuongezea nyama na pale Serikali ambapo itaona inafaa basi nao watayafanyia kazi. Kabla ya kutoa mchango huo wapo Wajumbe kadhaa ambao wameizungumzia suala la ubaguzi humu ndani, lakini wao wenyewe ndiyo wamekuwa wabaguzi wa kwanza kwa kuhoji kwa nini Wabunge wa Zanzibar wanachangia hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wanaotoka Zanzibar ni Wabunge halali wa Bunge la Muungano wa Tanzania sawa sawa na aliyetoka Rombo, Mwanza, Singida, au Kagera, kwa sababu wote wana majimbo yao na waliokuja kwa mikoa yao wamekuja kwa Mikoa yao ambayo iko ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wanapohoji kwa nini Wabunge wa Zanzibar wanajadili hili wanajisahau wao kwa nini wali-*panic* Jecha alipofanya vitu vyake kule. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala haya ya kujifanya huelewi tofauti ya Baraza la Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Muungano ndiyo walioyafanya waponze wenzao mpaka wakakosa Madiwani na Wawakilishi Zanzibar yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusiana na suala la hii sheria ambayo wanahoji kwa nini itumike Bara pake yake isitumike Zanzibar. Mimi ninaamini hii siyo sheria ya kwanza ziko sheria nyingi ambazo zimetungwa

zinatumika Bara peke yake na Zanzibar hazitumiki. Nikitolea mfano kuhusu umilikaji wa silaha za moto, Zanzibar raia yeyote haruhusiwi kumiliki silaha yeyote lakini Bara wanaruhusiwa, ni Bunge hili lilipitisha hawa hawakuliona au wanakuja kushangaa hii tu ya habari? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado niongelee kuhusiana na suala la adhabu, kwa upande wangu nimeona adhabu hii ni kubwa, kwa sababu hawa wanahabari wetu katika kuleta habari zao tunaweza tukajistukia magereza zote zimejaa wao, kule hatutaweza kuwalisha, hatutaweza kuwatunza, ni afadhali basi adhabu hii ipunguzwe, isipokuwa iongezwe kwa yule mtu wa kwanza mtoa habari, kwa sababu yule mtoa habari wa kwanza kama ataachiwa itakuwa anaendelea kutoa habari na wenzake wanaendelea kuzipotosha, sasa ni vizuri yule wa kwanza kabisa ndiyo apewe adhabu kubwa zaidi kuliko wale wengine wanaozambaza zile habari hata kama ni za upotofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuchangia hayo naona Muswada huu upo vizuri kwa sababu umetoa haki ya kupata taarifa kama Katiba ya nchi inavyotaka. Sasa hivi hali ilivyo unaweza kwenda kuomba taarifa na usipewe na huna wa kumuuliza na unaweza usijibiwe na yakaisha kimya kimya. Lakini kwa Muswada huu ambao tunapitisha bado itampa nafasi kubwa mwananchi kupata taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda ni mfupi umesema tutumie dakika 10 nina wenzangu ambao wana michango mizuri zaidi ninashukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako, mchango mzuri tu. Mheshimiwa Mtolea kwa muda tulionao nadhani utatutendea haki.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kwa uchache sana niweze kuchangia kidogo kuongezea kwenye yale ambayo jana niliwasilisha kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana kuna watu walikuwa wanasema hapa wanaomba tuaminiane, mimi niwaambie tu suala la kuaminiana siyo suala la kusimama na kusema, tunaaminiana kwa vitendo, ukifanya vitendo unaijenga imani *automatically* na ukiona kuna tatizo la imani kati ya Serikali na wananchi, maana yake tatizo lipo upande wa Serikali kwa sababu Serikali ndiye mtendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokuwa tunajadili Muswada huu tunahitaji kujua, kweli huu muswada umeletwa hapa kwa ajili ya maslahi mapana ya Taifa au kwa ajili ya maslahi mapana ya Mtawala, na kabla hatujafika huko

kwanza tuangalie Muswada huu wa Sheria ya Kupata Taarifa, lazima tuanze kuangalia mambo machache ambayo yameizunguka tasnia hii ya habari kabla hatupitisha muswada huu, ili tunachokipitisha hapa kisijekuwa ni mwendelezo wa kuwakandamiza zaidi watu wanaohusiana na vyombo vya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia hapa, vyombo vya habari vikifungwa, magazeti yakifungiwa na kosa linaweza kuwa pengine ni la mtu mmoja au mhariri au mwandishi hakufanya kazi yake vizuri, lakini linafungiwa gazeti lote. Katika kipindi hiki ambapo nchi ina tatizo kubwa la ajira, unalifungia gazeti, kuna mtu kazi yake ilikuwa ni kufagia tu ile ofisi inayotolewa lile gazeti anahusika vipi kwenye machungu haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekitii, kwa hiyo tunahitaji kufikiria zaidi wakati tunazitunga hizi sheria ili zisiende kuwatesa watu ambao hawakustahili kuteswa, unaangalia hapa kwa mfano hii sheria imekuja imetoa adhabu kali kweli, moja ya adhabu ambayo inayotolewa hapa ni kifungo cha miaka 15 mpaka miaka 20, hiki kifungo ni kikubwa mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kwamba nchi yetu yenyewe inakabiliwa na tatizo la mlundikano wa wafungwa magerezani na hao wafungwa wamejazana huko kwa sababu kila sheria tunayoitunga haiweki adhabu mbadala inakimbilia tu kuwaapeleka watu gerezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nategemea hii sheria kwa kuwa inawahusu wengi ni wataalamu ambao watakuwa ni watumishi, wataalamu wa habari, ndiyo wanaoguswa na sheria hii tuwape adhabu mbadala, adhabu iwe ni mtu kumfungia kufanya ile shughuli japo kwa mwaka mmoja, miaka miwili siyo kumpeleka gerezani, tumsaidie Waziri wa Mambo ya Ndani kupunguza wafungwa magerezani. Unamfunga mtu miaka 15 kisa tu alikosea kutoa taarifa kwa nini usimfukuzishe tu kazi, kwa nini asikae nje tu ya hiyo ajira yake kwa miaka miwili au mwaka mmoja, ni adhabu ya kutosha sana. Nimuombe Mheshimiwa Waziri uangalie hii adhabu ulizoziweka hapa wala haziwezi kuwa *applicable,* zitawatesa watu, tuwape watu adhabu zinazolingana na taaluma zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata taabu tena kwenye hizi siku 30 za kusubiria hizi taarifa. Mwanzo unapousoma Muswada huu unaona pengine huu Muswada una lengo zuri labda una lengo la ku-*compel government* iweze kutoa taarifa lakini sasa unapoweka hii *turn around* ya siku 30 unaona ile nia njema ya Serikali inaondoka! katika karne hii ya sayansi na teknolojia unawezaje kusubiri taarifa kwa siku 30?

Mheshimiwa Mwenyekiti, najaribu tu kufikiria kwa sauti kwamba labda Askari Polisi Mpelelezi anahitaji kupata taarifa za kitabibu za binti aliyebakwa, kama daktari kwa maksudi ataamua kumzungusha kwa kutumia *loophole* zilizopo katika sheria hii hizo taarifa zinaweza zikatoka wakati huyu binti emeshajifungua, kama siku hiyo alipata ujauzito. *(Makofi)*

Sasa tukiiangalia hi kwa maana tu ya kuya-*target* magazeti, tukumbuke kwamba kuna vitu vingine vingi vya kijamii tunavisahau na watu watakuja kuumia.

Kwa hiyo naomba *turn around time* ya kupata hizi taarifa iwe ni ndani ya saa 24 kama taarifa imeombwa kwa njia ya kielektroniki, lakini kama imeombwa kwa njia ya barua ya maandishi ndiyo iweze kuchukua siku saba kwa sababu ndio utaratibu wa kawaida kwenye ofisi zenu barua zinajibiwa ndani ya siku saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi taarifa tunapoziomba tunaziomba kwa sababu zipo na mnazo, hatuombi hizi taarifa ili muende mkazitafute halafu ndiyo mzilete. Lakini kwenye sheria mnasema hizo siku 30 ni za mtoa taarifa kujibu kwamba hiyo taarifa ipo au hiyo taarifa haipo au hiyo taarifa anaweza kuitoa yote au kuitoa sehemu, hivi majibu haya yanahitaji siku 30.

Mheshimiwa Waziri nikuombe sana ukija utuwekee wepesi katika kuzipata hizi taarifa, tuzipate hizi taarifa tukiomba kwa njia ya kielektroniki zije ndani ya masaa 24 na kama kwa maandishi basi zije siyo chini ya siku Saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Heche unaweza ukachangia?

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda mnauona hata ninyi, nina tangazo linatoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, anawatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo saa saba mara tu baada ya kusitisha shughuli za Bunge watakuwa na kikao ambacho kitafanyika Ukumbi wa Msekwa D; kwa hiyo, mnaombwa mhudhurie.

Waheshimiwa Wabunge, tumejitahidi hatutamaliza orodha hii tutatenda haki maana ndani ya dakika 60 saa 11 mpaka saa 12 tunaweza tukachukua Waheshimiwa Wabunge sita kwa dakika 10 *unless* mmoja anaongea kwa dakika tano, lakini sura ndiyo hiyo.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ambao wamo kwenye orodha ni Mheshimiwa John Heche, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani, Mheshimiwa Mary Chatanda, Mheshimiwa Augustine Vuma Holle na

Mheshimiwa Upendo Peneza, hivyo hiyo ndiyo sura ya mchana, baadaye mtoa hoja ataingia.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo nawashukuru kwa michango yenu asubuhi hii, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.55 Mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE - KATIBU MEZANI:**

**MUSWADA WA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Upatikanaji wa Habari wa mwaka 2016**
***(The Access to Information Bill, 2016)***

*(Majadilliano yanaendela)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa na orodha ya wachangiaji wachache ambao walikuwa wamebaki na tulikuwa tumekubaliana tuokoe muda, badala ya adakika 15 tutumie kila mmoja dakika 10. Sasa naanza na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Muswada wa Sheria wa Upatikanaji wa Habari wa mwaka 2016.

Pia nichukue nafasi hii kuwapongeza sana wenzetu Kamati ya Katiba na Sheria ambao waliona umuhimu wa kuleta sheria hii ili tuweze kuichanganua kadri tutakavyoweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, naomba pia niwapongeze sana wadau wote walioshiriki kuchakata sheria hii wakiwemo Chama cha Wanasheria, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Sekretarieti ya Msaada wa Sheria, Baraza la Habari Tanzania na wadau wengine wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba ni jambo jema sana ambalo limeletwa kwetu kwa misingi ya kwamba kutokana na hali halisi juu ya upatikanaji wa habari ambao umekuwa ukiendelea katika nchi yetu,

kumekuwa na haja kubwa sana ya kuleta sheria hii na kuweza kuifanyia marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa habari sasa hivi katika nchi yetu umekuwa ni wa kiholela tu, kila mtu anajiamulia kadri anavyoweza na anaweza akaamua tu akaanzisha habari yoyote ile isiyokuwa na uhakika; lakini pia Taifa letu tayari limeshaingia kwenye hali ya kuwa kila siku kunakuwa na habari zinaibuka na hatimaye tunakuwa na kazi ya kukanusha kanusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachelea kusema habari ambazo zinakuja kinyume na utaratibu ambazo hazijahakikishwa na hatimaye kutolewa, unaweza kusema ni sehemu ya umbea tu. Kwa sababu imeonekena kwamba habari nyiungi sana za kulipuka zinatupiwa kwenye magazeti, zinawafanya watu waweze kuuza magazeti tofauti na hali halisi ambayo inatakiwa iende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii itakwenda sasa moja kwa moja kumbana mtoa habari. Itakwenda kumbana mtu ambaye anayekwenda kutoa taarifa ambayo siyo. Kwa mfano, labda niseme tu, siyo muda mrefu kama mwezi mmoja na nusu au miwili imepita, nadhani wenzangu watakuwa mashahidi, kulikuwa na habari ambayo ilitupiwa kwenye mtandao kwamba Jerry Muro amekuwa ni Kaimu Mkurugenzi Ikulu, lakini ni jambo ambalo lilikuwa siyo la kweli. Hatimaye akasema kwamba amekuwa Kaimu Mkurugenzi na Greyson Msigwa amekuwa Mkurugenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hizi zilikuwa siyo za kweli, badala yake sasa Serikali ikaanza kufanya kazi ya kukanusha jambo hilo. Sasa hatuwezi kuwa na Taifa ambapo kila siku ni kupeleka habari, mtu anaamua tu; kesho yake mtu anaanza kukanusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo ni jambo ambalo kimsingi limempata dada yangu Mheshimiwa Magdalena Sakaya. Leo hii mmeshuhudia yeye mwenyewe anakanusha hapa. Wameshatengeneza habari kwamba amefukuzwa Chama cha *CUF,* jambo ambalo siyo kweli.

Kwa hiyo, tutakapokwenda kuitengeneza hii sheria na tukaiweka sawa sawa, itakuwa inasimama pande zote mbili; hakuna ambaye ataathiriwa na Sheria hiyo. Endapo tu kama mtu ataona yeye anahitaji kufanya hivyo, basi atakuwa ameamua yeye kwa makusudi na sheria itakuwa inachukua mkondo wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, nataka tu niwakumbushe wenzangu; juzi tumepata habari nyingine, eti Makamu wa Rais anataka kujiuzulu. Yaani ni mtu ameibuka tu anaanzisha kitu *from no where*. Kwa hiyo,

nadhani hii sheria ni vizuri tukaenda kuipitisha wote kwa pamoja ili kuepuka vitu ambavyo mtu anaweza akaibuka tu akajifanyia bila sababu za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeshuhudia juzi hapa tunaambiwa kwamba Mheshimiwa Freeman Mbowe ametolewa vitu vyake *National Housing,* jambo ambalo halina ukweli kwa sababu yeye mwenyewe amekuja amekanusha. Eti kwamba anadaiwa shilingi bilioni 1.6. Amekanusha na akasema kwamba anaenda mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sheria hii tukiisimamia vizuri, itacheza pande zote mbili ili kuwafanya watu katika nchi yetu tusiwe na ile hali ya kulipuka, kila mmoja anaamua *from no where* tu, mtu aanzisha habari yake, halafu tunarudi kwenda kukanusha; na tuone hii adha kwamba, badala ya kufanya shughuli nyingine basi tunaanza kuingia kwenye shughuli za kukanusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba naomba nikubaliane na kipengele ambacho kinasema, Sheria ya Usalama wa Taifa isiguswe. Mtu akitoa taarifa upande wa Usalama wa Taifa, mimi nikubaliane na kipengele hiki kwa Sheria ya mwaka 1970, chini ya Ibara ya (6) kwamba mtu huyu kwa kweli achukuliwe hatua za kisheria na aweze kufungwa miaka 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwenye *amendment* kwamba imefanyiwa marekebisho, badala ya kiama 20 na 15, basi mtu anaweza akafungwa kifungo cha miaka mitatu mpaka mitano. Mimi napendekeza miaka 15 na 20 ibaki pale pale badala ya kupunguzwa. Kwa sababu watu wengine watafanya kwa makusudi. Anakwenda kwa makusudi kutoa taarifa za usalama wa nchi ili nchi yetu iingie kwenye janga kubwa; na watu wengine wako tayari hata kujitoa mhanga. Kwa hiyo, miaka mitatu au miaka mitano ni kitu kidogo sana. Naomba kama inawezekana, hili jambo libaki pale pale na hii adhabu ibaki pale pale kwa maana ya miaka 15 mpaka miaka 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nichukue nafasi hii kumshukuru pia Mwenyezi Mungu kwa namna ambavyo imefika mahali ambapo sisi na wenzetu watani wetu tuko pamoja humu ndani. Ni jambo ambalo niseme tu wenzetu hawa tuliwa-*miss* sana na waliporudi sisi tuna amani na kimsingi wao wenyewe waliamua kuziba na baadaye wamezibua wenyewe.

Karibuni sana ndugu zetu, tuendelee kuchakata hizi sheria ili tuendelee kuwa pamoja, tuendelee kushirikiana kwa mustakabali wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naomba kuwasilisha. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Msongozi kwa mchango wako mzuri. Tunaendelea. Mchangiaji wetu anayefuata ni Mheshimiwa Upendo Furaha Peneza.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami pia napenda nichukue fursa hii nichangie katika Muswada huu wa Upatikanaji wa Taarifa. Napenda nianzie katika *section 6(1)(f)* ambacho kinazungumzia *infringe commercial interest.*

Napenda kuishauri Serikali kwamba hapa hatujapata maelezo kamili ya kujua hizi *commercial interest* ni zipi kwa maana ya kwamba kuna taarifa ambazo zinaweza zikawa zinahitajika hasa katika maeneo ya mikataba ambayo nchi inakuwa imeingia na wawekezaji. Sasa kama tukisema na hizi pia ziko katika kile kipengele cha taarifa ambazo haziwezi zikapatikana, maana yake ni kwamba haya ni mambo pia yanayowagusa wananchi moja kwa moja na ni sehemu pia ya *public interest.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia pia sehemu hiyo ya *sub section 6(6)* ambayo inazungumzia *any person who discloses exempt information withheld by the public authority in controversion of this Act commit an offence and shall, on conviction, be liable to imprisonment for a term not less than 15 years.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kipengele hiki nilikuwa napendekeza ya kwamba maeneo haya mengine ya juu ambapo ukianzia kwenye *sub-section (2)* ambayo inazungumzia maeneo ya *National Security,* nilikuwa napendekeza kwamba hii adhabu au hiki kipengele kizungumzie yale mambo ambayo yako chini tu ya mambo ya *National Security,* lakini mambo ambayo yako juu, ambayo siyo mambo ya *National Security,* hayo basi tuyaache kwa sababu taarifa nyingine inaweza ikatoka chini ya hicho kipengele cha *public interest.*

Mheshimiwa mwenyekiti, kwa hiyo, ukiangalia katika kipengele kingine cha (a), (b), (c), (d) na mengineyo, unaona kwamba kuna taarifa ambazo zinaweza zikatoka ambazo zinaweza zisiguse moja kwa moja usalama wa Taifa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hiyo adhabu ibaki kwa yale maeneo tu ambayo yanazungumzia mambo ya *National Security.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna kipengele cha 16 ambacho kinazungumzia; *"The information holder may be defer the provision of access to information until the happening of a particular event including the taking of some action required by law or some administrative action or until the expiration of a specified time, what is reasonable to do so in the public interest or having regard to normal and proper administration practices."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuangalia hiki kifungu katika hii *section* ya 16, kitu ambacho kinaonekana hapa ni kwamba kwa hiki kifungu maana yake ni kwamba taarifa zozote zile hazitaweza kupatikana kwa sababu taasisi husika inaweza ikaamua kunyima zile taarifa kwa kisingizio cha *public interest,* lakini hii *public interest* tunai-*define* kwa muktadha upi ili angalau tuhakikishe wananchi hawawezi wakanyimwa taarifa?

Mhesimiwa Mwenyekiti, tukiiacha kama hivi na tukaipitisha, sheria hii na hii *section* ya 16 tukaiacha kama ilivyo, maana yake ni kwamba tunasema kwamba sheria tumeandika kama sheria ambayo inaruhusu mambo ya *transparency,* lakini kimsingi ni kwamba tunavunja. Tunatambua ya kwamba mambo ya uwazi na uwajibikaji ni sehemu ya msingi katika demokrasia na ni mambo muhimu pia katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika hiki kipengele cha 16, kama hatutaweza kukifanyia kazi, maana yake ni kwamba tutakuwa tumetimiza matakwa ya Kimataifa ya kututaka Tanzania pia tupitishe sheria hii ambayo inahusiana na mambo ya utoaji wa taarifa, lakini kama nchi hatutaweza kutekeleza haki ya Kikatiba ya wananchi katika kuhakikisha kwamba wanapata sheria. Kwa hiyo, naomba tu nitoe ushauri kwa Serikali ili kuweza kuona namna gani hiki kitu kinaweza kikaangaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ni vyema tukafahamu ndani ya hili Bunge kwamba vyama vya siasa au upinzani kwa ujumla wake tusiuchukulie tu kwamba ni chama mbadala ambacho kiko tayari kusubiria nafasi ya kuweza kutawala, lakini tuchukulie kwamba ni sehemu pia ya kuwa wawajibishaji ndani ya nchi hii. Kwa hiyo, kama tunataka uwajibishwaji uweze kuwepo ndani ya nchi hii, lazima pia masuala ya uwazi yaweze kuwepo. Tunavyopitisha hii sheria tuangalie hicho kipengele, lakini pia tuangalie masuala mengine ambayo kama Serikali yamekuwa yakifungwa katika hilo suala zima la uwajibishwaji na upatikanaji wa taarifa, hasa kwa kuzingatia kwamba tulivyokuwa tunaanza hili Bunge, Serikali ilitangaza kuondoa Bunge la moja kwa moja la wananchi kutizama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba tumeifunga haki hiyo, leo tunapitisha hii sheria ambayo hatujui kiukweli kama hiki kipengele cha 16 kitabaki kama wananchi wataweza kupata hata hizi taarifa ambazo zimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapopata taarifa maana yake ni kwamba uweze kuwajibisha ofisi husika, maana yake ni kwamba uweze kupata majibu kutoka Serikalini. Nina imani kwamba vyama vya upinzani vina wajibu huo na hivyo Sheria ya Vyama vya Siasa naomba pia Serikali, viongozi walioko hapa, Mawaziri, waweze kumshauri Mheshimiwa Rais vyema kwamba ni bora kutii sheria za nchi zilizopo kwa sababu zimetungwa na Bunge hili. Kama tunaona ya

kwamba sheria hazifai, basi ni vizuri pia Serikali ikaleta marekebisho ya hizo Sheria za Vyama vya Siasa ili tuweze kuziangalia na kuzibadilisha na kuweza kuondoa watu kufanya mikutano ya hadhara katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mlinga ametoa ushauri, tunamchukulia ni mtu wa masihara, lakini kuna vitu alivyoviongea vya msingi. Kwa hiyo, tuombe pia Serikali iweze kumshauri Mheshimiwa Rais kuweza kuitii Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo iliyomchagua, ndiyo iliyomweka madarakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Mwalimu Nyerere mwenyewe aliweza kutamka katika hotuba yake akiwahutubia wananchi wa Tanzania kwamba Watanzania wasiruhusu kwa gharama yoyote ile mtu atakayeongoza kutoka kichwani mwake, lakini tuweze kuheshimu viongozi walioapa kwa Katiba na walio tayari kuilinda Katiba na wananchi wote tuweze kuwataka viongozi wetu kuweza kusimamia Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo siyo maneno yangu, ni maneno ya mtangulizi wetu Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere, ambaye anaheshimika na kila mmoja wetu. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako, tunaendelea. Mheshimiwa John Heche.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii uliyonipa nami niweze kuchangia kwenye muswada huu wa upatikanaji wa taarifa. Sasa kumekuwa na *contradiction* kubwa sana hapa, wengine wanasema Muswada wa Upatikanaji wa Habari, wengine Muswada wa Upatikanaji wa Taarifa. Ni kwa sababu mambo haya yalivyokuja yalikuja kinyumenyume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baadaye tutamhitaji Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe atuambie ni nini hasa ambacho walikusudia kuleta kwa sababu mwanzoni hata kwenye *Order Paper* ilivyoonekana ni tofauti na tunavyoijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nchi ni yetu sote. Wakati fulani kuna mambo ya msingi yanaletwa hapa, lakini watu wakitaka kuyajadili wanakwekwa na watu wengine baadaye wa kujibu vijembe, wanatoa vijembe upande wa pili bila kusikiliza kile watu wengine tunachokisema. Hata hapa tunajua kwamba kuna watu wameandaliwa, baadaye watachomekwa tu ili waje kushambulia yale tunayozungumza. Mimi sijali, nataka nizungumze na nishauri. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ikitolewa ndiyo inasababisha upatikanaji wa habari. Sasa taarifa ikiwa imetolewa, ikienda kwa *public* inakuwa habari.

Sasa huu Muswada wa upatikanaji wa taarifa ambao mwisho itakuwa habari umekuja wakati ambapo Taifa letu lipo kwenye majaribu makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupo kwenye wakati ambao tunajadili Muswada huu ambao kuna mtu mmoja, tunapokuja hapa tunapitisha bajeti yeye anakwenda anapitisha yake huko mtaani. Kama jana mliangalia vyombo vya habari vingi vilionesha, Mheshimiwa Rais alikuwa pale Magomeni, anasema atatoa shilingi bilioni kumi kujenga nyumba pale ambazo hatukupitisha kwenye bajeti. Kwa hiyo, hii ni *test* kubwa sana kwa sheria zetu. Unakuja wakati ambao sheria inaonekana siyo muhimu kwa Taifa hili. Muswada huu unakuja wakati ambao tunajadili mambo hapa, tunayapitisha yanaenda yanapindishwa huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tupo katika wakati ambao nafikiri na wananchi wenzangu wafuatilie haya. Je, kuna sababu zozote za Bunge hili kuwa linakaa hapa katika kipindi kama hiki au vipindi hata vya bajeti likatumia mabilioni ya pesa za Watanzania tukajadili jambo ambalo tunajua hatutalifanyia kazi? *At least* kwenye hii kwa sababu ina vipengele vingi vya kukandamiza, najua hii mnaweza kuifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo yupo Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, mwanasheria nguli, yupo Mwanasheria wa Serikali hapa, sheria zinapindishwa; watu wamezuiliwa kufanya mikutano kinyume cha sheria; Mwanasheria Mkuu wa Serikali yupo, kaka yangu Masaju tena anatoka Mkoa wa Mara. Sasa watu wa Mkoa wa Mara sisi huwa hatuogopi kusema ukweli na kushauri pale panapostahili. Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe yupo, mwanasheria nguli, lakini wote hao wanapiga makofi tu; wanampigia mtu mmoja makofi ambaye anavunja sheria hizi. Sasa ndiyo najiuliza, hivi kuna sababu gani ya kukaa hapa, tukatumia pesa nyingi kujadili mambo ambayo tunajua mwisho wa siku hatutayafanyia kazi kama hii sheria? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi kwenye huu muswada. Ukija kwenye kipengele cha 6(6) wamezungumza wenzangu; "mtu yeyote atakayetoa taarifa iliyozuiliwa kinyume cha mamlaka ya umma kisheria hii, atatenda kosa na endapo atatiwa hatiani atatumikia kifungo cha miaka 15 au 20." Yaani mtu ametoa taarifa ambayo inakwenda kuwa habari kwa wananchi na Katiba hii Ibara ya 18(c) imetamka kabisa kwamba wananchi wana haki ya kupata habari, mnamfunga miaka 20 Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, huyu mtu ameua mpaka mumfunge miaka yote hiyo? Yaani kwa kutoa taarifa tu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkisema taarifa za Usalama wa Taifa, taarifa za Majeshi; hizo sisi hatuna tatizo nazo; lakini taarifa, leo hata Mtendaji wa Kijiji akizuia taarifa sisi tukaitoa, kwa hiyo tufungwe miaka 20. Sasa nafikiri hii siyo sahihi.Ni lazima unapokuja Dkt. Mwakyembe uoneshe Udaktari wako hapa.

Usiunde tu watu nyumanyuma kuja kujibu hapa vijembe. Rekodi hizi zitabaki kwenye vitabu vya Bunge hili na watu wengine watakuja wasome wakati sisi hatupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele cha 19(3) unasema mtu yeyote ambaye hajaridhishwa na uamuzi wa Mkuu wa Taasisi uliofanywa, yaani ya kunyimwa taarifa, hajaridhishwa. Mimi nimekwenda nimenyimwa taarifa na Katibu Mkuu wako, sijaridhika, nikate rufaa kwako, yaani hii ni sawa na ile waswahili wanasema kesi ya ngedere unampelekea nyani. Hakuna kitakachopatikana hapa. Kwa hiyo, hivi vitu ni lazima kama kunatakiwa kuwepo na *checks and balances* muweke vyombo vingine ambavyo ni huru viweze kuwahoji au kuwalazimisha ninyi mtoe taarifa hizi ambazo zina manufaa ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unataka wewe mtu wa chini yako amekunyima taarifa na katika kipindi hiki ambacho nyie ni waoga vibaya sana, akishasema kule hata kama mnajua imevunjwa Katiba mpo kimya!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimwona pale kaka yangu Mheshimiwa Masaju na amekuja hapa alivyokuwa anahangaika Mwanasheria mzima kutetea uovu anashindwa; wanahabari wanambana hivi anasema hivi; aibu tupu, kwa sababu tu sheria zipo lakini hamtaki kuzifuata sheria hizi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona siyo sawa kwamba mtu wa chini ameshindwa, tukate rufaa kwako sijui na kwa mtu wa juu yake, hii naona siyo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 21 kinasema eti mmiliki wa taarifa ambaye maombi ya kupata taarifa yatatumwa kwake anaweza kutozwa ada iliyowekwa kwa ajili ya kutoa hiyo taarifa. Yaani kweli Katiba inasema ni haki ya mwananchi kupata habari na taarifa kwa mambo muhimu yanayohusu nchi yake, leo mnatuambia mtuuzie taarifa, yaani mnataka kweli kabisa Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe umeweka hapa kwamba taarifa inunuliwe, yaani vyombo vya habari vinataka taarifa za Serikali wawatangazie ninyi wananchi wajue mnachofanya, mnataka eti wanunue kutoka kwenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kwa nini tunatengeneza vitu vya aina hii? Mimi huwa nakaa najiuliza na wakati mwingine mnatunga haya mambo kama mnatukomoa sisi; lakini waangalieni wenzenu akina Basil Pesambili Mramba na wenzake, walikuwa Wabunge humu na Mawaziri tena waliokuwa wanaheshimika. Sasa hivi wananyea ndoo. Akina Harry Kitilya walikuwa watu wakubwa kwenye nchi hii, lakini wako mle ndani sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mnapotunga hivi vitu kama mnafikiria kukomoa watu, muwe mnawaza pia kwamba ipo siku kama historia haitawahukumu nyie wenyewe, watoto wenu hawatakuwa na nafasi hizo mlizonazo au wajukuu zenu hawatapata nafasi hizo mlizonazo, watakutana na mambo haya ya ajabu mliyoyaweka kwa ajili ya kubana watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nipo hapa kushauri na tunashauri kwa nia njema. Mmwambie hata Mheshimiwa Rais na ninyi wote humu mnajua na mnalalamika. Hatuwezi kuwa na Rais ambaye akienda huku, watu tunashika vichwa, leo atasema nini? Yaani hatuelewi! Anakuwa Zanzibar anasema watu watafia kwenye madimbwi ya maji. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Utaratibu. Kuhusu utaratibu!

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu, Mheshimiwa Heche.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa…

**MWENYEKITI:** Keti, keti, keti!

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu, kifungu gani?

**MBUNGE FULANI:** Kanuni ya 64(1)(a) mpaka (g) naisoma pamoja na Kanuni ya 68(7) mpaka (8) lakini naisoma pamoja na Kanuni ya 86(8).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba umwelekeze Mheshimiwa Mbunge aliemaliza kusema hapa…

**MBUNGE FULANI:** Hajamaliza.

**MBUNGE FULANI:** Au anayeendelea kusema, aseme hoja sawa na muktadha unaohusu Muswada huu na asiendelee kupotosha kwa kutumia vibaya jina la Rais na kufanya ushawishi usioeleweka. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kusema kila mara jambo hili, tunainuka na kukwambia; tunaomba utusaidie katika kusimamia kanuni hizi, maana hawa wenzetu inaonesha kanuni hizi hawasomi vizuri na kuzielewa. Bila kufanya hivyo, utaratibu wa kuvunjwa kwa kanuni utaendelea na wengine wataedelea kuvunja na itakuwa hatari humu katika Bunge lako. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nawasihi sana, pande zote; hili suala la zomea zomea halikujengei heshima Bunge hili. Nawaombeni sana na upande huu wa kushoto kwangu hamuwezi mkaanza majadiliano na Mbunge ambaye ana haki ya kusimama na kuomba suala la utaratibu; tuheshimu kanuni hizi. Nimeombwa utaratibu, Mheshimiwa John Heche alipokuwa anachangia nimemsikia ametaja tu jina la Mheshimiwa Rais mara moja. Ameendelea kusema maneno mengine mtu huyo; mimi nimeshindwa kuelewa huyo mtu ni nani? *(Makofi)*

Hata hivyo, kwa mtu yeyote anayefuatilia, nadhani ndiyo hoja ya Mheshimiwa, alieenda Magomeni alikuwa ni nani? Ni Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sipendi tufikishwe huko. Kanuni ya 64 ya makatazo hiyo, kumtaja Mheshimiwa Rais kwa dhihaka na kwa njia unayofikiria. Nawaombeni sana na ninasema Mheshimiwa John Heche, wewe endelea kuchangia, lakini kama unataka kumtaja Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, mtaje kwa heshima yake na katika muktadha unaotaka kuelezea. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaona *maturity* yako, nakushukuru sana, kwa sababu watu wengine wako humu wanafikiri tukimtaja Mheshimiwa Rais tunamchukia. Hatumchukii, sasa namtaja kwa Utukufu wake, Mheshimiwa Mtukufu Rais. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema, akienda sehemu hatujui ataongea nini; juzi, Mheshimiwa Ummy alikuwa hapa anakanusha taarifa, amesema watu wazae tu. Mheshimiwa Ummy amekanusha; sasa hilo lilikuwa linajulikana ataongea nini? Mtukufu Rais amesema, machinga waingie popote, Mheshimiwa Simbachawene yule pale, akakanusha juzi tu. Labda watu hawa hawana kumbukumbu na hawafuatilii. Ndiyo maana tunasema wala siyo kwa nia ya kurushiana vijembe wala kudhihaki mtu. Tunasema Taifa hili ni lazima tuliweke kwenye utaratibu wa kisheria na mambo yote yawe kwenye *chain* ya sheria na Katiba ili kila mtu ajue kwamba nikivuka mipaka hii, awe Mheshimiwa Rais, awe Mtukufu Rais kwa sababu nikisema Rais napigiwa kelele; awe nani, ajue nikivuka mipaka hii, sheria za nchi yetu hazitakubali, Katiba ya nchi yangu haitakubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhara yake, kuacha mambo yanajiendea, ndiyo maana unaona hata Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mheshimiwa Makonda anatoa amri eti Mikoa yote tarehe moja ipande miti, yaani Makonda naye ni Rais kwenye nchi hii! Uropokaji wa ajabu! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna sheria zinaeleza tuendesheje nchi; mtu anakaa Dar es Salaam kwa sababu amesifiwa mara mbili, amejiona na yeye ni kila kitu, anatoa amri; tarehe 1 mwezi Oktoba watu wote wapande miti nchi

nzima. Na yeye anatembea na Wanajeshi, ana Polisi. Sasa tukisema haya hatusemi kwa nia mbaya, tunasema kwamba tunakaa hapa tunatunga sheria na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, mnaaibisha *professional* zenu, yaani mnatia aibu! Hii nchi inatia aibu kweli kweli! Wasomi wa Vyuo Vikuu hawazungumzi, wako kimya… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Halima Mdee, atafuatiwa na Mheshimiwa Vuma Augustine na tutamalizia na Mheshimiwa Lusinde.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee. Mheshimiwa Augustine Vuma Holle.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kukushukuru sana kwa nafasi hii nzuri ili na mimi niweze kuchangia Muswada huu wa upatikanaji wa taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona ndugu yangu Heche alivyosikia jina langu limetajwa, baada yake alianza kutokwa na povu kama nimeandaliwa kwa ajili ya kumjibu. Niseme tu, mimi ni Mkristo safi, nitaendelea kusema ukweli, maana yake najua ukweli kwa mujibu wa dini yangu humweka mtu huru siku zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais, alivyokuja kwenye kampeni Jimboni kwangu pale Kasulu aliahidi kwamba atafuta vumbi Wilayani Kasulu na juzi nimeenda kule kwenye ziara yangu ya kuwashukuru wananchi, nimekuta ujenzi wa barabara upo kwa kasi ya ajabu. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Rais. Nasema hayo kwa sababu wananchi waliniambia niseme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, napenda kuishukuru Wizara ya Katiba na Sheria kwa Muswada huu. Muswada huu nimeupitia vizuri kuanzia kifungu cha kwanza mpaka kifungu cha mwisho cha 24. Nimeusoma vizuri lakini pia nimepata nafasi ya kupitia hii *schedule of amendment to be moved* na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba mwandishi mmoja anaitwa Malisa, mwaka 2004 aliwahi kusema katika chapisho lake liitwalo *Freedom of Information and Access to the Government Record Rose Around the World,* alisema; "*Access to information is the notion that public can obtain information*

*and the possession of the state and in some countries private entities are information for the purpose of being informed about the activities of the state.*"

Kwa tafsiri isiyo rasmi kwamba upatikanaji wa taarifa ni dhana ya kuwa Umma unaweza kupata taarifa zilizo chini ya himaya ya Serikali na katika baadhi ya nchi taasisi ya mtu binafsi kwa madhumuni… *(KichekoMakofi)*

**MBUNGE FULANI:** Endelea tu, kwa madhumuni maalum.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Kwa madhumuni maalum, hiyo nimesema siyo rasmi.

Nataka niseme kwamba ni wakati sahihi kabisa Muswada huu umekuja, wazungu wanasema, *information is power*. Taarifa ni zao la habari, kama ikitolewa visivyo sahihi huzaa habari isiyo sahihi. Kama Taifa hatuna utaratibu, hatuna sheria ya upatikanji wa taarifa, maana yake inaweza ikatupelekea katika mazingira ambayo kila mtu hawezi kuamini. Maana yake taarifa hizi ambazo siyo sahihi zimesababisha baadhi ya Mataifa kuingia katika vita vya wenyewe kwa wenyewe; vinapelekea baadhi ya usalama wa nchi mbalimbali duniani kupotea na kujikuta wakiwa katika mapigano na umwagaji wa damu. Kwahiyo, kuwa na sheria ya upatikanaji wa taarifa ni kitu sahihi kabisa na mimi naunga mkono Mheshimiwa Waziri mswada huu umekuja katika wakati sahihi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekaa nikafuatilia vizuri sana michango ya sehemu zote mbili; wapinzani na wengine lakini nimeona wengi tu hapa hasa ndugu zangu wa Upinzani wanarukia tu, hawajapata nafasi ya kuupitia vizuri muswada huu na wala hawajapata nafasi ya kupitia hii *schedule of amendment*. Kwa sababu naona ndugu yangu Mheshimiwa Heche pale na wengine waliosimama wakasema kwamba adhabu ni kali sana; lakini nikisoma kwenye *schedule of amendment* kipengele (c), ukija pale (a), (b), (c); kipengele cha (c) tena imeandikwa "*by deleting sub clause and substituting for it the following;* namba 6 (a):-

"*Any person discloses exempted information other than information related to the national security commit an offence and shall on conviction be liable to imprisonment for the term not less than three years and not exceeding five years.*" *(Kicheko/Makofi)*

Sasa nyie mnavyosema kwamba miaka 10 mpaka 15, maana yake mmerukia tu, mnataka kulidanganya Taifa; mmerukia bila kuangalia hii *schedule of amendment*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, wamesema hata hapa kwamba sheria hii ipo Bara peke yake. Labda niseme kwamba sheria hii Uingereza ilitungwa mwaka 2002. Uingereza kule ilivyotungwa Scotland wao walikuwa hawakuitumia, kama sisi tunavyofanya hivi, wamekuja kuiingiza mwaka 2002. Kwa hiyo, tupo sahihi, tupitishe sheria hii bila mizengwe yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine wamekuja hapa wakasema kwamba hii sheria iondoke, yaani hawataki kufanya chochote. Sasa mimi nadhani tumekuja hapa tunalipwa na Watanzania. Tunalipwa mamilioni ya Watanzania kwa siku ili tupate nafasi ya kutunga sheria kama kazi yetu ya Kikatiba kama Wabunge. Sasa muswada umekuja hapa, badala tutoe michango ya kuuboresha na hatimaye iwe sheria nzuri na kurekebisha Tanzania, wewe unakuja unasema kwamba iondoke, yaani maana yake upokee hela tu pasipo kufanya kazi yoyote; hii ni akili kweli jamani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba ifike mahali tuwe wazalendo wa kutosha, tusizungumze tu hapa kwa sababu ya kutaka umaarufu, tusizungumze hapa tukaacha maslahi mapana ya nchi pembeni. Amekuja hapa ndugu yangu, mtani wangu, Mheshimiwa Lema jana kasema mshahara wa dhambi siku zote ni mauti, na mimi nasema, hayo ni maneno ya Kanisani, sisi hapa Bungeni tunasema kwamba mshahara wa kutoheshimu mamlaka ni kibano. Kwa mfano, umeambiwa ulipe kodi, halafu unakaa haulipi kodi, vyombo vyako tutatoa nje hata kama ni kiongozi mkubwa katika nchi hii. Umeambiwa Kanuni zinasema kwamba tutii Kiti hapa Bungeni, wewe hauachi kutii Kiti hapa Bungeni, wewe utatolewa hata kama ukifunga *bandage* mdomoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilindie muda wangu, naomba unilindie muda wangu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Aaaah! Achangie Muswada jamaa basi!

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilindie muda wangu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu Bungeni. Endelea Mheshimiwa.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nasema hapa kwa sababu uzalendo wa watu, hasa ndugu zetu hawa umeondoka. Wamekuwa wakijaribu kutanguliza maslahi yao mbele pasi kutanguliza maslahi mapana ya Taifa. Wamekuja hapa Bunge lililopita, wamefungwa midomo na

kiongozi wao wakaondoka, walivyoondoka kule wameshindwa kuona udikteta wa kiongozi wao…*(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Eeehe! *(Kicheko)*

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilindie muda wangu, tafadhali! Wameshindwa kuona udikteta wa kiongozi wao… *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Eeehe! *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** …wanakuja kutuambia kwamba Mheshimiwa Rais…

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafadhali!

**MBUNGE FULANI:** Endelea!

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilindie muda wangu, tafadhali.

**MHE. MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

**MWENYEKITI:** Hebu naomba ukae kidogo Mheshimiwa.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza tuna tatizo, watu wa *Hansard* wanasema wanashindwa kuyapata vizuri maneno ya Mheshimiwa anayechangia kwa sababu ya hayo mnayosema kama kibwagizo. Nawasihi basi, tumruhusu Mheshimiwa Mbunge amalize muda wake kama yeye alivyokuwa ametulia wakati baadhi yenu mnachangia.

**MBUNGE FULANI:** Achangie mada.

**MWENYEKITI:** Naruda tena, inapofika kwa wengine tunawavumilia, mimi nawavumilia wanakwenda kidogo nje ya reli; inapofika kwenu, mnakuwa wagumu. Sasa nasema hivi, tumpe heshima Mheshimiwa Mbunge achangie tuendelee na shughuli zetu. Mheshimiwa malizia. *(Makofi)*

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kuweka vizuri hali ya Bungeni. Niseme tu kwamba Muswada huu umekuja wakati sahihi na wote tuungane kwenye kuupitisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Ahsante sana kwa hitimisho lako. Mheshimiwa Lusinde. *(Kicheko)*

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda nimshukuru Mungu kwa kunijalia zawadi ya uhai na afya njema ili na mimi niweze kusema machache juu ya mchango wangu kuhusu Muswada wa Upatikanaji wa Taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichukue fursa hii kuipongeza sana Serikali kwa kuuleta Muswada huu. Kabla ya Muswada huu, suala la kutoa taarifa halikuwa la lazima. Mtu angetaka kutoa anatoa; hataki, anakaa hivyo hivyo; lakini leo kwenye Muswada huu Afisa analazimishwa kutoa taarifa kama sheria tutakavyoipitisha. Kwa hiyo, tunaipongeza sana Serikali kwa uamuzi wake wa kuleta Muswada huu Bungeni ili watu wasitafute habari kwa kuomba, wasitafute habari kwa hisani, bali wazitafute habari kisheria. Hili ni jambo zuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi yanazungumzwa humu ndani kwamba Katiba inatoa haki, ndugu zangu, Waheshimiwa Wabunge, Katiba haifanyi kazi ya utendaji wanaotenda ni watu sio Katiba yenyewe ndiyo inayotekeleza. Leo Katiba inasema kila Mtanzania ana haki ya kuishi popote, lakini Rais au Waziri mwenye dhamana ya makazi ana uwezo wa kusema watu watoke hapa kuna mafuriko wakati Katiba haisemi hivyo. Kwa hiyo, tusiishi kama tumejifungia; maana yake kila mtu hapa anasema Katiba, Katiba. Katiba haitekelezi, Katiba ni sheria mama ya nchi. Zinatungwa sheria kutafsiri Katiba na ndiyo kazi ambayo tunataka kufanya hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasikitika sana ninapoona watu wanakimbilia kujificha kwenye Katiba. Katiba haitekelezi, wanatekeleza watu na hao watu wanaweza kutekeleza kitu ambacho kiko kwenye Katiba. Leo hii hapa tuna jengo la Bunge, lakini pakipita mafuriko litahama, hata kama imeandikwa hivyo kwenye sheria kwamba jengo la Bunge liwe hapa. Kwa hiyo, watu waelewe tu kwamba hapa tunatunga Sheria ya Upatikanaji wa Taarifa na hakuna sehemu tunapokwenda kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakuna sehemu tunapokwenda kinyume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona Waheshimiwa Wabunge wanajaribu kuwatisha baadhi ya Mawaziri na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, hivi kumbe ninyi mngeshinda nchi mngetunga sheria ambazo zingewa-*favour* akina Lowassa? Sheria ni msumeno, inatakiwa ikate kote kote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kama kuna mtu alikuwa Waziri akaivunja sheria amefungwa ni sawasawa. Hatutungi sheria kwa ajili ya wananchi tu; tunatunga sheria kwa ajili ya Watanzania wote na sisi wenyewe. Sasa naona kuna mtu anasimama anasema, shauri yenu, akina Mramba walikuwa hapo, leo wamefungwa. Hata ninyi mtafungwa, hata sisi Wabunge tutafungwa, hata mimi nitafungwa. Sheria inataka kila mtu aitekeleze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbe wenzetu wangepata Serikali hawa, wangetunga sheria za kukandamiza wananchi, wao zisingewahusu. Ndiyo maana mnaona kila wakisimama hapa, wanajaribu kukutisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wanajaribu kukwambia eti leo hii Lowassa anapigwa mabomu, angepigwa mabomu angekuepo? Amepigwa gesi za kutolea machozi, siyo bomu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusidanganyane hapa! Watu wanaowazungumza, hata kukimbia hatua tano hawawezi, apigwe bomu ataweza kuvumilia yule? Acheni mambo ya kudanganya kwenye Bunge hapa. Tusidanganyane! Watanzania lazima tuelewe, tunapotunga sheria na Wabunge tuelewe, hatuwatungii watu, tunajitungia na sisi wenyewe, hili ndiyo nataka lieleweke.

Kwa hiyo, isije ikafikiriwa kwamba kuna kundi tu tunalolilenga, hapana. Kumbe wenzetu wametupongeza kwamba Serikali ya CCM inatenda haki, inatunga sheria zinazowalamba mpaka Mawaziri, wametupongeza. Hizi tuzichukulie kama pongezi kabisa, kwa sababu leo hii kila kitu wanataka kiandikwe kwenye Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kuna Chama kimoja, Mwenyekiti wao anadaiwa, walikutana kikao kujadili deni, kwenye Katiba yao imeandiwa wapi? Imeandikwa wapi? Wapi kwenye Katiba yao imeandikwa Mwenyekiti akidaiwa mtaacha shughuli zote mkutane kwenye kikao kujadili deni? Kwa hiyo, kuna mambo mengine ya utekelezaji yanafanyika nje ya hizo Katiba kwa sababu ya hali halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa namna unavyoliendesha Bunge kisayansi na linavyokwenda. Nataka niseme leo, tajiri hanuniwi! Ukimnunia tajiri, inakula kwako. Kwa hiyo, hizi siku mbili mnazowaona watu wana uhuru fulani wanazungumza humu ndani, ndiyo uhuru umepatikana hivyo. Kwa hiyo, tuendelee kuwavumilia, tutakwenda nao vizuri tu hawa wa kwetu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya adhabu; hakuna sheria inayoweza kutekelezwa kama haitoi adhabu. Haiwezekani. Sheria yoyote ili itekelezwe, ni lazima iwe na adhabu. Kwa hiyo, kama kwenye sheria hii kuna mtu ataikosea sheria, atakwenda jela miaka mitano, iko sawa. Kumbe tutatungaje sheria bila kuweka adhabu? Hiyo sheria itatekelezwaje sasa? Sheria ili itekelezwe ni lazima iwe na upande wa kuadhibu ili watu tuogope; ili watu waogope. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusimama hapa na kusema upatikanaji wa habari ni haki ya Kikatiba. Kweli ni haki ya Kikatiba, lakini kwa mfano, kama mtu nyumbani kwake hajanunua redio, hana betri, anapataje habari? Hawa watu

wa ajabu sana! Ni haki kweli, lakini kuna haki ambazo ni lazima uzigharamie. Leo upatikanaji wa habari, huna *TV,* huna umeme unapataje hiyo habari? Wenzetu wanalazimisha, ooh, ni haki ya Kikatiba, haki ya Kikatiba, sasa Serikali igawe *TV* nchi nzima, Serikali igawe redio nchi nzima, igawe betri nchi nzima? Kwa hiyo, kuna vipande kwa vipande. Kuna haki na kuna wajibu. Uko wajibu! Ukitaka habari, ni lazima uwe na wajibu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tusitake kutumia fursa hii kudanganya. Zipo haki zimetajwa kwenye Katiba, lakini uko wajibu. Kila Mtanzania ana haki ya kuishi, lakini ana wajibu wa kulima ili apate chakula kitakachomfanya aishi. Sasa kama hafanyi kazi, hapiki chakula, anaishije? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tusidanganye watu kwa kutumia kisingizio cha Katiba, inatoa haki, Katiba inaminywa. Katiba inatoa haki na Katiba hiyo hiyo inatoa fursa. Mwanasheria Mkuu wa Serikali, watu wakikusonga sana, jua uko sahihi. Kwa hiyo, wewe endelea kufanya kazi zako, ndiyo maana unaona wanasimama wanakushutumu. Mawaziri endeleeni kupiga kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kila mtu akisimama hapa, mnataka kupotosha watu kwamba Mheshimiwa Rais amekataza kufanya mikutano!

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo!

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Hakuna mahali Mheshimiwa Rais amekataza kufanya mikutano. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila Mbunge anatakwa kufanya Mkutano kwenye Jimbo lake. Kilichokatazwa ni kuendelea na kampeni kwa tabia ambayo tulikuwa tumezoea. Uchaguzi unaisha, watu wanaendelea na kampeni miaka mitano, hiyo ndiyo haikubaliki. Mbunge gani, wa Jimbo gani, kaenda kufanya mkutano kwenye Jimbo lake akakatazwa? Nani? Hakuna mahali. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa walikuwa wameshazoea. Watanzania kwa sasa hivi hawana nafasi ya kupokea tena maneno, wanataka kupokea maendeleo, siyo maneno. Maneno mengi yameshazungumzwa, maneno mengi yameshasemwa, nyimbo nyingi zimeimbwa mpaka nyingine zimezuiwa kuimbwa, sasa hivi ni wakati wa kufanya kazi, siyo wakati wa maneno kama walivyokuwa wamezoea hawa.

Kwa hiyo, mkisikia wanalaumu, ooh, Mheshimiwa Rais ametukataza kufanya mkutano; wewe Jimbo lako la Tarime, nani kakukataza kufanya mkutano? Nenda kahutubie wananchi wako waliokuchagua, isipokuwa kutoka

Tarime unafunga safari kwenda Mpwapwa; Mpwapwa wana kiongozi wao waliomchagua, acheni afanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho leo nataka nikiseme, kauli ya Mheshimiwa Rais imewaumiza baadhi ya watu. Walikuwa wanatumia ruzuku vibaya, wakati huo wanajifanya kuna operesheni sijui nini; sijui operesheni ndorobo; sijui operesheni nini, kumbe wanakula hela za wananchi kwa kutumia mgongo wa operesheni. Sasa hiyo hakuna. Hakuna nafasi hiyo, kila Mbunge afanye mikutano kwenye Jimbo lake, ahamasishe maendeleo, shughuli za maendeleo zifanikiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuja kumsingizia Mheshimiwa Rais kwamba kazuia mikutano, siyo sahihi, lazima tuliweke vizuri jambo hili. Ulaji wa ruzuku kupitia vyama vya siasa umezuiwa, ndiyo maana mnaona kelele. Maana ilikuwa saa hizi unaona maspika yamefungwa, bendera zimefungwa; wapi? Mtera, kufanya nini? Mtera kuna Mbunge wake, mnakwenda kufanya nini? Miezi mitatu imepita tumefanya uchaguzi, leo hii tuendelee tena kuwajaza watu maneno? *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE :** Ukisikia kelele, ujue tayari! *(Kicheko/Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ahsante sana.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE :** Mimi hata mkipi…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lusinde, muda umekwisha.

**MBUNGE FULANI:** Aaaaaaaah!

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Serikali imeleta waka…

**MWENYEKITI:** Ahsante. Muda umekwisha. Muda wako umekwisha. Huyo ndio alikuwa mchangiaji wetu wa mwisho. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko hapa. Nipo! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hebu kaa chini.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Nimesharudi.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MBUNGE FULANI:** Kachelewa makusudi. Kaa chini!

**MBUNGE FULANI:** *Zima mic!*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kaa chini.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, Mheshimiwa Lusinde ndio alikuwa mchangiaji wetu wa mwisho. Nilimwita Mheshimiwa Halima Mdee. Siwezi kurudi nyuma, ndiyo uamuzi wangu. *(Kicheko/Makofi)*

Sasa kabla sijamwita mtoa hoja, nitakuwa na wachangiaji wa kumsaidia Mheshimiwa Waziri, tukianza na Mheshimiwa Nape, dakika kumi; atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa dakika kumi; halafu na Mheshimiwa Possi kwa dakika kumi; halafu ataingia mtoa hoja kuhitimisha hoja yake. Karibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye muswada huu muhimu ambao umewasilishwa. Nianze kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza maandalizi mazuri ya muswada huu, ni katika miswada mizuri, umechukua muda mrefu, lakini umeandaliwa vizuri na kwa hakika umejumuisha mawazo na michango na maoni ya wadau wengi, ndiyo maana ni katika miswada bora kabisa. Nachukua nafasi hii kuipongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, nadhani amefanya vizuri sana kwa sababu Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe licha ya kuwa ni mwanasheria lakini ni mwanahabari, kwa hiyo, ameutendea haki muswada huu. Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, nakupongeza na kukushukuru sana kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu ukipewa tafsiri finyu unaleta matatizo katika mjadala. Wachangiaji wengi wamekuwa wakizungumza na pengine labda kwa bahati mbaya wanauchanganya Muswada huu wa Haki ya Kupata Taarifa na Muswada wa Huduma ya Vyombo vya Habari ambao kwa kweli ni miswada miwili tofauti.

Muswada huu wa Haki ya Kupata Taarifa uko chini ya Wizara ya Katiba na Sheria na upo Muswada wa Huduma za Vyombo vya Habari ambao uko chini ya Wizara ya Habari ambao utakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wengi wamekuwa wakichangia kama vile huu ndiyo Muswada wa Huduma za Vyombo vya Habari, ndiyo maana michango mingi imekwenda huko. Sasa ama ni kwa bahati mbaya au kwa makusudi au kwa kutosoma vizuri na kuelewa ndiyo maana michango imekwenda hivyo ilivyokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, muswada huu una mambo ambayo hayagusi moja kwa moja tasnia ya habari na haya ni ya muhimu sana na ndiyo maana tukiupa tafsiri inayofaa michango yetu itakwenda vizuri. Muswada huu moja ya eneo ambalo utaisaidia sana nchi yetu, muswada huu unatupeleka kwenye kuongeza uwajibikaji na hasa wa taasisi za umma na watumishi wake. Moja ya eneo la uwajibikaji ni kuhakikisha taarifa zinapatikana. Siyo kila taarifa inayozungumzwa na muswada huu inakwenda kutumiwa na vyombo vya habari, hapana. Muswada huu unazungumza haki ya mwananchi wa kawaida kupewa taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mwananchi ana haki ya kupata taarifa juu ya miradi ya maendeleo ya eneo lake. Kiongozi katika eneo, Mtendaji wa Kijiji, Diwani, Mbunge, muswada huu unamfanya Afisa wa Umma ambaye anatumikia umma awe na wajibu wa kutoa taarifa za miradi ya maendeleo ya eneo lake ambalo kwa kufanya hivi, itaongeza uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukijikita na kudhani taarifa hizi zinazozungumzwa hapa ni taarifa ambazo zimelenga vyombo vya habari peke yake, nadhani tunataka kuupotosha Umma na siyo sawa sawa. Sasa anayeupinga Muswada huu, maana yake anapinga uwajibikaji. Tafsiri rahisi kabisa! Wakati huo tunapiga kelele ya uwajibikaji, tunatunga sheria itakayotusaidia kuwajibika zaidi, watu wanasimama wanapinga sheria hiyo isitungwe, maana yake wanapinga uwajibikaji kuongezeka katika nchi yetu. Na mimi nadhani ni vizuri tukaliweka sawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii inakuwenda kuondoa urasimu. Moja ya tatizo kubwa ambalo limekuwa likizungumzwa kwa muda mrefu, ni urasimu wa upatikanaji wa taarifa mbalimbali zinazowahusu wananchi, za maendeleo yao; za namna Ofisi za Umma zinavyofanya kazi. Kwa muda mrefu imekuwa ni kama hiari hivi. Ukienda kwenye Ofisi ya Umma unaweza kupewa taarifa au kutopewa, bila kujali ni mwandishi wa habari au sio mwandishi wa habari. Mwananchi wa kawaida anakwenda mahali anauliza, hivi mradi huu gharama yake ni kiasi gani? Usipokuwa na sheria ya namna hii, yule mwenye ile habari ana uhuru wa kutoa au kutokutoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii inakotupeleka ni kwenye kumfanya huyu afisa awe na wajibu wa kuhakikisha anampa taarifa huyu mwananchi wa kawaida. Kwa hiyo, tukiangalia tukaipa tafsiri ya kwamba tumelenga vyombo vya habari peke yake, nadhani tunakwenda kwenye ufinyu sana wa kutafsiri muswada huu, ambapo siyo jambo sawa na hatuutendei haki muswada huu. Nategemea Bunge hili liutendee haki muswada huu, unakwenda kujenga jambo la maana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ni nyenzo muhimu ya maendeleo; iwe ya kisiasa, kiuchumi, kijamii, ndiyo maana muswada huu kwa kweli lengo lake ni kutupeleka huko. Sasa hivi hali ilivyo kabla ya hii sheria kupita, utoaji wa taarifa unategemea busara, unategemea utayari wa mtoaji na unategemea uelewa wa mtoaji na hili limekuwa tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali inaleta Bungeni Muswada tuupitishe ili tusitegemee busara tena, tusitegemee utashi na utayari wa mtu kutoa taarifa. Mtu anayesimama kuupinga maana yake anataka turudi kule ambako watu wote tumekuwa tukilalamikia. Kwa hiyo, nadhani la kwanza ni vizuri tukaupa muswada huu tafsiri pana inayostahili Muswada huu, vinginevyo tutakuwa hatuutendei haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili; wale ambao sasa wamekuwa wakiupotisha muswada, wakidhani unagusa tu tasnia ya habari, huu muswada, mimi ni Waziri wa Habari na nimeupitia vizuri huu muswada na tumezungumza na wadau wa habari. Nilikwenda Mwanza nikakutana na wanahabari nikawaambia, nipeni maeneo mnayodhani yanakwaza tasnia ya habari katika huu muswada, wakayaorodhesha, tukazungumza na Waziri na ninataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri, ameyazingatia maeneo karibu yote ambayo kwa kweli kwa namna moja ama nyingine yangekwaza tasnia ya habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini muswada huu utasaidia sana kukuza tasnia ya habari kwa sababu mtoa taarifa mkubwa katika nchi yetu ni Serikali na vyombo vyake. Sasa sheria hii inakwenda kuilazimisha Serikali, inakwenda kuvilazimisha vyombo vya umma viwe na lazima ya kutoa taarifa kuwapa wanahabari. Sasa kuna jambo gani kubwa tunaweza tukaitendea haki tasnia ya habari kama kuitengenezea ulazima wa wao kupewa taarifa? Sasa tukileta hapa, watu wanasema hii hapana, hii hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani liko tatizo la kiwango kikubwa sana cha kutoaminiana ambacho ndiyo kinatufikisha hapa, watu wanabaki wanatoa mapovu, bila kuangalia jambo hili linakwenda wapi, hii ni shida. Ukiwa na watu ambao wanadhani muda wote ni lazima kufanya harakati, hata wakati

ambapo mnataka kuzungumza mambo ya manufaa kwa nchi yenu wenzenu wanadhani mnafanya harakati. Hii ndiyo shida ambayo inatokea.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa watu wamezungumza, wanasema, aah, unajua siku hizi vyombo vya habari vinafungiwa hovyo na sasa wanatafsiri kwamba kama vile huu muswada unakwenda kumwongezea nguvu Waziri mhusika na wanasema Nape, kama vile Nape atadumu milele hapa. Nape yupo leo, kesho hayupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri, muda ndiyo huo. Unga mkono hoja. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa mara nyingine tena kuniwezesha na mimi niweze kushiriki katika mjadala huu. Pia nakushukuru kwa kuniruhusu na vilevile namshukuru sana Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe kwa kuleta muswada huu ikiwa ni kukidhi hitaji la Katiba kwenye Ibara ya 18(d) ambayo inatoa haki ya watu kupewa taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hakika muswada huu umeletwa na mtu ambaye hasa ndio anayestahili kuleta, kwa sababu kwa *background* yake, yeye ni mwanataaluma wa uandishi wa habari, lakini pia mwanasheria aliyebobea kwa kuleta muswada huu, ameangalia mambo yote. Ameangalia haki ya kupata hizo taarifa, lakini pia na wajibu wa huyo mtu anayetaka kutoa taarifa au kuzisambaza hizo taarifa. Ni kwa maana hii sasa unaona mantiki ile ya Ibara ya 6 katika muswada huu.

Mhehimiwa Mwenyekiti, ni kwamba katika *scheme* ya Katiba yetu ni haki na wajibu. Ukisoma Ibara ya 12 mpaka 28 ya Katiba, inaeleza juu ya haki na wajibu. Inaeleza juu ya haki na wajibu, Ibara ya 29 na ya 30. Kwa hiyo, hakuna kitu ambacho kimekiuka Katiba katika yale yaliyoorodheshwa katika Ibara ya 6 ya muswada. Mambo yote yale Usalama wa Taifa, siri, faragha, mambo yote yaliyowekwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kweli, mambo haya tayari yako katika sheria mbalimbali za nchi yetu. Utakuta katika Sheria ya *National Security Act*, utakuta katika Sheria ya *Whistle Blowers and Witness Protection Act*, utakuta katika sheria nyingi. Kitu ambacho tumefanya katika muswada huu, ni kuyaleta pamoja haya ambayo yamekwishatamkwa katika sheria hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitashangaa kama miongoni mwetu kwa kweli tukaanza kutilia mashaka mambo ambayo yameorodheshwa katika Ibara ya 6 ya muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambieni pia kwamba muswada huu pia haukusudii kuua upatikanaji wa habari kwa sababu Ibara ya 5(3) imeeleza vizuri kwamba muswada huu hauzuii kutungwa kwa sheria nyingine ile ambayo inaruhusu utoaji wa habari. Kwa hiyo, muswada huu haukusudii wala hata kuficha sijui mnaita ufusadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, tayari tumetunga sheria ya *Whistleblowers and Witness Protection Act* ambayo inatoa fursa kwamba hata vitendo vya uhalifu vitajwe, mambo ya ufisadi yatajwe; lakini tunayo sheria ya kuzuia na kupambana na rushwa imeeleza hayo mambo. Tumetunga Sheria ya *Tanzania Extractive Industry (Transparency and Accountability)*. Kwa hiyo, kusema kwamba tunatunga sheria hii kwamba hiyo itakuwa ni namna ya kuzuia upatikanaji wa habari, hapana. Ni namna ya ku-*enhance* zaidi upatikanaji wa habari lakini kwa namna ambayo tutafanya kwa kuzingatia maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia baadhi yetu tumezungumza Ibara ya 16, maslahi ya umma. Moja ya mambo mnayoweza kuyasema, haiwezekani kila kitu tuna-*define* kwamba ni maslahi ya umma, lakini ukieleza yale mambo yaliyotajwa yote katika Ibara ya 6 hayo ni sehemu ya maslahi ya umma na kipimo chake ni *public*. Ndiyo maana sasa mtu anayeona kwamba hakuna maslahi ya umma hapa, anaweza akaenda mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kusema kwamba siyo vyema kulaumu sana hapa kwamba kumekuwa na ukiukwaji wa Katiba. Ni nani amekiuka hii Katiba? Katiba yenyewe inamtaka Rais kusimamia na kutekeleza sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 36 ya Katiba hii inatutaka kila mmoja azingatie Katiba na Sheria ya nchi; na mtu ambaye anaona kwamba hiyo Sheria inavunjwa au Katiba aende mahakamani. Haiwezekani kwamba sasa mtu anayesimamia utekelezaji wa sheria aonekane kwamba yeye ndio anayevunja Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana wakati fulani nikiongea na umma niliuliza ni kifungu gani cha Katiba? Ni kifungu gani cha sheria kimekiukwa? Maana yake hapa wamezungumza, nimewasikia wanasema anavunja Katiba, anavunja Katiba. Waseme ni kifungu kipi cha Katiba *so far* kimekiukwa? Kwa hiyo, tuwe *responsible* tunapochangia ndani ya Bunge.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kwa hiyo, tukupe taarifa au?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilifikiri kwamba ni vizuri…

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Taarifa!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifikiri kwamba ni vizuri tukawa makini tunapochangia kwenye masuala haya.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Taarifa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipata fursa hapa, nimewasikiliza Waheshimiwa Wabunge wakizungumza kwamba muswada huu ambao utatumika Bara peke yake lakini umechangiwa na watu kutoka Zanzibar.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Taarifa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba yetu, uraia ni jambo la Muungano. Bunge hili linatoa haki kwa kila Mbunge, haijalishi anatoka Rombo au anatoka Musoma au anatoka Unguja au anatoka Pemba. Kwa hiyo, hii tabia ya kuanza kubaguana humu ndani nayo siyo nzuri. Haiwezekani ninyi mkawa wamoja halafu mkaanza kubaguana baguana humu ndani. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo vizuri kuunganisha na maslahi ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hivi vitendo lazima tuvikemee, hivi ndivyo vinavyovunja Katiba. Kwa sababu Ibara ya 100 ya Katiba ya nchi inayosema haki ya kujadili ya Mbunge yoyote aliyoko hapa bila kujalisha kwamba ni wa Viti Maalum, anatoka Pemba, anatoka Musoma au ni wapi. Kwa hiyo, mambo haya tunachezea lakini ni ya gharama kubwa sana. Ndiyo maana namuunga mkono sana Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe kuja na muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba kushauri tu kwamba Waheshimiwa Wabunge tuupokee huu muswada, ni mzuri kwa mtu ambaye anataka kuishi vizuri kwa kuzingatia sheria na Katiba za nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nimepata fursa hapa, namshukuru sana Mheshimiwa Halima Mdee ameleta mapendekezo ya kuboresha muswada huu na katika Ibara ya 6 hii ame-*single out* kifungu kidogo… *(Kicheko/Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Na iko tayari kwenye *amendment*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Iko kwenye *amendment,* hiki ndicho tunachokitaka. Kwa sababu nina muda mdogo tu hapa, kama ningekuwa na muda nikayasoma yale mambo yote yaliyoorodheshwa kwenye Ibara ya 6 yale, nani anaruhusu, kama yeye angekuwa kiongozi? Hivi ninyi mnazungumza mambo ya faragha; mambo ya faragha yale yako *protected* Ibara ya 16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yanayoendelea mahakamani, tumetunga sheria hapa, tunayo Sheria ya Mtoto inayozungumza kwamba hata zile *proceedings* zinazomhusu mtoto zisikilizwe kwa usiri *(in camera)*. Wanawake waliobakwa, mashauri yao yanasikilizwa kwa siri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii ni sheria tu, nadhani Waheshimiwa Wabunge hawakupata fursa ya kuisoma. Wale ambao wamepata fursa wameisoma, wameelewa. Mimi naomba kushauri Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu. Mheshimiwa Possi kwa dakika kumitena.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uhai siku ya leo. Nimepata hii fursa ya kuchangia huu muswada, nitachangia kwa haraka haraka baadhi ya mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kusema ukweli ni kwamba kwa Taifa letu hili la Tanzania lenye watu zaidi ya milioni 50, lenye mikoa mingi, mipaka kuanzia Mara mpaka Ruvuma, Katavi mpaka Pemba, haiwezekani hata siku moja, hata ingetokea mtu aangalie *television* zote, asome magazeti yote kwa siku akagundua, akapata habari zote za nchi; hata kama angepita kwenye mbao za matangazo kwenye ofisi zote za Serikali zilizopo katika eneo analoishi. Ndiyo maana sasa kuwe na utaratibu maalum wa kumwezesha Mtazania kupata habari pale anapoihitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wanaweza wakawa wamefanya tafiti ama za kitaaluma, ama za masuala mengine na utagundua ukweli ni kwamba siyo kila taarifa utaipata kwenye vyombo vya habari au utaipata kwenye *notice* za matangazo au kwamba utakwenda tu ikawa hapo hapo.

Kwa mfano, huwezi ukaenda leo ukasema naomba taarifa inayohusiana na historia ya elimu maalum Tanzania toka mkoloni mpaka mwaka 1980, halafu ukategemea utaipata hapo hapo; au huwezi uka-*expect* kwamba Afisa wa Serikali atajua tu wewe ukifika taarifa unayotaka ni hiyo.

Kwa hiyo, ni lazima kuwe na utaratibu maalum. Kwa maana hiyo, sheria hii inarahisisha sasa upatikanaji wa taarifa mbalimbali kinyume na baaadhi ya Wabunge wengi waliodhani kwamba hii taarifa, maana waliishia kwenye mfano mmoja kwamba labda inahusiana na taarifa za masoko au vikao vya Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kutokana na ukweli huo, ni lazima tutenganishe vitu viwili; sheria hii, nilikuwa nashangaa kidogo, mtu anaongelea hili *as if* waandishi wa habari sasa kabla ya kutoa taarifa yoyote, lazima wa-*apply* taarifa, hapana. Hiyo ingekuwa *unreasonable*, haikuwepo wala hata kabla ya kipindi cha mwaka 1984 wakati hatujawa na *Bill of Rights.* Pia kuliwa na mkanganyiko wa kuchanganya mambo ya *Whistleblowers* na muswada huu. Ni vitu viwili tofauti. Hapa tunazungumzia Mwananchi ambaye anataka taarifa. *Whistleblowers* ni mtu ambaye tayari ana taarifa, *the two do not go together.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine na bahati nzuri kwenye taarifa ya Upinzani walirejea katika Mkataba wa Umoja wa Mataifa unaozungumzia haki za kisiasa na haki za kiraia ambao kwa kweli Ibara ya 19 ya Mkataba huo inazungumzia haki ya uhuru wa habari. Cha kusikitisha, labda ni kwa bahati mbaya, wengi waliorejea hapo, wakasahau kurejea dokezo namba 34 la mwaka 2011 linalotolewa na Kamati ya Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa ambalo lilikuwa linatolea ufafanuzi kuhusiana na Ibara hiyo hiyo 19 ya huo mkataba ambao ni Ibara yetu ya 18 ya Katiba. Kama wangefanya marejeo hapo, mkanganyiko mwingi na vijembe vingi vilivyokuwa vinatolewa visingekuwepo kwa sababu ufahamu ungekuwa umeimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niende haraka haraka tu nitoe mfano. Nimesema kwa mfano, muswada huu hauna haja ya kuzuia habari, kwa sababu ukisoma kwa mfano Ibara ya 4, 5 na 9 inakuonesha. Kifungu cha 5 ni wajibu wa mwenye taarifa kutoa taarifa; kifungu cha 9, kikisomwa na marekebisho, bahati mbaya kuna watu walijitapa kwamba wamesoma, wameelewa jana, lakini walichokuwa wanachangia kinaonesha kwamba hata haya marekebisho ambayo Mwenyekiti aliweka pale mezani,

hawakutaka kuyasoma. Ukisoma na marekebisho, kifungu cha 9 kinasema; sheria itakapoanza kazi ndani ya miezi 36, Maafisa wote ni lazima waweke hizo taarifa hadharani. Hata kama kwa sababu moja au nyingine wasipoziweka, haimzuii, haiathiri haki ya mtu kupata taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 11 kinaonyesha kwamba *of course* mtu ukiandika taarifa bado unaweza ukajibiwa kwamba hili tayari linajulikana liko *public.* Maana yake nii? Ina-*imply* kwamba kuna uwezekano bado, licha ya sheria hii kutokea kwa mtu kupata taarifa kwa njia nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitumia busara tu, hivi ni kweli kwa muswada huu tunataka kudhani kwamba mwandishi wa habari akitaka kumhoji Mbunge au Waziri ni lazima aombe ruhusa kwa kupitia sheria hii hapa? Sidhani na *that is not correct.* Pia ukisoma vizuri Ibara ya 12 inakwambia hakuna chochote kwenye sheria hii kitakachomzuia mtoa taarifa kutoa taarifa kwa njia nyingine zaidi ya zile ambazo zimeelezewa katika muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema mwanzo lile la *Whistleblowers*, nasikitika sana hasa kwa wale ambao wanasema waliisoma muswada huu vizuri, hawakupitia Kifungu namba 23, hawakupitia ibara ya 23(1), hawakupitia Ibara ya 24. Ibara ya 23 inasema, hakuna atakaye adhibiwa iwapo atatoa taarifa inayoonyesha kuwa mtu ametenda kosa. *The same* na Ibara ya 24, hamna atakayeadhibiwa kwa mtu ambaye ametoa taarifa akiwa na nia njema. Kuna watu wakasema, anaadhibiwa vipi mtu akiwa amepewa taarifa mbovu? Jamani eeh, kwenye kanuni za adhabu kuna *defence* ya sheria inaitwa *mistake of fact*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mtu akitembea hapa akaokota *box*, kumbe lile *box* lina hela, hatahukumiwa kwamba ameiba pesa, kwa sababu *in his mind* alichoona ni *box.* Kwa hiyo, ukipewa taarifa wewe ukaamini ni kweli na ukaitoa chini ya kanuni za adhabu hutaadhibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kilichosemwa kingine hapa, aidha ni ....

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ni…

*(Hapa kengele ya kwanza ililia)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kengele ya kwanza au ya pili?

**MBUNGE FULANI:** Ya kwanza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Aah ya kwanza, *okay*. Niendelee na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ile *exemption* ya Ibara ya 6, kuna mtu mmoja alisimama jana akasema kwa mfano mambo ya faragha, kwamba hii ina mpango wa kuzuia maslahi ya viongozi. Faragha ni haki pia iko kwenye Katiba.

Kwa hiyo, hatuwezi tukaona haki moja tukaacha haki nyingine. Bahati nzuri hata katika huo Mkataba wa Umoja wa Mataifa ambao bahati nzuri Kambi ya Upinzani wame-*refer,* moja ya *limitation to the right of freedom of information* ni *privacy.* Sasa nashindwa kuelewa kwa nini hayo hayakuoneka, yanaonekana hapa? *That is either double standard* au unasoma ukiwa *biased*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia na masuala ya usalama. Kuna watu wanaona kama hili jambo geni. Kwa bahati nzuri katika hotuba yao waka-*refer* kwa mfano, jamaa wa *WikiLeaks* Julian Assange, kitu ambacho hawakusema, Julian Assange sasa yuko katika hifadhi ya kisiasa kwenye Ubalozi wa Ecuador kwa sababu Marekani wanamtafuta, alitoa taarifa zinazohatarisha usalama wake. Ni Marekani hiyo hiyo ambayo jana tuliambiwa hapa kiongozi wake George Washington aliyetoa *definition* ya *democracy*, hawazungumzii kuhusu Snowden aliyetoa taarifa za usalama, lakini leo taarifa za usalama za Tanzania zinaonekana ni kuzuia uhuru wa vyombo vya habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba tu niseme kwamba ni vizuri tunapochangia miswada tusome, tuielewe na tuwe wakweli. Siyo tabia njema kwa kiongozi aliyeaminiwa na hata aliyejigamba kwamba ameelewa kitu anachoki-*present* kusema mambo ambayo ukiangalia mara moja unagundua kwamba *he was simply not serious* katika *homework* yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, naomba nimalizie kwa kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Possi kwa mchango wako mzuri, umetusaidia sana. Sasa namwita mtoa hoja na mnauona muda wetu Waheshimiwa Wabunge, lakini tutajitahidi mtoa hoja dakika 50 hizi zitusaidie kabla ya kuingia kwenye Kamati ya Bunge Zima. Zege halilali.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuhitimisha hoja iliyoko mbele yetu kwa kujibu rai, mawazo na mapendekezo mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya Waheshimiwa Wabunge 39 wamechangia Muswada huu kwa kuongea na Waheshimiwa Wabunge watano kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ufafanuzi mzuri wa Waheshimiwa Wabunge mbalimbali pamoja na Mheshimiwa Waziri Nape, Mheshimiwa Naibu Waziri Possi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, naomba niongelee hoja chache tu za ujumla zilizochukua sehemu kubwa ya hotuba za baadhi za Waheshimiwa Wabunge, jana na hata leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa kifupi tu Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Abdallah Mtolea, Mbunge wa Temeke ambaye kwa bahati mbaya aliamua kutengeneza Muswada wake wa Habari na kuujadili, badala ya kujadili Muswada wa Taarifa ambao nimeuwasilisha hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msemaji wa Upinzani ameongelea kwenye hotuba yake kila kinachomkera, *NGO's*, magazeti kufungiwa, watuhumiwa kubambikiziwa kesi na polisi na kadhalika vitu ambavyo kwa kweli viko nje kabisa ya maudhui na muktadha wa muswada ulioko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kwa karibu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 18(b) na (d), inasema, naomba turudie, wenzangu wamejaribu sana kuelezea hii. Ibara ya 18(b) inasema: "Kila mtu ana haki ya kutafuta;" yaani *to seek (to look for),* kupokea *(to receive)* na kutoa *(to disseminate),* kusambaza habari bila ya kujali mipaka ya nchi. Sasa hii inaongelea habari *without frontiers;* unakwenda popote. Unaweza kutuma kwenda Marekani. Hii inahusu habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 18(d) inazungumza: "Kila mtu anayo haki ya kupewa taarifa." Sasa badala ya habari, imekuja taarifa, wakati wote. Tena hili "wakati wote," neno hili nakumbuka jana Mheshimiwa Mwalimu Bilago alifurahia sana akasema ehee ni kila wakati. Nikawa naogopa, nasema eeh Mwalimu siyo maana ya kila wakati, hata ukilala unapewa tu taarifa; usingizini unapewa taarifa. Utawehuka, sio hivyo! Ukiisoma kwa *context,* ukitumia; sisi tunaita *contexualist approach,* haina maana ya kila wakati, ina maana ya pale unapohitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, inasema kila mtu anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia kuhusu masuala muhimu kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili liko wazi, lakini ni huku kujichanganya kwa hii dhana kwamba tunaongelea habari badala ya taarifa ndiko kulifanya huu muswada kwa mara ya kwanza kwenye Bunge la Kumi kuondolewa na

tukaagizwa kuufanyia kazi zaidi na kwa kweli tumeufanyia kazi zaidi kama ambavyo Bunge lilivyoagiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria - Mheshimiwa Mchengerwa, ameelezea hapa katika hotuba yake ukurasa wa tatu kuwa Kamati yake iliita makundi mbalimbali ya wadau. Yalikuwa makundi 10 ukisoma, lakini matano kati ya hayo yalikuwa makundi ya wanahabari na ameyataja, sitaki kupoteza muda, ameyataja ukurasa wa tatu. Makundi matano, watu wazito katika tasnia ya habari. Alifanya hivyo kwa makusudi mazuri sana, ni kwa sababu wanahabari ndio walikuwa kwa kweli ni chanzo kikubwa cha huu muswada kuondolewa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimsikia Mheshimiwa Anatropia Theonest hapa akisema uandishi wa habari wa nini kwenye Muswada wa Taarifa? Hapana! Ilikuwa lazima tuwaite Mheshimiwa kwa sababu nzuri tu ya kwamba walikuwa wao ndio sababu kubwa ya huu muswada kuondolewa Bungeni kwa sababu walidhani muswada huu ni wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa rafiki zangu hapa siwaoni, Mheshimiwa Lema, Mheshimiwa Msigwa…

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Nipo hapa.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Aha! Vilevile na Mheshimiwa Silinde, jana walitumia muda mwingi wakidai kuielewa zaidi tasnia ya uandishi wa habari kuliko waandishi wa habari wenyewe waliokuwepo. Waliokuwepo tumekaa nao kwenye Kamati kwa muda mrefu sana. Huu Muswada umechukua miaka kumi kufika hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi kama mwandishi, kwa *background* yangu naweza kusema kwamba sheria hii inawaongezea waandishi wa habari wigo zaidi. Kwa nini? Ni kwa sababu sheria hii inamhusu mtu wa kawaida, Mtanzania yeyote na mwandishi wa habari ni sehemu ya Watanzania. Anaweza akapata taarifa kama mwananchi na hiyo taarifa akiipata yeye anaigeuza kuwa habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa pili chini ya Sheria ya Habari, yeye ana *Press Card* chini ya Sheria ya Uandishi wa Habari ambayo itaheshimu kipengele cha Katiba kinachosema ana haki ya kutafuta, ana haki ya kupokea, ana haki ya ku-*disseminate,* ana madaraka makubwa zaidi kuliko sisi hapa tunamfikiria mtu wa kawaida kwamba hili Taifa limegeuka la waandishi wa habari watupu, hapana.

Kwa hiyo, wenzangu Waheshimiwa Wabunge jana wameongelea sana kuhusu waandishi wa habari, wakafikia hata hatua wakasema siku moja eti CCM isijisahau, inaweza kuwa Upinzani na CHADEMA ikawa Chama Tawala. Aah, wapi na wapi bwana *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbushane tu kwamba Kiongozi wenu mwenyewe mnamjua, amekiri kuwa nyie bado ni kikundi cha wanaharakati, bado kukua kuwa chama cha siasa. Na mimi sijawahi kuona duniani hapa kikundi chochote cha wanaharakati kikaunda Serikali. Mtasubiri sana kama fisi yule wa hadithi ambaye alisubiri mkono wa binadamu udondoke, mpaka mtoke kwenye uanaharakati. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Silinde anadai Mheshimiwa Rais kashauriwa vibaya kuhusu muswada huu. Mheshimiwa Silinde alikuwepo Bunge la Kumi. *He is not honest!* Muswada huu anajua una umri wa miaka kumi na alikuwepo ulipoondolewa hapa Bungeni. Sasa huyu Rais Magufuli anatokea wapi katika muswada huu na akashauriwa vibaya? Muswada huu tumeupokea ndiyo maana tumeusoma mara ya pili na ya tatu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lema na Mheshimiwa Msigwa wamenituhumu mimi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushindwa kumshauri Mheshimiwa Rais vizuri, yaani tumshauri wanavyotaka wao. Hivi ndugu zangu, tena yupo hapa ndugu yangu Mheshimiwa Mbowe, anapowaambia wote tutoke ndani ya Bunge hili na wote mnatoka kama kumbikumbi, mnatoa ushauri gani ninyi? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza; namuuliza Mheshimiwa Lema na Mheshimiwa Mchungaji Msigwa! Kuweni wavumilivu… *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, *order in the house*. Naomba utulivu. Nakuona Mheshimiwa, mnafahamu mimi sipendi kutaniwa kwenye Kiti. Naombeni sana Waheshimiwa Wabunge tuheshimu Kiti. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa mtoa hoja anajibu yale yaliyosemwa jana. Wakati baadhi yenu mnachangia mimi niliwavumilia kwa sababu mlikuwa mnaenda nje ya hoja. Sasa lazima nitende haki kwa pande zote mbili. Nawaambieni Waheshimiwa Wabunge, mtoa hoja lazima ajibu kama anavyoona inafaa kujibu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri, endelea. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nivumiliwe tu kwa sababu ninayo *right of reply* kwa yale yaliyosemwa hapa na yameingia kwenye *Hansard*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeongelewa hapa kwamba tunamshauri Mheshimiwa Rais vibaya. Na mimi nauliza, Mheshimwa Silinde na Mheshimiwa Msigwa mlivyokuwa mnasema hapo jana, wakati ndugu yangu Mheshimiwa Slaa anaenguliwa, anaingizwa mtu ambaye wala hamkumchagua kushika bendera, mlikuwa wapi kumshauri? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sikujua, mkuki kwa nguruwe, kumbe kwa binadamu mchungu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuja huko, naweka tu *basis* ya *argument* kwamba leo Mheshimiwa Lema na Mheshimiwa Msigwa mmetumia muda mrefu mki-*question integrity* ya *Attorney General* na mimi, na mimi nawajibu hapa kwamba ninyi hamna *moral authority* ya kuweza ku-*question integrity* yetu sisi kwa sababu ninyi hamna *integrity! (Makofi/Kicheko/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa linamkumbuka Mheshimiwa Lema na Mheshimiwa Msigwa, mmezunguka mkimtangaza Mheshimiwa Lowassa kuwa fisadi, leo mnalamba nyayo zake. *(Makofi/Kicheko/Kelele)*

**MBUNGE FULANI:** Huo siyo muswada.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niruhusiwe kujibu hoja zote zilizosemwa jana hapa na nina muda wa kutosha.

**MBUNGE FULANI:** Jibu. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Naomba nisisitize, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hajavunja sheria yoyote, hajavunja Katiba, alichofanya ni kuheshimu kiapo chake cha kuhifadhi, kuilinda na kutetea Katiba na sheria za nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameeleza vizuri sana hapa, wajibu…

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimezoea, hii ndiyo *style* ya wanaharakati, kwa hiyo hamna wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema tu ni kwamba alichofanya Mheshimiwa Rais ni kuzuia siasa za shari za uanaharakati zisilisambaratishe Taifa letu. Ndiyo alichokifanya na ni wajibu wake Kikatiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais najua leo ali-*perceive danger, hence the moratorium*. Nilitegemea busara kwa chama chochote kwenda mahakamani kama alivyosema *Attorney General.* Kama huendi mahakamani

basi jipange, hebu dai majadiliano na Serikali. Mpaka leo sijaona, nimemuuliza *Attorney General,* hata ofisini kwangu hatujapata hata siku moja hata *indication* ya kwamba wenzenu tunataka tujadiliane hili suala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais kama unadhani alisema kitu ambacho siyo sahihi, lakini jibu lake siyo wewe ku-*call for civil disobedience* nchi nzima bila ukomo, hilo halikubaliki! *If you believe the President was wrong still, two wrongs do not constitute a right!* Na sisi wanasheria tunasema, *he who seeks equity, should come with clean hands. I don't see clean hands across this floor. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyosema mimi na *Attorney General* hatujawahi kupokea mawazo yoyote kutoka kwa Upinzani. Tubadilike, tuwe chama; milango yetu iko wazi. Tusiupe uanaharakati nafasi katika shughuli zetu za kuendesha nchi. Mengine nayaacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya haya mafupi ya utangulizi, sasa naomba nisisitize tu kuwa muswada ambao uko mbele yetu leo, unalenga kupanua wigo wa upatikanaji wa taarifa, siyo tu kwa wananchi, lakini hata kwa wale tunaodhani wamelengwa kuminywa (waandishi wa habari) na hii inalenga kama nilivyosema mwanzoni na wenzangu wengi wamesema, kwa kweli kutekeleza matakwa ya Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muswada huu naomba sana Waheshimiwa Wabunge tuusome vizuri. Haukusudiii kudhibiti vyombo vya habari, *not at all!* Haukumdhibiti mtu yeyote mwingine lakini kupanua tu wigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba vile vile uamuzi wa Serikali kuleta Muswada huu, pia umechagizwa na Malengo Endelevu *(Sustainable Development Goals)*. Yaliyowekwa na nchi 193 wanachama wa Umoja wa Mataifa ambao na sisi ni wanachama, tarehe 25 Septemba, 2015 lengo namba *SDG16.10* linasema, *"every country to ensure public access to information."* Lengo hili kimsingi linakusudia kupanua wigo wa upatikanaji wa taarifa kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya ya jumla, naomba sasa nijibu hoja moja moja, nyingine zimeshajibiwa na wenzangu, kwa hiyo, nitazigusia tu juu juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu adhabu inayopendekezwa kutolewa kupitia kifungu cha 6(6) cha hii sheria inayopendekezwa kwa wale watakaotoa taarifa zilizozuiliwa, tumetafakari kwa kirefu hoja zilizotolewa na Kamati na Waheshimiwa Wabunge wawili Mheshimiwa Zedi na Mheshimiwa Mhagama na hivyo tunapendekeza kwenye *schedule of amendment* ya kifungu cha 6(6) kwa

madhumuni ya kutenganisha adhabu kati ya kosa la kutoa taarifa zilizozuiliwa zinazohusu Usalama wa Taifa na kutoa taarifa zilizozuiliwa zisizohusu Usalama wa Taifa.

Hivyo basi, Jedwali la Marekebisho linapendekeza adhabu ya kifungo kisichopungua miaka mitatu na kisichozidi miaka mitano kwa kutoa taarifa ambazo zilizuiliwa na ambazo hazihusu masuala ya usalama wa Taifa. Marekebisho hayo pia yanapendekeza kuwa endapo mtu atatiwa hatiani kwa kosa la kutoa taarifa zilizozuiliwa zinazohuzu masuala ya Usalama wa Taifa adhabu yake itolewe kwa mujibu wa Sheria ya Usalama wa Taifa. Hayo ndiyo marekebisho tumeyafanya kutokana na maoni yenu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuzuia baadhi ya taarifa zisitolewe kwa umma, napenda kumjibu Mheshimiwa Mollel, Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Selasini na Mheshimiwa Riziki nafikiri waliongelea hili. Huu ni utaratibu wa kawaida duniani, sijawahi kuona nchi yoyote yenye *open door policy* kwenye masuala yake ya kiusalama. Aidha, haki na uhuru wowote duniani una mipaka na hata sisi tumeweka mipaka na mipaka yote ya namna hiyo inaruhusiwa Kikatiba, ndiyo maana kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Possi, Bwana Julian Assange anajibanza kwenye Ubalozi wa Ecuador, London tangu mwaka 2012 mpaka leo hajatoka, tena akiwa amekera nchi kubwa duniani Marekani, Uingereza na Sweden.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zote duniani ambazo zina sheria ya upatikanaji wa taarifa zimeweka mipaka ya aina hiyo ya taarifa ambazo zinazoweza kutolewa kwa umma na zisizoweza kutolewa kwa umma. Aidha, hata taasisi za Kimataifa ambazo zimekuwa zikiandaa sheria za mifano kwa nchi zetu ambazo zilikuwa bado hazina hiyo Sheria ya Upatikanaji wa Taarifa zinaweka vifungu vinavyozuia baadhi ya taarifa kutolewa kwa umma. Mathalani Sheria ya Mfano wa Upatikanaji wa Taarifa ya Umoja wa Mataifa *(Model Law on Access to Information for Africa)* inaweka masharti yanayozuia baadhi ya taarifa kutotolewa kwa umma. Kwa faida ya Bunge lako Tukufu sheria hiyo ya mfano imeandaliwa na Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ambayo ina dhamana ya kusimamia haki za binadamu katika Bara letu la Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo kwa kifungu cha 6 kinachoweka masharti ya kuzuia baadhi ya taarifa kutolewa kwa umma kumefanywa kwa nia njema na kwa maslahi ya Taifa, raia wote na ustawi wa jamii nzima ya Kitanzania. Hivyo, niliombe Bunge lako Tukufu kuridhia masharti ya kifungu hicho kama ilivyopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, nakumbuka Mheshimiwa Mollel na Mheshimiwa Kangi

Lugola waliochangia muswada huu wameonesha wasiwasi wa kutokuwepo kwa tafsiri ya neno *national security* na kwa maneno hayo yanaweza kutumika kufifisha haki ya upatikanaji wa taarifa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge kuwa taarifa zinazohusu *national security* zimefafanuliwa kwa kina katika Ibara ya 6(3), sijui wengine hapa hawakusoma muswada huu ndiyo maana walikuwa wanalalamika. Taarifa za *national security* zimeelezwa kuwa ni taarifa zinazohusu, pengine ninukuu kwa haraka haraka tu, *section* ya 6 inasema, zinazohusu mikakati ya kijeshi, mafundisho, uwezo, nafasi au usambazaji; taarifa ya Serikali ya kigeni inayohusisha Usalama wa Taifa na kazi za kijasusi, vyanzo, uwezo, utaratibu au usiri.

Kwa hiyo, vimeainishwa humu pamoja na kwamba wengine wetu tuliona kwamba kwa kweli kuna mapengo makubwa katika muswada huu. Masuala haya kwa ujumla wake ni nyeti kwa usalama wa nchi na mahusiano yake na mataifa mengine na hivyo hayatakiwi kutolewa kwa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, umeoneshwa wasiwasi na Mheshimiwa Ruth Mollel kuhusu taarifa zinazohusu faragha ya mtu, amelijibu vizuri sana Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Possi. Nisisitize tu kwamba msingi wa kuzuia taarifa za faragha unatokana na Katiba, Ibara ya 16(1) inayoeleza kuwa kila mtu anastahili kuheshimiwa na kupata hifadhi kwa nafsi yake, maisha yake binafsi na familia yake. Hivyo basi, tunapendekeza pia katika muswada huu kuzuia ukiukaji wa haki ya faragha isipokuwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Katiba na Sheria ilipendekeza kufanyia marekebisho kifungu cha 7 kwa minajili ya kumtaka mkuu wa taasisi anayeshindwa kumteua Afisa Taarifa kuwa Afisa Taarifa mwenyewe kwa madhumuni ya sheria inayopendekezwa. Kimsingi Wizara yangu haina pingamizi na pendekezo hilo na tayari Jedwali la Marekebisho linapendekeza hilo ambalo Waheshimiwa Wabunge walitaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu muda wa siku thelathini wa kushughulikia maombi ya taarifa kuonekana mrefu sana, ni rai ya Wizara yangu kuwa muda huo ni muafaka tukizingatia wingi wa taarifa zitakazokuwa zikiombwa na ukubwa wa nchi yetu. Hata hivyo, kupitia Jedwali la Marekebisho tunapendekeza muda wa kushughulikia maombi hayo iwe mapema iwezekanavyo na si zaidi ya siku thelathini tangu kupokelewa kwa maombi husika kutoka kokote kule nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kanuni ambazo tumeanza kuandaa zinaainisha aina ya taarifa na muda wa kutolewa siku moja, mbili, tatu na kadhalika lakini muda hautazidi siku thelathini, hiyo ndio maana yetu. Kwa

mantiki hiyo basi zipo taarifa ambazo kwa mujibu wa kanuni zitakazotengenezwa zitatolewa ndani ya muda mfupi kama siku moja na hivyo kuondoa uwezekano wa kuwepo kwa ucheleweshaji usio wa lazima. Kwa mfano, kama nilivyosema katika hotuba yangu ya mwanzo mtu yuko kijijini anaomba *BOQ* ya barabara inayojengwa kijijini kwake, sisi katika kanuni zetu tutapendekeza apewe ndani ya siku moja maana *BOQ* iko pale pale Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati vilevile ilipendekeza kuwa Waziri asiwe na mamlaka ya mwisho ya kushughulikia rufaa zitakazotokana na maamuzi ya wamiliki wa taarifa kutotoa taarifa kwa mujibu wa sheria inayopendekezwa. Niseme tu katika nchi yetu inayoheshimu utawala wa sheria, kwa mujibu wa Ibara ya 107A ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina kauli ya mwisho katika masuala yote ya utoaji haki. Aidha, Mahakama Kuu ina mamlaka ya asili tunaita *inherent jurisdiction* ya kufanya *intervention* au kufanya mapitio ya uamuzi wowote uliofanywa na chombo chochote cha utendaji na pale Waziri anapokuwa anasikiliza pengine *appeal* hawi mahakama ni *quasi- judicial body*.

Vilevile bado tunadhani mahakama hata bila kutaja maana sheria nyingi zinaeleza hivyo zinapomtaja Waziri zinamtaja kiongozi wa upande wa utendaji lakini madaraka ya Waziri ni ya utendaji tu, lakini hayawezi kuifunga mahakama. Kwa hiyo, bado mahakama itakuwa na mamlaka ya mwisho ya kuamua hatma ya maombi ya taarifa yatakayokataliwa na mmiliki wa taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumeboresha kifungu cha 19 kwa kuongeza kifungu kidogo cha (4) kinachosema pale ambapo mmiliki wa taarifa anayelalamikiwa yupo ndani au yuko chini ya Wizara ambayo itakuwa Wizara yangu basi Waziri katika suala hilo hatakuwa na mamlaka ya rufaa na mlalamikaji atakuwa huru kwenda Mahakama Kuu. Tumefanya maboresho hayo na lengo la kwenda Mahakama Kuu ni kupitia maamuzi hayo. Hayo yamo kwenye *schedule of amendment.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema wakati wa kuwasilisha Muswada huu mbele ya Bunge lako Tukufu taarifa ni nyenzo muhimu ya kufikia malengo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii katika jamii yoyote. Mwanafalsafa wa kale wa China aliwahi kusema, *the journey of a thousand miles begins with one step* yaani safari ndefu huanza na hatua moja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri samahani kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, watu wa *Hansard* bado wananiambia tunashauriana kwa sauti ya juu mno. Naomba tushauriane lakini isiwe kwa sauti ya juu. Ahsante, Mheshimiwa Waziri endelea. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema kwamba sasa ndiyo tunapiga hatua yetu ya kwanza ya kutekeleza masharti ya Ibara ya 18(d) ya Katiba kuhusu haki ya kupata taarifa. Kwa msingi huo, niliombe Bunge lako Tukufu liliridhie sheria imhusu raia wa Jamhuri ya Muungano pekee kwa kuanzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani, Mheshimiwa Anatropia Theonest, Mheshimiwa Mwalongo, Mheshimiwa Amina Mollel na Mheshimiwa Devotha Minja waliongelea hili, lakini mimi naomba waelewe kwamba huu ni mwanzo, tunahitaji kujifunza na kujidhatiti kabla ya kufungua milango yote na madirisha kwa watu wasio raia kunufaika na masharti ya sheria hii. Tukifungua milango na madirisha yote wakati huu wa mwanzo kuna hatari sana ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge ya kuingiza vitu tusivyovitarajia na hatimaye kuhatarisha usalama wa Taifa letu. Kupanga ni kuchagua na kila jambo lina wakati wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati vilevile ilipendekeza kuwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ipewe mamlaka ya kusimamia utekelezaji wa sheria inayopendekezwa. Wengine wamependekeza kuwa kiundwe chombo mahsusi kitakachosimamia utekelezaji wa sheria inayopendekezwa. Ni maoni ya Wizara yangu kuwa kwa mujibu wa *principles* zinazotoa mwongozo wa muundo wa mamlaka wa vyombo aina ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora tuliyonayo hapa Tanzania si muafaka kwa Tume kupewa wajibu huo kwani kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sheria inayoanzisha Tume, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni chombo cha ushauri kwa Serikali na hivyo hakiwezi tena kufanya shughuli za uratibu ambazo kwa kweli zinatakiwa kufanywa na Serikali yenyewe. Bado wananchi wana haki ya kupeleka malalamiko yao kwenye Tume wakiona haki yao ya kupata taarifa inakanyagwa kinyume na sheria. Tume ni *ombudsman* yenye wigo mpana wa kufanya *intervention* wakati wowote.

Aidha, kwa sasa Serikali bado haioni haja ya kuwa na chombo mahsusi kabisa kushughulikia masuala ya upatikanaji wa taarifa, itakuwa gharama bure kwa Taifa. Hivyo basi, tunapendekeza jukumu la usimamizi wa sheria inayopendekezwa kwa kuanzia liachwe mikononi mwa Wizara husika yenye dhamana ya masuala ya haki itakayowajibika kusimamia, kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa sheria inayopendekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mengine nitaruka kutokana na muda, hatua gani zitachukuliwa kwa mmiliki wa taarifa atakayetoa taarifa potofu, hii ni Kambi Rasmi ya Upinzani na Mheshimiwa David Silinde na Mheshimiwa Waitara. Naomba niseme tu kwamba Ibara ya 21 ya muswada inapendekeza adhabu ya faini isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili kwa mtu yeyote atakayetiwa hatiani kwa kubadili, kufuta maandishi yasisomeke,

kuzuia, kuharibu au kuficha kumbukumbu zozote zinazoshikiliwa na mmiliki wa taarifa kwa dhamira ya kuzuia upatikanaji wa taarifa.

Mheshimiwa Kangi Lugola alisema Serikali iweke wajibu kwa taasisi za umma zinazomiliki taarifa ili zitoe taarifa kila baada ya kipindi fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimrejeshe Mheshimiwa Kangi Lugola Ibara ya 9 ya muswada huu ambayo inajieleza vizuri sana. Hata wenzangu waligusia katika maelezo, Ibara ya 9 inasema; "Kila mmiliki wa taarifa, si zaidi ya miezi thelathini na sita baada ya kuanza kutumika kwa sheria hii, atatoa kwenye gazeti, tovuti au gazeti linalopatikana kwa wingi likiwa na, maelezo juu ya aina, kazi na majukumu ikijumuisha majukumu yoyote ya kisheria ya maafisa au kamati za ushauri; maelezo ya jumla ya aina za taarifa zinazopatikana kwa mmiliki wa taarifa huyo; maelezo ya vijarida vyote na aina nyingine za nyaraka na kadhalika. Kwa hiyo, nilitaka kueleza tu hapa kwamba tumeweka kifungu kwenye sheria hii kuwataka wamiliki wote wa taarifa kutoa hizo taarifa, ukiingia kwenye Wizara, kwenye ofisi yoyote ya mmiliki wa taarifa ukute hizo taarifa, *it should be a standard practice*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Hussein Bashe alitaka Serikali iweke utaratibu wa kurekebisha mfumo wa utoaji adhabu katika sheria zilizopo na zilizopitishwa na Bunge. Ni wazo zuri na Wizara yangu imelipokea na tutalifanyia kazi. N kweli kabisa kwamba tunahitaji *policy* ya kutu-*guide* kuhusu masuala ya adhabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwalongo alisema taarifa zitolewe kulingana na shughuli za uzalishaji za eneo husika na nafikiri nimelieleza hilo kwamba Ibara ya 9 itatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa muswada unaopendekezwa kila mmiliki wa taarifa popote alipo ndani ya mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anawajibika kutoa taarifa alizonazo kulingana na shughuli zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mheshimiwa David Silinde, nimeshalieleza hilo la kwamba Serikali imebadili maudhui ya muswada, hapana hatujabadili maudhui. Yeye alikuwepo katika Bunge la Kumi anaelewa kilichotokea, huu ni Muswada wa Taarifa siyo wa Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile taarifa zinazozuiliwa na maslahi ya kibiashara ziondolewe katika muswada kwa kuwa zinaweza kusababisha mikataba inayoingiwa na Serikali kuwa siri.

Waheshimiwa Wabunge, pengine mmesahau kwamba nyie mna madaraka ya kuitisha mkataba wowote mkauangalia lakini taarifa inazuia

endapo kutolewa kwake kunaweza tu kuathiri maslahi ya kibiashara yakiwemo pia ya mmiliki wa taarifa ikiwemo Serikali. Ni vyema kipengele hiki Waheshimiwa Wabunge kikaendelea kuwepo ndani ya muswada huu na hii ndiyo *practice* ya dunia nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, kutoa taarifa ya nchi nyingine ambayo itasaidia usalama wa nchi ni kosa, aliuliza Mheshimiwa Hussein Bashe. Mimi ninachotaka kusema kwa ujumla ni kwamba ukiwa na taarifa za nchi nyingine zenye athari kwa usalama wa nchi yetu si vyema kutangaza, *share with the government*, unakuwa pale na wewe kama *a whistleblower* itasaidia zaidi kuliko kwenda peke yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwita Waitara, Mheshimiwa Joseph Selasini, Mheshimiwa Anatropia Theonest, Mheshimiwa Pauline Gekul waliuliza kwa nini sheria hii inapendekezwa itumike Tanzania Bara tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri imeelezwa sana na Waheshimiwa Wabunge wengi, kwanza niseme kwamba hii si sheria ya kwanza ya aina hiyo. Tumetunga sheria nyingi sana ambazo *application* yake ni Bara na wala haziendi mpaka Zanzibar na wenzetu Zanzibar wakishaona umuhimu wa hiyo sheria nao wanai-*domesticate* kupitia Baraza lao la Wawakilishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili msingi wa Sheria ya Upatikanaji wa Taarifa tumesema ni Ibara ya 18 ya Katiba yetu na vilevile kwa Katiba ya Zanzibar nao wana Ibara ya 18 inaeleza hayo hayo na mimi nimepata mwelekeo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar nayo itakuwa na sheria hiyo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Pauline Gekul alikuwa anasisitiza sana jana kwamba hii ni Sheria ya Katiba hapana hii siyo Sheria ya Katiba ni sheria ya kawaida. Sheria zote nchini msingi wake ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na vitu vingine vichache. Mheshimiwa Hussein Bashe, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, sheria imlinde *third party* au mchapishaji wa taarifa ambaye ataitoa *in good faith* kama inavyomlinda mtoa taarifa *in good faith.*

Naomba tu niwahakikishie kwamba kwa maudhui ya ibara hii ni kumlinda mtu aliye chini ya mmiliki wa taarifa dhidi ya hatua za kisheria, kiutawala au kiajira, pale anapotoa taarifa zinazofichua maovu ya mmiliki wa taarifa kwa nia njema akiamini kuwa taarifa hizo ni za kweli. Msingi wa ibara hii ni kuendana na masharti ya Sheria ya Kuwalinda Watoa Taarifa za Uhalifu wa Mashahidi *(The Whistleblower and Witness Protection Act)* ambayo tumeipitisha sisi wenyewe kwenye Bunge hili na imeanza kufanya kazi. Hivyo basi, mtu anayechapisha

taarifa ya aina hiyo kwa nia njema akiamini kuwa ni kweli anaweza pia kuchukuliwa kuwa ni mtoa taarifa ya uhalifu anayestahili kulindwa kwa mujibu wa sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mheshimiwa Mwita Waitara alisema simu itumike kama mojawapo ya njia za kutoa taarifa. Ni wazo zuri, kanuni tunaziandaa sasa hivi, zitaainisha njia mbalimbali za kutoa taarifa na hatutasahau huo mchango wa Mheshimiwa Waitara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, neno habari litafsiriwe, Mheshimiwa Omar King. Muswada huu unahusu taarifa na si habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupigiwa hiyo kengele ya kwanza, kwa kumalizia nisisitize kuwa muswada huu umeletwa kwa nia njema ya kupanua wigo wa upatikanaji wa taarifa ambazo ni chachu kwa maendeleo ya Taifa letu. Niliombe Bunge lako Tukufu kuupitisha muswada huu ili wananchi waanze kunufaika na taarifa mbalimbali muhimu kwa mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, hoja imetolewa na imeungwa mkono. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaingia kwenye hatua inayofuata ili tuutendee Muswada huu haki maana tunaingia sasa kwenye shughuli ya kutunga sheria kwa maana ya kwenda kifungu kimoja baada ya kingine na kwa muda mnavyouona, hata kama nitatumia zile dakika 30 kama Kanuni zinavyoniruhusu bado hatutakaa vizuri lakini lazima tumalize leo.

Kwa hiyo, nilikuwa nashauri hoja itolewe kwa mujibu wa Kanuni ya 153 cha Kutengua Kanuni ya 28(4) ili tuendelee na Muswada huu tukiwa kwenye Kamati ya Bunge Zima hadi hapo tutakapomaliza na Mtoa Hoja kuja kutoa Taarifa. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa na muda wa kuufanyia kazi muswada huu kwani yapo mapendekezo ya mabadiliko mengi na ndiyo tunatunga sheria ni kitu kizuri sana, sasa tuonekane kweli kazi hii tunaifanya kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**HOJA YA KUTENGUA KANUNI**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 28(3), ikisomwa pamoja na Kanuni ya 153, naomba nitoe hoja ili Bunge lako liendelee na kazi hii na liahirishwe pale ambapo tutakuwa tumemaliza shughuli ambayo ilikuwa imepangwa leo katika *Order Paper*. Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa imeungwa mkono, sasa muiamue Waheshimiwa Wabunge.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bunge liliridhia kuongeza muda mpaka litakapokamilisha kazi zilizopangwa)*

**MWENYEKITI:** Wote wameafiki, tuendelee na kazi, Katibu. *(Makofi)*

**NDG. THEONIST RUHILABAKE - KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Wajumbe wa Kamati tuketi. Katibu.

Ibara ya 1

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 2

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Tibaijuka.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika *clause* ya 2(2)(b)(ii), napendekeza tuongeze maneno ya kufafanua hawa watu wanaohusika na muswada huu. Naunga mkono muswada na nasimama hapa kujaribu kuboresha.

Pendekezo langu ni kwamba, kati ya maneno *which* na *is* tuweke kwamba; *"Of information which has been declared by the court of jurisdiction as of significant public interest."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naleta pendekezo hili kwa sababu nimeona muswada huu pia utahusu sio tu taarifa za kutoka kwenye mashirika ya umma lakini pia hata mashirika binafsi. Katika dunia ya ushindani ni lazima pia tuwe na sheria ambazo zinalinda *privacy* ya mashirika kama ya biashara.

Kwa hiyo, nikaona kama kweli *information* itaonekana ina maslahi ya umma na jambo hilo linawezekana na halina ukakasi, mahakama ndiyo iseme toa habari hii kwa sababu umma una maslahi nayo. Kuiachia hivi hivi tunajiweka mikononi mwa binadamu na binadamu wote tunajua mapungufu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo mantiki ya *amendment* yangu. Naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa mtoa hoja au yeyote kama mlivyojipanga, Mheshimiwa Dkt. Possi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona kwamba utaratibu huo utakwenda kinyume na dhima nzima ya sheria hii ambayo ni kupunguza urasimu katika upatikanaji wa taarifa. Ukweli ni kwamba ina *presume* wakati wowote kwanza mtu anakwenda mahakamani, ana-*seek relief,* Mahakama ndiyo itaje kwamba hili ni *public interest* halafu tena ndiyo arudi. Ukweli ni kwamba *public interest* ni neno ambalo limekuwa limetumika katika sheria nyingi kwenye muktadha wake mpana sana. Kwa hiyo, tunaona hili litakwenda kinyume kabisa na sheria yenyewe na ukweli utekelezaji wake pia utakuwa ni mgumu sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kwa maelezo hayo Mheshimiwa Profesa Tibaijuka unasemaje? Ni maelezo mazuri tu.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali ni maelezo mazuri, lakini na mimi naomba Mheshimiwa Waziri aangalie maelezo yangu kwamba hapa tunazungumzia watekelezaji kwa makampuni binafsi, mtu anaweza kuja kwako akasema anataka habari kwa sababu kuna maslahi ya umma. Mimi naweka utaratibu kuhakikisha kwamba unatulinda wote maana ili sheria ikae vizuri lazima ilinde *possible interest of all parties.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kweli nimemsikia Mheshimiwa Waziri alivyofafanua, lakini sijaridhika na ufafanuzi wake. Bado naona kwamba *amendment* yangu na yenyewe inatekelezeka, lazima tulinde watu ambao

wana taasisi zinazoweza kuingiliwa na watu wanaotumia madaraka yao vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama pendekezo langu halieleweki naomba nitoe hoja ijadiliwe, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza bado hata hizo *private bodies* kwa sheria hii haziondolewi uhuru wao wa kwenda Mahakamani kama wakiona inafaa kwa sababu kwa kukataa kwao hawaadhibiwi moja kwa moja. Kwa hiyo, bado wana haki yao ya kupeleka mashauri yao kuomba sasa *information* yao iwe *protected,* hakuna chochote kwenye sheria hii kinachozuwia wao kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ili kuondoa urasimu na msongamano wa kesi, kwa sababu tunaangalia katika watu milioni 50 na *private sectors* na watu wanataka *information,* hapana. Tukiruhusu hili tutaleta msongamano wa kesi nyingi sana mahakamani na *bureaucracy* kwa sababu taarifa nyingi sidhani kama mtu atataka kuona *patent rights,* shughuli za kimkakati za kibenki, *that one will not be the case, it is for public interest* na *public* inajulikana siyo taarifa ya siri ya kampuni fulani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Tibaijuka, maelezo ni mazuri hata mimi nilikuwa nasema, kwa nini tusiipatie nafasi sheria hii ikaanza kutumika, mbele ya safari haya uliyoyasema kama yatajitokeza *then* Bunge litakuwepo, Serikali itaendelea kuwepo wanaweza wakaja wakairekebisha tu, unaonaje Profesa?

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, mimi nakubaliana kwamba unaweza kuwa *positive* lakini kitu cha kujaribisha kwanza tuone sheria itakwendaje halafu ndiyo turudi linaweza likatukwamisha. Mimi naomba hoja yangu ijadiliwe. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Hoja ya kuchangia hapa ni *whether* tunataka maneno haya yaingie kwenye kifungu cha 2(2)(b)(ii) kama inavyopendekezwa na Profesa Tibaijuka. Hivyo ndivyo mjadala utakavyokuwa, yaingie au yasiingie, tusilete *story* ndefu ya kwenda huku na huku. Mheshimiwa Profesa umeshatoa hoja yako lakini sikuona inaungwa mkono. Ili tumtendee haki wasije wakasema mimi, irudie tu tuone kama inaungwa mkono halafu iingie katika hatua ya mjadala.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Hoja yangu ni kwamba maneno hayo niliyoyaeleza yawekwe ili kulinda watu ambao wanaweza kutumia mamlaka yao vibaya kusumbua *private bodies* ambazo zinafanya shughuli zake. Kwa mfano, mtu anakwenda kuwadai habari bila utaratibu wowote akidai kwamba kuna maslahi ya umma waweze kulindwa kwa kuweka hayo maneno ambayo nayaleta na ambayo hayapingani na mantiki au azma nzuri ya kuwa na sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa hoja, Waheshimiwa Wabunge sijui mnaniunga mkono au ndiyo niko peke yangu? *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Naona haijaungwa mkono, tunaendelea.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3

**MWENYEKITI:** Tuanze na Mheshimiwa Profesa Tibaijuka halafu tutakwenda kwa Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hoja yangu ya kwanza haikuungwa mkono ilikuwa inaendana na hii ya pili, kwa hiyo, hii naitoa mezani.

**MWENYEKITI:** Sawasawa, ahsante. Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeleta mabadiliko kwenye hiyo *clause 3* ya tafsiri. Nimeona kwamba neno *third party* au mtu wa tatu limetumika zaidi ya mara tatu kwenye huu muswada lakini halijatafsiriwa ni kitu gani. Najua kwamba kuna baadhi ya nchi ambazo zimeshapitisha Muswada huu kuwa sheria ikiwa ni pamoja na Afrika Kusini kwa Afrika na Uganda ambapo nimeweza kuzipitia sheria zao na kuona wao wame-*interpret.* Kwa hiyo, nikafikiri kwamba sisi kama nchi ni lazima tujue huyo *third part* ni nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu pia imeelezwa katika Ibara ya 15(1) kuhusu mtu huyo wa tatu, kinasema katika kushughulikia ombi la kupata taarifa, mmiliki wa taarifa atachukua hatua zote za msingi za kumuarifu mtu wa tatu ambaye kumbukumbu yoyote ya taarifa iliyoombwa inamhusu. Kwenye kifungu cha 6(f) nacho pia kinamtaja, kwa mfano kinasema, *infringe commercial interests, including intellectual property rights of that information holder or a third party from whom information was obtained.* Nikadhani kuna haja kabisa ya sisi kujua huyu *third party* ni nani kwa kutafsiriwa na majukumu yake yajulikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo ilikuwa hoja yangu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Upande wa Serikali, Mheshimiwa Dkt. Possi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza labda niseme hivi, *definition* katika sheria, maneno hayatafsiriwi tu sio kwa sababu yametajwa mara nyingi ila yanatafsiriwa kwa sababu yanataka kutatua utata unaoweza kujitokeza. Katika muktadha wa kawaida kabisa wa sheria *third party* ni mtu yeyote yule ambaye sio *privy* katika *transaction* ambayo iko *involved*. Kwa hiyo, tunaona tukiileta hii, kwanza katika uandishi tu wa sheria ni *unnecessary* lakini pia inaweza ikatuingiza katika *gate keeping function* ya kuanza kuchagua nani anaingia nani anatoka kitu ambacho siyo dhamira ya sheria hii.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lyimo, umepata maelezo ya Serikali.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nakubaliana naye kwamba siyo lazima kila kitu kitafsiriwe lakini nasema kwamba suala la *third party* binafsi nadhani ni muhimu sana. Nasema hili kwa sababu ninazo sheria za nchi mbalimbali za hii *Access to Information* na jambo hilo hata wao siyo wajinga na wao pia wamelitafsiri ili watu waelewe hasa *third party* ni nini. Sielewi Serikali inaona kutakuwa na athari gani hiyo tafsiri ikiwekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bado nasimamia kwamba ni muhimu sana tujue *third party* ni kitu gani *according to* muswada huu. Kama Serikali bado inang'ang'ania msimamo wake, naomba tujadili suala hili.

**MWENYEKITI:** Ngoja waseme kwanza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapotunga sheria tukiiangalia mifano ya nje tunaitunga pia tukiangalia na mazingira halisi ya kwetu. Yawezekana hawa jamaa walivyo-*define third party* kulikuwa kuna kitu au kuna mazingira yoyote ambayo kwa namna moja au nyingine walikuwa wanataka kuya-*clarify* lakini kama nilivyosema katika sheria yoyote iwe ni ya ardhi, *contract* au kitu chochote, *third party* ni *any person who is not privy to the transaction,* anaweza akawa ni *natural person or a private body.* Kwa hiyo, sioni utata unakuja wapi katika suala hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Lyimo na mimi naelekea upande wa Serikali kwa sababu mimi kama mwanasheria, kwa sheria za Tanzania ukishasema tu hiyo *third party* inaeleweka wala haina matatizo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** *(Aliongea nje ya kipaza sauti).*

**MWENYEKITI:** Ngoja, ili tuelewane wote lakini kama wewe unadhani, kwa sababu hizo sheria unazozitaja sisi hatukupata bahati ya kuwanazo hapa. Sasa hatuwezi kuja na utaratibu…

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** *(Aliongea nje ya kipaza sauti).*

**MWENYEKITI:** Sawa lakini hatushtukizwi tunapotunga sheria na ndiyo maana tunakuwa wa wazi. Ulipoleta *schedule of amendment* yako hata hiyo unayoisema ungeiweka tu Serikali wakaiona, hakuna tatizo, ili na wenyewe waisome katika *context* nzima ya sheria husika; mazingira yao ni yapi na ya kwetu ni yapi lakini kama unaendelea, ahsante. Mheshimiwa Kangi Lugola.

**MHE. KANGI A. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hoja Mheshimiwa Susan Lyimo kwa mtazamo wangu ina mashiko kwamba tusipotafsiri hili neno *third party,* nina wasiwasi kwa upande wa Zanzibar ambako Mheshimiwa Waziri amesema kwamba sheria hii haitumiki Zanzibar lakini Wazanzibar ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa vile tumesema kwamba kila raia anayo haki ya kuomba apatiwe taarifa anaweza akawa Mzanzibar kwa sababu ni raia akaomba taarifa kwenye ofisi yoyote hapa Bara. Labda ni mwandishi wa habari yupo Zanzibar akaomba taarifa halafu akatoa habari kwenye gazeti akapotosha. Baada ya kupotosha kwenye sheria yetu hii inasema kuwa ni kosa kupotosha taarifa uliyopewa lakini Mzanzibari kwa sababu amepotosha na kosa limetendeka Zanzibar ambako sheria hii haitumiki maana yake sheria hii haitambana na upotoshaji umefanyika ndani ya mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tusipotafsiri hapa tunaweza tukapata shida Wazanzibar wakawa wanachukua taarifa kwa sababu ni raia wakapotoshea Zanzibar na sheria hii haiwezi ikawashtaki kwa sababu kosa walipotendea Zanzibar sheria hii haitumiki. Kwa hiyo, naona inawezekana msingi wa hoja yake imetokana na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, naona kwamba neno hili ni vyema likatafsiriwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa *AG*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine kwa kweli, hivi hili neno kweli lingetufaa lituweke hapa? Maneno ambayo yana asili hata ukisoma kwenye *dictionary* unapata maana ya *third party*. Tumetumia hili neno *third party on so many laws* halafu leo mnataka tutafsiri hapa *third party?*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Moja ya athari yake ni hii Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane ili tuelewane, unaacha nani na nani? Waziri amefafanua kwamba *third party* ni yeyote yule asiyehusika kwenye suala lile.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Hatutaki! Hatuwezi kutuwezi kutunga sheria ya hovyo namna hiyo.

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** *That is true!* Hatuwezi kupoteza muda wetu hapa kwa ku-*define third party* ambayo ipo kwenye sheria chungu nzima. Hata hii anayosema Mheshimiwa Lugola kifungu cha 5(4) si kimefafanua? *A person is citizen of the United Republic,* Mzanzibar ana haki hiyo na aki-*abuse* analazimika kama raia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Waheshimiwa Wabunge kwa nini tusiende kwenye mambo mengine zaidi ya maana? Hili suala Mheshimiwa aende atafute kwenye *dictionary third party* maana yake ni nini? Hatuwezi kuwa kila sheria tunatunga tunaweka *third party* maana yake ni nini. Sasa kila neno tulilotumia hapa tutoe tafsiri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba kushauri, Mheshimiwa Susan hoja yako ni ya msingi lakini Mheshimiwa Waziri amesema haijulikani kwamba hilo limetumika kwenye *context* ipi? Sisi tunatunga sheria itakayo-*apply* Tanzania, tumeshasema wahusika hapa ni akina nani, sasa unataka tu-*define* hapa? Leo unaanza hapa halafu baadaye unafungua tena, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Lyimo kwa maelezo ya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu na yale niliyoanza nayo mimi unasemaje?

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sijamuelewa kwa sababu nilikuwa namuona anafoka tu, sikuelewa anaongea nini? Kwa hiyo, sijui ameongea nini, walau Waziri nilimsikia lakini Mheshimiwa *AG* kwanza alikuwa hatumii *microphone,* kila mtu alikuwa anamshangaa, mimi simuelewi.

**MWENYEKITI:** Endelea sasa na hatua ya pili.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kazi kubwa ya Mbunge ni kutunga sheria kama ambavyo mpaka muda umeongeza na kila mtu ana uelewa wake. Kwa hiyo, ilikuwa ni kiasi cha kueleweshwa tukaona hiyo mantiki ya kutokuweka hiyo tafsiri ni nini lakini kwa kweli alivyoongea AG mimi

sikumuelewa. Niseme tu kwamba kama wameona hivyo ndivyo basi sawasawa tu.

**MWENYEKITI:** Hapana, sasa unakuwa na hasira. Haya ukizira basi. Wewe ndiyo umependekeza hayo nilikuwa nataka kufahamu kama unataka kuendeleza hoja yako maana wengine naona wanataka kuchangia lakini haijatolewa hoja, siwezi kwenda namna hiyo! Ndiyo maana nilikuwa nauliza unataka kuendeleza tu hoja hiyo au unakubaliana na maelezo ya Serikali.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna mwingine ambaye angependa kuchangia labda ingeweza kusaidia zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Susan Lyimo kama ambavyo iliongezewa nyama na Mheshimiwa Lugola. Kwa maelezo ya Waziri jana na maelezo ya wachangiaji wengi jana hasa kutoka upande huu, hii sheria pamoja na mambo mengine inamlenga mwananchi wa kawaida kabisa anayetaka kwenda kupata taarifa. Inamlenga mwananchi wa kawaida ambaye siyo mwanasheria ambaye hajui hayo maneno ambayo Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe anayasema na Dokta pale anayasema na Mheshimiwa Ummy anayasema kwa sababu wao ni wanasheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hoja hapa, kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali anakiri kwamba *third party* ni mtu mwingine yeyote ukiachia huyo mhusika, kuna shida gani haya maneno hata kama unadhani hayo maneno yaliyowekwa na Mheshimiwa Susan Lyimo yapo *complicated* yatafungua *pandora's box*, atoe tafsiri ambayo mtu mwingine ambaye hajasoma sheria akiona neno *third party* ambalo lime-*appear* kwenye maeneo mengi hapa hataona kizunguzungu. Kwa hiyo, mimi sidhani kama ni busara kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kufoka. Amepewa hiyo nafasi ili atueleze kwa utaratibu tumuelewe tukubaliane na hoja zake ama tusikubaliane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama dhamira ni ile ambayo ilisemwa na siyo vinginevyo, kwa sababu hatutarajii kwa mfano mwananchi wa kawaida anataka aangalie hii sheria inamsaidia nini aende akatafute mwanasheria amsaidie kutafsiri vitu ambavyo vinatakiwa vile *straight forward* ili ajue mipaka yake ya kisheria ni ipi na kitu ambacho anaruhusiwa na kitu ambacho haruhusiwi. Kwa hiyo, mimi naunga mkono na nimuombe Mwalimu wangu Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, kuna masuala yanahitaji ushabiki na masuala mengine yapo *straight forward*. Tafsiri ya *third party* ikitolewa hapa sidhani kama itakuwa na madhara yoyote ili mradi mtoe kwa matakwa yenu ambayo mnadhani yapo sahihi. Ni hayo tu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemuelewa Mheshimiwa Halima Mdee lakini nimuombe, sheria hizi tunavyotunga zinatupa nafasi ya kukua nazo, *this is our first experience*. Hivi kuna shida gani tukiona kuna ukakasi unakuja tutaileta tena kufanya *amendment*.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Ndiyo tunaanza *let us experience* hayo matatizo, maana kusema anaweza akatokea mtu mwishoni tutakuwa na sheria yenye *paragraph* zaidi ya 400 hapa. Mimi ningeomba tu kwamba hebu tuanze nayo hivi, ukitokea utata tutaleta mara moja hapa kuibadilisha na kuongeza *definition* hiyo.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Na ndiyo *spirit*. Jamani huwa nawaambia kila siku, uzuri au ubaya wa sheria ni pale unapoanza kuitumia na ndiyo maana nilipoanza kumwambia Profesa ilikuwa kwa *spirit* hiyo hiyo anayosema Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Lyimo sitaki kushawishi Kamati ya Bunge Zima lakini ningekuwa na-*draft* Muswada huu kwa hali tuliyofikia na kwa mapendekezo yako ningekuwa upande wa Serikali kwa sasa. Wajumbe, tunaendelea.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 4

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lyimo tusikie hoja yako ya mabadiliko.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nipo kwenye Ibara ya 4, *the objectives of this Act are,* kwa sababu lengo na madhumuni ya Ibara hii ni kuipa nguvu Ibara ya 18 ya Katiba yetu, kwa hiyo, nafikiri tuondoe kile kifungu (a) tuka-*replace* na hii ya kwangu ambayo inasema, *to give effect to Article* 18(d), ambayo kimsingi ndiyo inahusiana kabisa na taarifa kuliko ilivyokuwa inasema tu imetolewa na Katiba. Kwa hiyo, nadhani ni vema tukawa *specific* kwenye hiyo Ibara ili kuleta maana zaidi mtu akisoma anakuwa na uelewa zaidi kuliko kusema tu imekuwa *provided* na

Katiba. Kwa hiyo, niliona ilikuwa *too general* nikaenda *specific* kwenye *Article* ambayo inahusiana kabisa na suala zima la kupata taarifa.

**MWENYEKITI:** Lakini Ibara ya 18(d) ya Katiba haipo ndani ya Katiba?

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Cha ngapi?

**MWENYEKITI:** Ibara ya 18(d) ya Katiba haipo ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano?

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Ibara ya 18(d)?

**MWENYEKITI:** Ndiyo

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Imo ndiyo lakini nasema…

**MWENYEKITI:** Wao wanasema, *to give effect by citizens as provided for by the Constitution.* Tofauti yako na Serikali ni nini? Kwa sababu ile ya Serikali imebeba yote wewe unataka tu tuegemee kwenye Ibara ya 18(d). Mimi naona hii ndiyo imekaa vizuri. Unaafiki Mheshimiwa Lyimo?

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hatujaelewana, nimesema kwamba ya Serikali ipo *too general*, mimi nimeenda kwenye *specific* kwenye kipengele kinachohusiana na taarifa, *that is what I thought.* Kwa hiyo, kama unaona ya Serikali ibakie kwa sababu ni *more general* kwa Katiba nzima, *fine*.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 5

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 6

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mhehsimiwa Mwenyekiti, nimeleta mapendekezo katika hii *clause* ya 6(3) kwa ku-*delete paragraph* (d), hiki kifungu kimetoa tafsiri ya masuala mbalimbali ama taarifa zinazohusiana na masuala ya kiusalama. Kwenye (d) imeandika *foreign relations* na *foreign activities* yaani mahusiano ya nje ama shughuli za mambo ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nadhani kwa kuwa kifungu hiki kinahusiana na masuala ya usalama peke yake na kwa kuwa kifungu kinachohusiana na usalama kinachohusisha masuala ya mambo ya nje kimeshakuwa *covered* na (b), nadhani ni makosa kuweka mahusiano ya mambo ya nje ki-*general* na shughuli za mambo ya nje ambapo kinakuwa kipo *open-handed.* Kwa mfano labda mwananchi wa kawaida anataka taarifa ama ya kibiashara ama ya uwekezaji inayohusiana na India na Tanzania *obvious* ataandika Wizara ya Mambo ya Nje kwa taratibu ambazo zimewekwa kisheria ili kuweza ku-*seek those informations.* Kwa kuweka kifungu hiki ambacho kipo *too general* na wala hakisemi kabisa kinahusiana na masuala ya kiusalama kinaweza kikatumika vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mapendekezo yangu ni kwamba kifungu hiki kiondolewe na kikishaondolewa tu-*renumber* kama kawaida hizi *alphabet* kwa sababu (d) itakuwa imeshaondoka kwa hiyo *alphabet* zitapangwa tu kwa utaratibu wa kawaida. Kwa hiyo, ni suala *simple tu* kwa sababu halihusiani kabisa na masuala ya kiusalama, nadhani nimeeleweka.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa maelezo yako. Upande wa Serikali nani anatoa maelezo, Mheshimiwa Dkt. Possi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mazingira mawili hapa. Kwa hali ya sasa hatuwezi tukadhani tunaweza tukalinda usalama wa nchi yetu kwa kujiangalia sisi ndani lazima tunashirikiana na nchi nyingine na. Hata hivyo, mahusano ya kidiplomasia pia kwa upande mmoja au mwingine yanaweza yakawa na mahusiano ya kiusalama. *And after all* tafsiri hii haihusiani na mtu ambaye anataka kufanya biashara China na vitu vingine. *May be* ni *oversight or what* ya Mheshimiwa Mbunge lakini ukweli ni kwamba hatuna mpango wowote wa kukibadili.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana labda mpango wa kutokubadilisha kitu hata kama kinaonekana kipo wazi ndiyo upo. Kama ni hivyo, ni bora hata hizi *schedule of amendment* tusipoteze sauti zetu bure. Kwa nini nasema hivi?

Kifungu cha 6 kimeeelezea taarifa ambazo haziruhusiwi kutolewa kiujumla wake na taarifa ambazo haziruhusiwi kutolewa ambazo tumezungumza tokea jana ni taarifa zinazohusiana na masuala ya usalama wa taifa na hakuna mtu anayebisha. Vifungu vinavyoendelea vimeelezea mazingira mbalimbali ya taarifa. Kifungu cha (3) kimesema:-

*"For the purposes of paragraph (a) of subsection (2), information relating to national security includes-*

*(b) Foreign government information with implications to national security.*

*(d) Foreign relations or foreign activities.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *foreign relations na foreign activities* ni vitu ambavyo ni vipana mno. Hata hivyo, kwa kuwa kifungu kinasema masuala ya usalama tukiingiza hiki kifungu kesho amekuja Waziri wa Mambo ya Nje wa India amekutana na Waziri wetu wa Mambo ya Nje wanataka kuzungumza masuala ya biashara na fursa za kibiashara, anatokea Mtanzania wa kawaida huku, mfanyabiashara, anataka kwenda kuwekeza India kwa mfano, anataka kupata taarifa inayohusiana na mahusiano yetu na India ya kibiashara ama ya kiuwekezaji, hiki kifungu hapa ambacho kipo *too broad* kinaweza kikatumika ku-*block*. Sasa kama dhamira ilikuwa ni taarifa za kiusalama ndiyo maana nimesema imeshakuwa *covered* na (b) tusiingize vitu vingine kwa uchochoro wa *national security*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo yale masuala ya jana yaliyokuwa yakijadiliwa yatakuwa *proved* hapa kwa sababu *foreign relations* na *foreign activities is too broad*. Nashukuru Dokta, Profesa na *AG* wanajibu, ama watuambie tafsiri yao ya *foreign relations or foreign activities* ni ipi inapokuja hii sheria? Nadhani kitu kipo *straight forward,* kama dhamira ya kifungu cha 6 ilikuwa ni usalama wa taifa *then* (d) haitakiwi kuwepo hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunaleta *amendments* huku mlango umeshafungwa bora tujue mapema tusitumie *energy* nyingi hapa *for nothing*. Kwa sababu lile la Mheshimiwa Susan lilikuwa halieleweki, mmelikataa lakini kulikuwa hakuna sababu ya kukataa na hili mtalikataa wakati hakuna sababu ya kulikataa kwa sababu vitu vipo *straight forward*. Ni hayo tu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dokta Possi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napitia tu hapa, Mheshimiwa Mbunge angesoma *Article* hii pamoja na kifungu kidogo cha (2) pale inapoanza, *exempt information may be withheld* kwamba hii inaweza siyo *shall be withheld, so under the appropriate circumstances* hoja yake inaweza ikafanya kazi. Kwa hiyo, hamna haya ya kukukibadili hiki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa maelezo ya Serikali ni kwamba unapoanza na Ibara ya 6(1), *information requested under this Act shall,* unaenda nayo mpaka mwisho (a) na (b) halafu (2), *exempt information may* (yaweza) kutokutolewa kama utoaji wake utagusa haya na haya. Maana mwanzoni nilifikiri ulipokuwa unasema *foreign activities,* Mtanzania kwenda kuwekeza ndiyo ilikuwa *concern*

kwamba atanyimwa kwenda kuwekeza kwa sababu ya kifungu hiki, maana ni nini hasa. Mheshimiwa Halima Mdee tuelewane kwanza, ile tofauti ya *shall* na *may* huioni wewe katika vifungu hivi?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unapotaka kuingiza dhana tofauti ya *shall* na *may* katika mazingira haya, kwa sababu hiyo inampa *option,* kwa sababu itakuwa yule mtu anayetakiwa atoe taarifa ndiyo ataona kwamba *yes, it is not mandatory* anaweza akatoa ama asitoe. Sasa inapokuwa mazingira hayo ni mtu mwenyewe anaamua. Ndiyo maana nilisema, hivi vifungu vyote ambavyo moja kwa moja vinahusiana na masuala ya usalama sina tatizo navyo lakini hiki kipengele kimoja ambacho kiko *too broad,* hakina mahusiano yoyote na masaula ya usalama kwa sababu linalohusiana na masuala ya usalama kwa mambo ya nje limeshaelezwa hapa hakina haja ya kuwepo kwa sababu kikiwepo mtu anaweza kuzuia kwa sababu ni *discretion* yake kutoa ama kutokutoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama nilivyosema mwisho wa siku Bunge ndiyo litaamua. Kwa hiyo, tuhoji Bunge kama linaona hiki kifungu ambacho kiko *too broad* kwamba anayetakiwa kutoa taarifa anaweza aka-*take advantage of it* kwa sababu hajalazimishwa, hakina *link* yoyote na masuala ya *national security* na kikidumbukizwe hapa kinaweza kikawa uchochoro, watu wakataka kupata taarifa mbalimbali zinazohusiana na mahusiano ya mataifa mawili kuhusiana na mambo mbalimbali, yawe ya kibiashara, yawe ya kijamii, wakanyimwa hiyo taarifa basi liamue. Kwa hiyo, hiyo ndiyo *concept* yangu na iko *straight forward.* Ni wao wenyewe waamue ama kuchukua au kuacha lakini najua *deep down in their hearts* wameelewa kwa sababu wanajua hiki ni kikwazo cha mtu kuweza kupata taarifa kwa sababu mtoa taarifa ataamua mwenyewe kwa *discretion* yake kwa sababu sheria haimbani. Ni hayo tu.

**MWENYEKITI:** Basi ngoja nihoji Kamati kuhusu mapendekezo yako Mheshimiwa Halima Mdee.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tibaijuka.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika *clause* hii ya 6, nina mapendekezo katika kifungu cha (2)(a), ukurasa wa sita. Mimi nimeelewa kwamba sheria hii inahusu pia *private bodies* kama zimesajiliwa na sheria mbalimbali za nchi. Kwa mantiki hiyo nikaangalia (e) ambayo inasema ina-*involve unwarranted invasion of the privacy of an individual, other than an applicant.* Mimi napendekeza tuweke *an individual or a private body* kwa sababu *a private body* pia ina *right* ya ku-*enjoy privacy.* Labda nilieleza

vibaya naona sipati ushirikiano lakini *private legislation* ikionekana iko *too intrusive* kwenye *affairs za private bodies* itafukuza wawekezaji. Hawa wenzetu wengi wanapokuja wanaangalia *the legal framework* imekaaje, kama iko *too intrusive,* wanaona kwamba huwezi kwenda mahali ukafanya kitu yenyewe itawafukuza tu *automatically,* wanaangalia *legal framework* imekaaje. Kwa hiyo, nikafikiria kwamba hii *provision* ambayo inalinda *privacy* ilinde pia ya *private body* kusudi ziwe *protected* wa-*feel* kwamba hatumkomoi mtu tunaweka kitu kulinda maslahi ya Taifa. Hiyo ni *amendment* ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kosa kwenye *amendment* yangu, *it is subsection (2)* sio *subsection (1)(e), page six*. Nina-*introduce* neno, *just a simple word, or a private body* kusudi tunapo-*protect privacy* sio ya *individual* tu hata na *private bodies because they are legal entities* zinaweza kuwa na maslahi ya kutaka kulinda mambo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mengine, niendelee au nisimame hapo kwanza?

**MWENYEKITI:** Ile (d)?

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** (e).

**MWENYEKITI:** Ndiyo unataka kumalizia hapo?

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo (e), sijui kama naeleweka, niko *page six* kwa wale ambao wanaangalia kwa *page,* (e) inasema:-

*"Involve unwarranted invasion of the privacy of an individual, other than an applicant or a person on whose behalf an application has been made".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *my amendment would therefore say:-*

*"Involve unwarranted invasion of the privacy of an individual or a private body, other than an applicant or a person or a private body on whose behalf an application has been made".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu *there are these corporate bodies* tunazisahau, *they have their individual character,* wana mambo yake na *legal framework* inaonekana iko makini kama ina-*protect* pia *right* ya *private bodies.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa wasilisho lako. Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Possi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli *registered bodies* kisheria ni *legal persons* lakini katika muktadha wa haki za binadamu zilizopo katika Katiba mojawapo ikiwa ni uhuru wa faragha, hizi zinakwenda kwa mtu *by virtue of being a human being.* Ndiyo maana tuna *human rights* sio *persons rights* na kwa maana hiyo hii hapa ililenga ile *Article* 16 ya Katiba *and for that matter* kifungu hiki hakifanyiwi mabadiliko.

**MWENYEKITI:** Mheshimwiwa Tibaijuka, umemuelewa mtoa hoja?

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemuelewa mtoa hoja lakini nadhani na yeye ameelewa nachokisema kwamba sheria hii ikienda kama ilivyo hakuna mahali ambapo inaonekana iko *sensitive to the privacy of private corporate bodies* na mimi nataka kuwa *on record* kwamba *that is poor legislation.* Hatuwezi kusema kwamba hatuelewi suala hili, linaeleweka, kuna kampuni watu wana mambo yao *as long as* havunji sheria, haingilii maslahi ya Taifa anatakiwa kulindwa, kuiacha ikaenda hivihivi ni kosa. Sasa kama hakuna *support for it* twende nalo lakini lazima iwe *on record* kwamba ni kosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Haya, nawahoji mapendekezo ya Mheshimiwa Profesa Tibaijuka.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Tibaijuka.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani sana, bado sijamaliza *amendments* zangu chini ya *clause 6,* tumemaliza ya kwanza naomba niingie ya pili *under clause 6(6),* inasema:-

*"Any person who discloses exempt information withheld by the public authority in contravention of this Act, commits an offence and shall, on conviction, be liable to imprisonment for a term not less than fifteen years..."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaona *amendments* za Serikali inawezekana kwamba sisi hapa hatukuziona lakini kama Serikali haijarekebisha hiyo sheria mimi *amendment* yangu inakwenda hivi. Kwanza nafuta hayo maneno,

*withheld by the public authority,* nafikiria kwamba kuheshimu kwa mfano unafanya kazi kwenye…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa, hebu soma ukurasa wa pili wa marekebisho ya Serikali pale juu halafu ndiyo uendelee.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *my problem* hapa *I must admit,* tuko *constrained,* hatukupata marekebisho ya Serikali, ningeyapata yangesaidia labda imeshakuwa *overtaken by events*.

**MWENYEKITI:** Serikali kwenye eneo hilo inasema hivi:-

*"By deleting subclause (6) and substituting for it the following-*
*(6) Any person who-*

*(a) discloses exempt information, other than information relating to national security, commits an offense and shall, on conviction be liable to imprisonment for a term of not less than three years and not exceeding five years".*

Mheshimiwa Profesa Tibaijuka, unasemaje hapo, pamekaa vizuri.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo, *with that amendment* ya Serikali *then* tunaweza tukaendelea, ahsante.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 7

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 8

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 9

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Ibara ya 9 nimeomba yafutwe maneno miezi thelathini na sita ambayo yapo katikati ya maneno *than* na *after* na kuyabadilisha na maneno mwaka mmoja. Nimesema hivi kwa sababu kwa mtazamo wangu mimi, miezi sita ambayo ni miaka mitatu

ni mirefu mno lakini vilevile kwa mujibu wa kifungu cha 1 cha sheria hii kinasema sheria hii itaanza kutumika tarehe ambayo Waziri kupitia Gazeti la Serikali atatangaza. Sasa nafahamu hapa kwanza katika hatua ya kwanza tukishapitisha itaenda kwa Rais akiwa kama sehemu ya Bunge na yeye atapitisha baada ya hapo itakuwa *gazetted.* Tukisema tena kwamba baada ya kuwa *gazetted* tena tusubiri miezi mingine thelathini na sita ambayo ni miaka mitatu hawa watu waanze kutoa taarifa zao itakuwa hii sheria tukifika 2020 ndiyo inaanza kutumika. Sasa na *spirit* yenyewe na mbwembwe zote tulizokuwa tukijinasibu hapa kumbe inakuwa haina maana. Kwa hiyo, nilikuwa naomba, japokuwa naona Kiti pale mbele hakina ushirikiano sana, hii miezi sita…

**MWENYEKITI:** Unaiongea na Kiti, acha uchokozi. *(Kicheko)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Sawa mkuu. Miezi thelathini na sita ipunguzwe iwe mwaka mmoja au miezi kumi na mbili ili mchakato wa utekelezaji wa hii sheria uanze. Kwa hiyo, badiliko langu la kwanza la *clause* 9 kati ya mawili niliyoyaomba ni itoke *thirty six months* ije *one year* ili basi utekelezaji wake tuuanze ndani ya kipindi hiki cha miaka mitano. Ni hayo tu, sidhani kama lina *complications* zozote.

**MWENYEKITI:** Pendekezo la pili ni nini?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nimeomba yafutwe maneno, *and upon request,* ambayo yametokea katikati ya *comma* na herufi a. Nimeomba hivyo kwa sababu kwa uelewa wangu mimi hii sheria kuna hatua mbili. Hatua ya kwanza ni wajibu wa mwenye taarifa kutangaza taarifa ambayo imekuwa *covered* na hiki kipengele cha 9, naomba nikirejee kwa Kiswahili, kinasema hivi:-

*"Kila mmiliki wa taarifa, si zaidi ya miezi thelathini na sita, ambayo nimeomba iwe mwaka mmoja au miezi kumi na mbili, baada ya kuanza kutumika kwa sheria hii, baada ya kuombwa, atatoa kwenye Gazeti, tovuti au gazeti linalopatikana kwa wingi likiwa na:-*

*(a) maelezo juu ya aina, kazi na majukumu ikijumuisha majukumu yote ya kisheria ya maafisa wake;*
*(b) maelezo ya jumla ya aina za taarifa zinazopatikana kwa mmiliki wa taarifa huyo".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hiki kifungu…

**MWENYEKITI:** Twende ya Kiingereza sasa, tunatunga Muswada kwa Kiingereza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Sawa. Kwa Kiingereza sasa inasema:-

"*Every information holder shall, not later than thirty six months,* ambayo mimi nimeomba iwe *one year, after the commencement of this Act, and upon request issue a notice to the public in the Gazette, website or newspaper of wide circulation containing the following-*

*(a) description of its structure*
(b) *general description of categories of information held by such information holder*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nimeomba haya mabadiliko? La kwanza nimesema kwamba baada ya hii sheria kupitishwa sasa ndani ya hicho kipindi cha mwaka mmoja hao watu ambao sheria inawataka watoe taarifa kwenye hizo *website* zao, waelezee kuna shughuli za aina gani wanazozifanya ambapo ndiyo *spirit* ya Ibara ya 9, ili mwananchi sasa kama anataka kuja kuomba taarifa ajue anapokwenda kuomba taarifa atapata taarifa ya aina gani. Kwa hiyo, kuna hatua mbili, kuna hatua inayohusu watoa taarifa lakini kuna hatua ya pili ambayo inamhusu mtu anayetafuta taarifa, sasa hivyo ni vitu viwili ambavyo ni lazima tuvitenganishe. Kwa hiyo, ndiyo maana nikasema kwanza kusiwe na neno *upon request,* iwe ni wajibu watu ambao sheria hii imewataka wawe na jukumu la kutoa taarifa mara baada ya hii sheria kupitishwa katika hatua zote na kutangazwa basi waweke kwenye *websites* zao wanatoa ama wanashughulika na vitu gani ili kama mkulima kule Njombe anataka taarifa za tumbaku ajue hizi taarifa za tumbaku katika vyombo hivi nitaomba pale. Sasa tukisema *upon request* nani anayefanya hayo maombi, ni Serikali mtakaoomba…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Naona Mwalimu wangu ametikisa kichwa nadhani amenisomasoma kidogo.

**MWENYEKITI:** Ngoja kidogo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Wewe ni mwanasheria, tunatunga sheria hapa, inaanza kusema hivi, *every information holder shall, not later than thirty six months after commencement of this Act, and upon request.* Kwa hiyo, kuna *situations* mbili hapa usiziunganishe, kuna ile ambayo sasa kile ambacho kitatakiwa kufanyika lakini pia na pale wanapoombwa watoe. Ukishaondoa hayo inakuwa tofauti na ilivyokusudiwa, ndiyo maana nimekusoma haraka sana, umenielewa Mheshimiwa Halima? Umeelewa kwanza maelezo?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimekuelewa…

**MWENYEKITI:** Namna ya kuisoma, *comma* hizo zina maana sana katika utungaji wa sheria.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeelewa maelezo yako lakini naomba Mheshimiwa Waziri apewe nafasi ajibu usimsaidie, ajibu kwa sababu alinielewa, kuna mazingira mawili tofauti. Kuna mtu ambaye ana taarifa zake na kuna huyu wa pili ambaye anatakiwa akaombe taarifa, kwa hiyo 9 na 10 vikisomwa kuna *contradiction.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria!

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna vitu viwili na ningemuomba Mheshimiwa Mdee tukubaliane basi. Kuna suala la miezi thelathini na sita, hata mimi naliona ni refu lakini tulifikia hapo baada ya kukaa na wataalam kuangalia utekelezaji wake. Tulikuwa tumeangalia tuna kipindi tunahitaji pia kufanya *mass awareness* wajue haki waliyonayo ili kila mtu aweze kufaidika na hii haki lakini pia kuna maandalizi ya kibajeti ili kila mtu aweze kikidhi hiyo haja.

Tatu tuliangalia tu ni kipindi gani ambacho hatuwezi kuwa *frustrated* tukiwaambia watu wote wakawa tayari, tukafikia hiyo miezi miezi thelathini na sita. Hata hivyo, ukikubali tui-*maintain* hiyo maana itatupa *comfort* sana kila idara ya Serikali, kila mtu anayehusika awe tayari basi hilo neno *upon request* na hata mimi nilikuwa naona kama *may be* tunatoa *comfort* mno kwa upande wa vyombo vya Serikali, nimemuelewa Mheshimiwa Mdee *may be* tukaondoe basi kale lakini hebu tuachie hii miezi hawa jamaa wahangaike maana tukiwapa miezi miezi kumi na mbili nina uhakika tutashindwa *completely* kufikia hiyo hali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Ndiyo, nakubaliana na Mwalimu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kwa maana ya kuondoa *and upon request*?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge eneo hili la Muswada linafanyiwa marekebisho kwenye Ibara ya 9(1) kwa kuondoa maneno hayo matatu, '*and upon request*'.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 10

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tibaijuka naomba uwasilishe mapendekezo yako ya mabadiliko.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuona marekebisho ya Serikali yamekidhi yale yaliyokuwa yananitatiza, kwa hiyo, naondoa pendekezo langu.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 11

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 12

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 13

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 14

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 15

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 16

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 17

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Tibaijuka.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Katika Ibara hii ya 17 nina marekebisho kwenye kifungu cha (3), napendekeza kwamba tuongeze kipengele ambacho kinasema:-

*"Would involve inordinate huge cost or time to the information holder"*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kinalinda yule ambaye anatoa taarifa lakini pia nimeona kwamba pamoja na nia zetu nzuri kutoa taarifa na kuweka taarifa kuna gharama zake. Nikafikiria kwamba hapa tuboreshe kwa kuongeza, *after (c)* tunaweka (d) ambayo inasema:-

*"Would involve inordinate huge cost or time to the information holder"*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hiyo sasa ambayo ni (d) inakuwa (e). Na-*introduce* kipengele cha kuhakikisha kwamba tuko *cost conscious* kwa sababu anaweza kuja mtu anadai vitu ambavyo kimsingi gharama yake haitekelezeki kwa yule ambaye anatakiwa kutoa taarifa hii. Hii yote siyo kuzuia kazi hii kufanyika ila kulinda sasa haki za wale ambao wanatakiwa kutoa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Upande wa Serikali mna maelezo kwa hoja hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, *of course section* hii kuhusiana na *form* ya taarifa ililengwa hasa kwa watu wenye ulemavu au mtu ambaye kwa namna moja au nyingine asingeweza kuipata *information* katika hali inayozuilika lakini hata tukiangalia muktadha wa *Persons Disability Act*, Na. 9 ya mwaka 2010 suala la *reasonable accommodation* huwa linaendana na gharama pia. Kwa hiyo, nafikiri pendekezo lake pia ni sahihi kwa sababu haitobadili wala haitonyima fursa watu wenye ulemavu kupata taarifa, tunaliafiki.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Bunge Zima Kifungu hicho kinaafikiwa pamoja na marekebisho yaliyowasilishwa na Profesa Tibaijuka.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 18

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mdee.

**MHE. HALIMA J.MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Ibara ya 18(2) nimependekeza yafutwe maneno: "Be *liable to imprisonment for a term not less than five years*" ambayo yapo baada ya maneno, "*conviction*" na *comma* na kuya-*replace* na *maneno "be liable to imprisonment for a term not less than two years but not exceeding five tears*".

Mheshimiwa Mwenyekiti nimeleta hoja hii kwa sababu hiki kifungu kikiachwa kama kilivyo kinaweza kikaua ile dhamira ya kurekebisha mtu na kutengeneza mazingira ya kukomoana. Kwa sababu unaposema mtu afungwe kifungo kisichopungua miaka mitano maana yake mtu anaweza akafungwa miaka kumi, miaka kumi na tano, miaka ishirini na hata ile *spirit* ya kile kifungu ambacho Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe kilikuwa kina *sentence* kubwa sana cha miaka kumi na tano mpaka ishirini mlichokibadilisha na kukishusha chini nadhani lazima kijengwe katika misingi hii. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri maneno hayo yafutwe yanayoashiria muda usiopungua miaka mitano na yawekwe muda usiopungua miaka miwili lakini isizidi miaka mitano. Kukiwa hakuna *limit* tunaruhusu watu waweze ku-*abuse* nafasi zao na watu wanaweza wakaumizwa. Kwa hiyo, dhamira ilikuwa ni hiyo tu Mwenyekiti kwa sababu hiki kifungu hakijakaa vizuri kabisa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Profesa Tibaijuka.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kama alivyosema Mheshimiwa Mdee na mimi nimepata ukakasi kuhusu hii adhabu ambayo imeonekana imeanza juu mno. Kwa hiyo, mimi mapendekezo yangu ni kwamba adhabu isiwe chini ya mwaka mmoja lakini nimependekeza kwamba isizidi miaka kumi. Maana makosa haya yanaweza yakatofautiana, athari zinaweza zikatofautiana kwa hiyo ndiyo nimeweka *range* ya mwaka mmoja mpaka miaka kumi kutoa uhuru kulingana na lile kosa maaana makosa haya yanaweza yakatofautiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naungana naye kabisa kusema kwamba katika mambo haya hizi ni *penitentiaries*, tunataka ziwe *deterrent* siyo kutaka kujaza watu magerezani. Tunataka kuweka sheria ambazo ni *deterrent,* mtu anajua kwamba jambo hili siyo sahihi unaweza ukafungwa lakini sasa kufungwa kwenyewe kuanzia miaka mitano na kuendelea inaoneka iko *excessive*. Kwa hiyo, mimi napendekeza mwaka mmoja hadi kumi, mahakama zinakuwa na nafasi ya kuangalia uzito wa kosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mwaka mmoja hadi kumi na mwingine miaka miwili hadi mitano, Serikali.

**WAZIRI WA SHERIA NA KATIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewasikiliza wote, Mheshimiwa Mdee na Mheshimiwa Profesa Tibaijuka. Nimuombe dada yangu Mheshimiwa Tibaijuka ambaye hivi karibuni tu ameipa heshima nchi yetu kwa kupata tuzo ya Kimataifa, hebu ile *proposal* yake yeye akubali tu, wote tukubaliane na *proposal* ya Mheshimiwa Halima Mdee ambayo ukiangalia haipishani sana na ile ya Serikali kwa sababu tumekuwa tunashusha kote na ile nyingine kwa mfano ya *national security* tumeipeleka kwenye Sheria ya *National Security* yenyewe. Ile ya miaka miwili mpaka mpaka mitano hatuoni kama litakuwa *gap* kubwa sana lakini mwaka mmoja mpaka kumi ningeomba tu Mheshimiwa Profesa atumie tu *profesiory discretion* yako kukubaliana na sisi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali kwamba ya Mheshimiwa Mdee iko sawa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wajumbe kifungu cha 18(2) kama kilivyorekebishwa kupitia marekebisho ya Mheshimiwa Halima Mdee kinaafikiwa?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 19

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza, nafurahi kwamba Serikali ilisikia kilio cha Wabunge wengi pale ambapo walikuwa wamefanya Waziri ndiyo mwenye maamuzi ya mwisho na wakaleta marekebisho. Hata hivyo, katika marekebisho yao nilikuwa naomba na mimi niweke rekebisho kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kwamba *justice delayed is justice denied.* Kwa hiyo, nadhani pale mwisho kwenye yale marekebisho ya Serikali baada ya maneno, "*High Court for review*" tuongeze maneno, "*within thirty days*" ili sasa mtu aweze ku-*appeal.* Tukiiacha kama ilivyo naona kama huyu mtu atapata shida sana. Anaweza akakaa mwaka, miaka, kwa hiyo, nikadhani lazima tuweke *timeline* ili huyu mtu aweze kupeleka malalamiko yake *High Court.*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wajumbe, ili tumuelewe Mheshimiwa Susan Lyimo, naamini wote tuna *schedule of amendment* ya Serikali, ukurasa wa 3, ndiyo maana ametumia *in amended clause* 19(4), mwanzoni nilikuwa sijampata sasa nimempata. Sasa wote muisome hiyo ndiyo muelewe anachotaka kusema hapo. Baada ya maelezo hayo Serikali mna-*react* vipi. Mheshimiwa Dokta Possi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nieleze tu kitu kimoja, hapa ni suala la mtu ku-*review* (kuomba marejeo) *of administrative action in court*. Tukiweka siku thelathini hatari yake ni nini? Zikipita siku thelathini huyu mtu hawezi kwenda tena Mahakamani mpaka aanze mlolongo mwingine mrefu wa kuomba *application for limitation* na kadhalika. Tusipoweka siku thelathini huyu mtu atakuwa *protected* na sheria nyingine inayohusiana na masuala ya muda katika *application of judicial review* ambayo nafikiri itakuwa ni nzuri zaidi kuliko hii ambayo tutaiweka ya *thirty days.* Kwa hiyo, nafikiri tuiache jinsi ilivyo ili sheria nyingine inayohusiana na *application for prerogative orders* iendelee.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 20

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 21

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho ya Serikali)*

Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. THEONIST RUHILABAKE - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba kamati ya Bunge zima imemaliza shughuli yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria ya Upatikanaji wa Taarifa ya Mwaka 2016 *(The Access to Information Act, 2016),* kifungu kwa kifungu na kukubali pamoja na marekebisho yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imetolewa na imeungwa mkono sasa itabidi niwahoji muiamue.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NDG. ZAINAB ISSA - KATIBU MEZANI:**

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kutunga sheria ya haki ya kupata taarifa, kuanzisha wigo wa taarifa ambazo umma unazo haki ya kupewa, kukuza uwazi na uwajibikaji wa wamiliki wa taarifa na kuweka masharti mengine yanayohusiana na hayo (*A Bill of an act to provide for access to information, define the scope of information which the public has the right to access, promote transparency and accountability of information holders and to provide for other related matters).*

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 91 ya Kanuni za Bunge, hatua hii ndiyo inachukuliwa kwamba Bunge limeupitisha rasmi Muswada huu wa Sheria ambao ulikuwa mbele ya Bunge ili ufuate hatua sasa ya kwenda kwa Mheshimiwa Rais kama sehemu ya pili ya Bunge kupata kibali cha Muswada huu.

Waheshimiwa Wabunge, niwashukuru sana tangu jana kwa kazi nzuri mliyofanya lakini niwashukuru zaidi kwa kazi mliyoifanya jioni ya leo kwenye Kamati ya Bunge Zima. Nawapongezeni sana na ndiyo kazi sasa ya kutunga sheria.

Mimi nimeshukuru sana mmefika wote mnaona hakuna *bipartisanship* katika masuala ya sheria. Mmenyoosha maeneo mengi yamekaa vizuri na sheria hii itakapoanza kutumika kama nilivyosema tutaona maeneo mengine labda hayajakaa vizuri, Serikali au Wabunge wenyewe kupitia Hoja Binafsi mnaweza mkafanya marekebisho lakini huo ndiyo utungaji sahihi wa sheria za nchi. Nawashukuru sana na nawapongeza sana na muendelee hivyo. *(Makofi)*

Nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe na timu yake, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Possi wametusaidia sana katika hili. Naelewea ulikuwa ni Muswada mzito kwa sababu ya *nature* na historia yake. Nawashukuru sana kwamba tumeweza kuona fursa hii na kuitumia vizuri. Nawashukuru Serikali kwa kazi hiyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo moja tu. Kesho tarehe 8 Septemba, 2016, saa 7.30 mchana, Ukumbi wa Msekwa kutakuwa na semina kwa Wabunge wote kuhusu kazi za Benki ya Amana Tanzania *(Amana Bank)*, wote mnakaribishwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kazi kubwa mliyofanya na kwa kujituma na Watanzania wanawashukuru sana, sasa naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.19 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 8 Septemba, 2016, Saa Tatu Asubuhi)*